# Nipashe

Jumamosi Agosti 24, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580005

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ww.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US






## Majaliwa amweka DED pabaya, ataka taarifa za utendaji wake

UKURASA 4

UKURASA 13



# Mawakili 14 wa serikali wamkabili Lissu mahakamani

• **Ni** katika kesi ya kupinga kuvuliwa ubunge, waongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali, wataka itupwe kisa... *Uk.2*



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Dunia (WB), Kanda ya Afrika, Anne Kabagambe (wa pili kushoto), akiangalia ujenzi wa Reli ya Kisasa kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR), alipotembelea kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro, jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Reli, Mhandisi Felix Nlalio. **PICHA: WFM**

## Majeruhi wa moto waanza mazoezi

UKURASA 3

## Kipenga uchaguzi serikali za mitaa chapulizwa rasmi

UK. 2

**MICHEZO** **YANGA YAACHIWA MJI, SIMBA WAITANA** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mawakili 14 serikali wamkabili Lissu

**Na Hellen Mwango**

JOPO la Mawakili 14 wa Serikali wakiongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Clement Mashamba, wamewasilisha hoja nane za kupinga maombi ya Mbunge wa zamani wa Singida Mashariki (Chadema), Tundu Lissu, kwamba hayana mashiko kisheria kwa kuwa aliyemwakilisha kuyafungua hana mamlaka kufanya hivyo.

Jopo hilo kwa nyakati tofauti limeomba maombi hayo yatupiliwe mbali na mlalamikaji alipe gharama za kesi dhidi ya walalamikiwa ambao ni Spika wa Bunge la Tanzania, Job Ndugai na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Pingamizi hilo lilisikilizwa jana katika Mahakama Kuu kanda ya Dar es Salaam chini ya Jaji Sirilius Matupa.

Dk. Mashamba alidai kuwa walalamikiwa wamewasilisha pingamizi lenye sababu nane kupinga maombi yaliyowasilishwa na Lissu kupitia mawakili wake, Peter Kibatala, John Mallya na Jeremiah Mtobesya.

Alidai kuwa katika sababu hizo nane, ndani yake kwa ujumla kuna hoja nne ambazo kwa nyakati tofauti zitawasilishwa na mawakili wenzake wa serikali na pale inapohitajika atasaidia.


Alizitaja hoja hizo nne kuwa ni kuhoji kwanza, mamlaka ya mahakama kusikiliza maombi kama yalivyowasilishwa, pili, kama mleta maombi ana uwezo wa kufanya hivyo, tatu kama maombi hayo yaliwasilishwa katika mahakama yenye mamlaka na nne, kama nafuu zilizoombwa ni sahihi kutolewa na mahakama hiyo.

Akianza kuwasilisha hoja, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abubakar Mrisha, alidai maombi yaliyowasilishwa mahakamani hayana nguvu kisheria kwa sababu maombi au mashauri yanapofikishwa mahakamani lazima yawe yamezingatia vigezo sita.

Mrisha alidai kuwa kigezo cha kwanza kama maombi yaliletwa ndani ya miezi sita baada ya jambo husika kutolewa uamuzi, pili, mwombaji awe anaelewa vizuri shauri, uamuzi uwapo kisheria, iwe hakuna namna nyingine ya kufanya kuhusu uamuzi huo, kama mahakama itasikiliza na kuona kuna haja ya kutoa uamuzi na sita, maombi yanatakiwa yawe katika nia njema na wala si kwa kupotosha au kuwa na lengo la kujinufaisha.

" Mtukufu Jaji, maombi yaliyopo mbele yako yametimiza kigezo kimoja ambacho ni kuyawasilisha maombi ndani ya miezi sita. Ukitazama vigezo vitano vimekose-

INAENDELEA UK 8




Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Uwekezaji, Dorothy Mwaluko (wa pili kulia), akipokea mfano wa hundi ya Sh. milioni 8, kutoka kwa Naibu Balozi wa China hapa nchini, Xu Chen, jijini Dar es Salaam jana, kwaajili ya kusaidia majeruhi wa ajali ya moto, wanaoendelea na matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Kulia ni Mratibu wa Huduma za Dharura na Maafa, Dk. Christopher Mnzara na Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara ya China hapa nchini, Zhu Jin Feng. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Msamaha wagonjwa waitesa Muhimbili

**Na Mary Geofrey**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa (MNH), Prof. Lawrence Museru, amesema hospitali hiyo inatumia kati ya Sh. milioni 500 na 600 kila mwezi kugharamia matibabu kwa wagojwa wasio na uwezo, maarufu wagonjwa wa msamaha.

Ili kukabiliana na changamoto hiyo, mkurugenzi huyo amewataka Watanzania kujiunga na bima ya afya ili kuwa na uhakika wa matibabu.

Prof. Museru aliyasema hayo jana wakati akikabidhiwa Sh. milioni tano na Wakili Albert Msando kwa ajili ya kulipa deni la matibabu ya marehemu Sabina Loita (52) alilokuwa anadaiwa mtoto wake na MNH.

Agosti 11, mwaka huu, Rais John Magufuli alitembelea MNH kuwajualia hali majeruhi 46 wa ajali ya moto iliyotokea mkoani Morogoro Oktoba 10, mwaka huu na kukutana na mama aliyemlilia, akidai mwili wa mama yake umezuiwa hospitalini hapo kutokana na kudaiwa kiasi hicho cha fedha ambazo aliahidi kuzilipa.

Prof. Museru alisema mbali na mama huyo, kuna idadi kubwa ya wagonjwa ambao wanasemehewa madeni yao kutokana na kukosa uwezo wa kulipa.

"Leo (jana) tumepokea Sh. milioni tano kutoka kwa wananchi waliowakilishwa na ndugu yetu Wakili Msando, siyo tu mama huyo, wapo wagonjwa wengi wanashindwa kumudu gharama za matibabu.

"Ni muhimu kuwahamasisha wananchi kutumia bima ya afya ili kuipunguzia mzigo hospitali yetu," Prof. Museru alisema.

Mkurugenzi huyo alisema tayari walishamwandikia barua Rais John

INAENDELEA UK 8

# Kipenga chapulizwa uchaguzi wa mitaa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KIPENGA cha uchaguzi wa serikali za mitaa 2019, kimepulizwa rasmi baada ya Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kutangza utafanyika Novemba 24, mwaka huu.

Ofisi hiyo imewataka Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa kuhakikisha wanazingatia miongozo na kanuni za uchaguzi huo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alitangaza rasmi kuanza kwa mchakato wa uchaguzi huo jana jijini hapa.

Alisema uchaguzi huo unaongozwa kwa Kanuni za Uchaguzi wa Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Ngazi ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa katika Mamlaka za Wilaya na Mamlaka za Miji, Matangazo ya Serikali Namba 371, 372, 373 na 374 ya Mwaka 2019.

Alisema upigaji wa kura utaanza saa mbili asubuhi hadi saa 10 kamili jioni huku akitaka kuwapo na amani na utulivu kipindi chote cha uchaguzi huo.

"Utakuwa ni uchaguzi bora kabisa ambao umeziba mapengo yaliyokuwa yamejitokeza katika uchaguzi uliopita kutokana na mchakato wa uchaguzi kushirikisha wadau wote vikiwamo vyama vyote vya siasa," Jafo alisema.

Alitaja nafasi zinazogombewa kuwa ni Mwenyekiti wa Kitongoji wa Mamlaka za Miji Midogo, Mwenyekiti wa Mtaa, Kijiji, wajumbe wa kamati ya mtaa na wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji.

"Kwa mujibu wa kanuni hizi, kura zitapigwa kwa kutumia karatasi maalum za kupigia kura ambazo zitatakiwa kutumbukizwa katika masanduku maalum ya kupigia kura.

"Wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi watatakiwa kuwa wanachama na wadhaminiwe na vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu," Jafo alisema.

Kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi huo, maombi ya uangalizi wa uchaguzi yatafanyika Agosti 27 hadi Septemba 16 na yatatumwa kwa Katibu Mkuu Tamisemi.

"Uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi utafanyika Septemba 2-9, tangazo la majina ya mipaka ya vijiji na vitongoji Septemba 13, uteuzi wa wasimamizi wasaidizi na wasimamizi wa vituo Septemba 16-22.

"Uandikishaji wapiga kura utafanyika Oktoba 8-14, Kubandikwa kwa orodha ya wapiga kura Oktoba 15, ukaguzi wa orodha ya wapiga kura Oktoba 15-21, Pingamizi kuhusu uandikishaji wapiga kura Oktoba 15-21, Uamuzi kuhusu Pingamizi Oktoba 21-22, Kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa pingamizi Oktoba 21-23 na uamuzi wa rufaa Oktoba 21-26," alisema.

Jafo aliongeza kuwa kukoma kwa viongozi walioko madarakani kutakuwa Oktoba 22, kuchukua fomu za kugombea Oktoba 29 na kurejesha ni Oktoba 29 hadi Novemba 4.

"Uteuzi wa kamati za rufani utafanyika Oktoba 29, uteuzi wa wagombea Novemba 5, uwasilishaji wa mapingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea Novemba 5-9, uamuzi wa pingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea Novemba 5-7, kukata rufaa kuhusu pingamizi la uteuzi Novemba 5-9," alisema.

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# Majeruhi lori la mafuta sasa waanza mazoezi

**Na Mary Geofrey**

WAKATI idadi ya watu waliopoteza maisha kufuatia ajali ya lori la mafuta mkoani Morogoro Agosti 10, mwaka huu, ikifika 101, majeruhi watatu wameimarika kiafya na wameanza kufanya mazoezi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa MNH, Aminiel Aligaesha, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema majeruhi wengine 11 wapo katika chumba cha uangalizi maalum (ICU) wakiendelea kupatiwa matibabu na wengine watatu wapo wodi za kawaida.

"Hawa majeruhi watatu wapo wodi ya Sewahaji wakiendelea kupatiwa matibabu na hali zao zinaendelea vizuri na tayari wameshaanza kufanya mazoezi ya kunyoosha viungo," alisema.

Aligaesha alisema majeruhi wengine walioko ICU, wanaendelea na matibabu na kwamba wataalamu wao wanahakikisha wanafanya kila linalowezekana kuokoa maisha yao. Alimtaja aliyefariki dunia jana alfajiri kuwa ni Sadick Buganga (32). Alisema Buganga alipoteza maisha wakati akipatiwa matibabu na kufanya idadi ya vifo kufika 33 kati ya majeruhi 47 waliopokelewa hospitalini hapo Agosti 10, mwaka huu.

Aligaenda alisema hospitali hiyo inaendelea na jitihada za kuhakikisha inaokoa maisha ya majeruhi wengine waliobaki kwa sababu ina wataalamu na vifaa tiba vya kutosha.

Majeruhi hao walipatwa na baa la kuungua kwa moto baada ya lori lililokuwa limebeba tangi la mafuta ya petroli, kuanguka eneo la Msamvu Itigi mkoani Morogoro na baadaye kulipuka wakati baadhi ya wananchi wakichota mafuta yaliyokuwa yanamwagika.

Tayari serikali imeshaunda tume ya uchunguzi kuhusu tukio hili, ikitaka kufahamu kama kuna taasisi haikuwajibika ipasavyo katika utekelezaji wa majukumu yake kuhusiana na tukio hilo lililoua watu wengi.




Wanafunzi wa Shule ya Msingi Bongoyo, iliyopo Oysterbay, jijini Dar es Salaam, wakijisomea katika maktaba ya kisasa iliyokarabatiwa kwa msaada wa Korea Kusini, shuleni hapo jana, ikiwa ni maandalizi ya mitihani ya darasa la saba. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Kigogo CCM atamani kurejea kufundisha

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amesema siku moja atarudi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kuendelea na kazi ya kukuza maarifa.

Aliyasema hayo juzi wakati akizindua mradi wa kuwasha taa za barabarani Mtaa wa Chief Kunambi. Taa hizo zinatumia nishati ya jua.

"Hata mimi niliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kigoda cha Mwalimu wakati nikiwa chuoni hapa, lakini kwa sasa nipo kwenye siasa, nipo likizo na kila siku nafikiria kurudi hapa kufundisha.

"Mungu akinijalia ipo siku nitarudi hapa kuendelea na kazi ya kukuza maarifa," Dk. Bashiru alisema.

Alieleza kuwa anakikumbuka chuo hicho katika maisha yake, akikumbusha kuwa mwaka 1997 alipokuwa mwanafunzi wa mwaka wa kwanza chuoni hapo, kulikuwa na uhaba mkubwa wa makazi ya wanafunzi.

Alisema kipindi hicho waliunda cheo cha 'cumpus' ambacho hakikuwapo na lengo kuu lilikuwa ni kuanzisha harakati za ujenzi wa mabweni ya wanafunzi na yeye kuwa Rais.

Alisema harakati hizo zilizaa matunda na kufanikisha kujengwa kwa mabweni ya wanafunzi katika eneo la Mabibo jijini.

Dk. Bashiru aliutaka uongozi wa UDSM wakati wakisherehekea kumbukizi ya kuanzishwa kwa chuo hicho Oktoba 25, mwaka huu, waendeshe pia matukio ya kitaaluma ya kuunga mkono juhudi za viongozi wa Jumuiya ya Nchi Kusini mwa Afrika (SADC) za kuhakikisha Zimbabwe inaondolewa vikwazo.

"Oktoba 25, mwaka huu, ninajua ni kumbukumbu ya kuanzishwa kwa UDSM, tarehe hiyo pia imepangwa na wakuu wa SADC iwe ni siku ya kutoa tamko kwa mataifa ya Ulaya kuiondolea vikwanzo Zimbabwe, niwaombe na nyie mshiriki katika mpango huo, siyo kwa kupiga kelele, bali kwa kuendesha matukio ya kitaaluma," Dk. Bashiru alishauri.

Kigogo huyo wa CCM pia aliwataka wenyeviti wa Kigoda cha Mwalimu Nyerere kutenda haki kwa kukuza maarifa kupitia jina la Mwalimu Nyerere.

Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. William Anangisye, alisema mradi huo wa taa umegharimu Dola za Marekani 49,300 (Sh. milioni 113) ukitekelezwa na Kampuni ya Stecko iliyosimika nguzo 36 za taa.

Alisema taa hizo zina uwezo wa kufanya kazi kwa saa 50,000 bila ya kubadilishwa na zilianza kuwekwa Juni hadi Julai mwaka huu.

"Taa hizi ni za kisasa, zinajiwasha na kujizima zenyewe ifikapo asubuhi, mradi huu ulikuwa ni wazo la Dk. Bashiru ambalo Ubalozi wa China ulilifadhili," Prof. Anangisye alisema.

Aliongeza kuwa kujengwa kwa taa hizo kutaimarisha ulinzi na usalama katika mtaa huo na zitapunguza gharama za umeme kwa kuwa pesa zilizokuwa zinatumika kulipa Shirika la Umeme (Tanesco), sasa zitatumika kwa mambo mengine muhimu.

Balozi wa China nchini, Wang Ke alisema: "Tulipokea ombi la kujenga taa kutoka kwa Dk. Bashiru Ally na Prof. William Anangisye, nilipotembelea ni kweli nikaona kuna giza, nikaona kuna umuhimu wa kuweka taa."

# Vigogo wa halmashauri watimuliwa bungeni

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

OFISI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG) imeagizwa kufanya ukaguzi maalum wa upotevu wa zaidi ya Sh. bilioni tatu ndani ya miezi mitatu katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyangh'wale mkoani Geita.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Abdallah Chikota, baada ya kufanya mahojiano na viongozi wa halmashauri hiyo kuhusu hoja za ukaguzi za CAG kwa mwaka wa fedha 2017/18.

Alisema waliamua kuwatimua vigogo wa halmashauri hiyo kutokana na kushindwa kujibu hoja zilizoibuliwa na CAG na kwa kiasi kikubwa ripoti waliyopelekewa na ofisi ya CAG imejaa ubadhirifu.

Chikota alisema pamoja na kwamba kuna watumishi ambao wapo ndani na wengine kesi zao ziko mahakamani, bado kuna wengine wako nje, hivyo kuna haja CAG afanye ukaguzi huo maalum.

"Wengine wapo nje kwa sababu hawakufanyiwa ukaguzi ili nao wajumuishwe na kuchukuliwa hatua," Chikota alisema.

Alibainisha kuwa kati ya fedha hizo, kuna vitabu 50 vya vyanzo taarifa zake hazikuwasilishwa.

"Kuna hati za malipo zenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni moja hazikuwasilishwa, kuna uhamisho wa fedha bila kuonyesha shughuli zilizofanyiwa kiasi cha Sh. bilioni 1.7, malipo yasiyo na viambatanisho Sh. milioni 339.7," alisema.

Chikota pia alieleza kuwa Sh. milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya hazionekani na kituo hakijajengwa huku akisisitiza halmashauri hiyo imekuwa na changamoto ya kuchelewa kukamilisha miradi ya maendeleo.

"Kuna fedha za P4R kwa shule za sekondari kiasi cha Sh. milioni 576 zimetumika nje ya malengo yaliyokusudiwa, fedha kwa ajili ya mradi wa maji wa Sh. milioni 74.1 ambazo taarifa ya benki inaonyesha Sh. milioni 71.1 hazipo," alisema.

Aliongeza kuwa kwa kiasi kikubwa halmashauri hiyo haiwatendei haki wananchi wake maana fedha zilizoibwa ni za miradi ya maendeleo.

Alisisitiza kuwa watendaji hao wamekiuka maadili ya utumishi wa umma na kuamua kuzitafuna fedha hizo ambazo kati yake, Sh. bilioni 1.9 ni za miradi, Sh. milioni 700 zimefanyiwa kazi huku Sh. bilioni 7.2 zikiwa zimeteketezwa.

"Kuna fedha kwa ajili ya mradi wa maji Sh. milioni 400 hazipo na hazijawasilishwa kwa mkaguzi, hivyo kamati imeamua tusiwahoji, tumemwagiza CAG wa kanda hiyo akafanye kazi ya ukaguzi maalum ndani ya miezi mitatu alete majibu," alisema.

Alisisitiza lazima ukaguzi ufanyike na wahojiwe kutokana na fedha kutumika bila kufuata utaratibu.

"Hatuwezi kufumbia macho suala hili maana hata kama kuna watendaji wapya kwa sasa, hatuwezi kuwasifia wakati wizi bado unaendelea kufanyika," alisema.

Chikota pia aliagiza Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi)

INAENDELEA UK 8

# Majaliwa amweka DED kikaangoni

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa, amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, kumpelekea taarifa za utendaji kazi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, Waryoba Gunza, baada ya kushindwa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa mradi wa maji kata ya Rutamba.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye kijiji cha Rutamba akiwa katika ziara yake ya kikazi ya kukagua shughuli za maendeleo na huduma za jamii mkoani Lindi.

Alitoa agizo hilo baada ya kumtaka mkurugenzi huyo kutoa maelezo walivyojipanga kutekeleza mradi wa maji kwenye kata hiyo ambayo wakazi wake wanakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa huduma hiyo na kushindwa kufanya hivyo.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka ofisi ya mhandisi wa maji wa wilaya, mradi wa kata hiyo unakabiliwa na uchakavu wa miundombinu na ukarabati wake unahitaji Sh. milioni 75 ambazo wameziomba kutoka Wizara ya Maji.

Waziri Mkuu alisema miradi yote ambayo gharama zake ziko chini ya Sh. milioni 100 inatakiwa itekelezwe kwa kutumia fedha za ndani ya halmashauri husika.

"Miundombinu hiyo ilitakiwa iwe imebadilishwa. Mradi wa Sh. milioni 75 unaomba fedha wizarani? Huo ni uvivu," alisema.

Waziri Mkuu alisema suala la huduma ya maji limewekewa msisitizo na Rais John Magufuli kwa kuanzisha kampeni ya kumtua mama ndoo kichwani, inayolenga kuwawezesha wananchi kupata maji safi na salama karibu na makazi yao.

Aliwaambia wananchi kuwa serikali ina mikakati mizuri inayolenga kuondoa tatizo la maji nchini kote ili kusaidia wananchi hasa wanawake kutumia muda mwingi kufanya kazi za maendeleo kuliko kutafuta maji.

Waziri Mkuu aliwahakikisha wananchi hao kwamba licha ya kuagiza mradi huo wa ukarabati wa miundombinu ya kusambazia maji ufanyike kwa haraka, pia serikali inatekeleza mradi mwingine wa maji wa Milola ambao ukikamilika na maji yatafikishwa hadi Rutamba.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu aliwaagiza wakuu wa wilaya nchini wahakikishe wanawasimia vizuri watumishi wa umma na kuwachukulia hatua wote watakaobainika kushindwa kutekeleza majikumu yao ipasavyo.

"Rais Magufuli ana nia njema ya kuwapa huduma safi wananchi wote hadi wanyonge na ameelekeza wahudumiwe vizuri bila ubaguzi. Wananchi kama kuna mtumishi asiyewahudumia vizuri, msisite kumtaja kwa sababu serikali hii haitamvumilia," alisema.

Waziri Mkuu asema ni lazima kila mtumishi wa umma anayelipwa mshahara kwa kutumia kodi za wananchi ahakikishe anatekeleza ipasavyo majukumu yake kwani asipofanya hivyo hatokuwa na nafasi ya kuendelea na kufanya kazi ndani ya Serikali.



## Mpango kuwapeleka kina Tenga mahakama mafisadi waandaliwa

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya kutakatisha fedha inayowakabili vigogo wa Kampuni ya Six Telecoms, akiwamo Wakili wa kujitegemea Dk. Ringo Tenga, umedai mahakamani kwamba bado unaandaa nyaraka muhimu kwa ajili kukamilisha hatua za kuhamishwa kesi hiyo kwenda Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa.

Kesi hiyo ilipangwa kutajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Hata hivyo, Wakili wa Serikali Jacqueline Nyantori alidai kuwa upande wa Jamhuri unaandaa nyaraka muhimu kwa ajili ya kukamilisha kesi hiyo kuhamishiwa Mahakama Kuu.

Kutokana na mpango huo, alidai kuwa upande wa Jamhuri unaomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Wakili wa utetezi, Alex Mgongolwa, alidai kuwa wanaomba muda wa kujadiliana na washtakiwa.

Hakimu alisema kesi hiyo ya muda mrefu na kwamba washtakiwa walifikishwa Mahakamani Novemba 20, 2017 hivyo wanataka kujua hatima yao.

Alisema mawakili wa pande zote mbili wahakikishe kesi hiyo inasonga mbele.

Hakimu Simba alisema kesi hiyo itatajwa Agosti 28, mwaka huu, na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Mapema Aprili 5, mwaka huu, upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika.

"Mheshimiwa hakimu kesi hii imepangwa kwa ajili ya kutajwa na Jamhuri tunaifahamisha mahakama kwamba upelelezi wake umekamilika tunaandaa nyaraka kwa ajili ya kuanza mchakato wa kusikilizwa," ulidai upande wa Jamhuri.

Mbali na Dk. Tenga, washtakiwa wengine ni Mhandisi na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Hafidhi Shamte maarufu Rashidi Shamte, mfanyabiashara na mkurugenzi wa kampuni hiyo, Peter Noni, Mkuu wa Fedha Noel Chacha na kampuni ya Six Telecoms Limited ambao wanadaiwa kutakatisha Sh. bilioni nane.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashitaka sita yakiwamo ya utakatishaji wa fedha, hivyo kuwafanya wakae mahabusu kwa kuwa makosa hayo hayana dhamana kwa mujibu wa sheria.

# Waziri akemea ubaguzi umeme

**Na Mwandishi Wetu, IGUNGA**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameendelea na ukaguzi wa usambazaji wa umeme vijijini wilayani Igunga, akisisitiza kuwa huduma hiyo itatolewa kwa wananchi wote bila kujali aina ya nyumba wanazomiliki.

Amesema wizara yake itahakikisha lengo la serikali la vijiji vyote kufikiwa na nishati ya umeme ifikapo mwaka 2021 linafanikiwa.

Akiwa katika vijiji vya Mwisi, Uswaya na Isenegeja juzi, waziri huyo alikagua utekelezaji wa mradi huo na kuwasha umeme kwenye Kijiji cha Isenegeja.

Akizungumza na wananchi katika vijiji hivyo, Dk. Kalemani alisisitiza wananchi kulipia gharama ya Sh. 27,000 tu kuunganishwa huduma ya umeme.

"Umeme ndiyo nguzo kuu ya maendeleo, hivyo nawasisitiza kuchangamkia huduma hii inayotolewa na serikali ili mfanye shughuli mbalimbali za kiuchumi.

"Kama tulivyosema, umeme hautachagua nyumba, umeme wa serikali hii unapelekwa kwa Watanzania wote bila kisingizio chochote," alisema.

Dk. Kalemani aliwaagiza wakandarasi kuacha tabia ya kuchelewa kuwaunganisha umeme wananchi, akisisitiza kuwa mwananchi akishalipia, aunganishwe na huduma hiyo nndani ya siku saba.

Kuhusu hali ya umeme nchini, waziri huyo alisema inaridhisha na kunapotokea kukatika kwa nishati hiyo, ni kwa sababu za hitilafu.

Mbunge wa Jimbo la Manonga wilayani Igunga, Seif Gulamali (CCM), aliishukuru serikali kwa utekelezaji wa mradi huo muhimu na kumpongeza Waziri Kalemani kwa ufuatiliaji wake.

Gulamali pia alisema amefurahishwa na agizo la waziri huyo la kutaka umeme upelekwe katika vitongoji vyote vya vijiji vinavyopitiwa na mradi huo kabla ya mkandarasi hajaondoka eneo la mradi Oktoba mwaka huu.

"Waziri pia ametoa taarifa ya kulipwa kwa fidia kwa vijiji vya Mwisi, Chabutwa na Simbo kuanzia Septemba Mosi, mwaka huu kwani taratibu zote za malipo zimekamilika. Wanaolipwa fidia ni wale waliopitiwa na nguzo za umeme kutoka njia kuu ambao walitakiwa kulipwa toka mwaka 2012," alisema.






TANGAZO

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## TANGAZO LA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA MWAKA 2019

*(Limetolewa chini ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2019 (Matangazo ya Serikali Na. 371, 372, 373 na 374 ya mwaka 2019)*

**1.0 UTANGULIZI**

Tangu kurejeshwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mfumo wa utawala kupitia Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika ngazi ya Mtaa, Kijiji na Kitongoji umekuwa ukifanyika katika kila kipindi cha miaka mitano. Uchaguzi wa mwisho ulifanyika mwezi Oktoba mwaka 2014 na hivyo Uchaguzi mwingine unatakiwa kufanyika mwaka 2019. Uchaguzi huu unaongozwa kwa Kanuni za Uchaguzi wa Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa katika Mamlaka za Wilaya na Mamlaka za Miji, Matangazo ya Serikali Na. 371, 372 373 na 374 ya Mwaka 2019. Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Waziri anapaswa kutoa Tangazo la Uchaguzi likianisha Ratiba, shughuli za uchaguzi zinazohusika na masharti muhimu ya uchaguzi.

**2.0 MASHARTI MUHIMU YA UCHAGUZI**

Masharti muhimu ya kuzingatia katika Uchaguzi huo ni kama ifuatavyo:

**a) Nafasi zitakazogombewa;**
Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Nafasi zitakazogombewa katika Uchaguzi huu ni:-

(i) Mwenyeviti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo. Kwa nafasi hiyo, Uchaguzi utaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo za Mwaka 2019 (Tangazo la Serikali Na. 371 la Mwaka 2019);

(ii) Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa (Kundi Mchanganyiko la Wanaume na Wanawake) na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa (Kundi la Wanawake) katika Mamlaka za Miji. Kwa nafasi hizo, Uchaguzi utaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2019 (Tangazo la Serikali Na. 372 la Mwaka 2019);

(iii) Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (Kundi Mchanganyiko la Wanaume na Wanawake), Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (Kundi la Wanawake) na Wenyeviti wa Vitongoji katika Mamlaka za Wilaya. Kwa nafasi hizo, Uchaguzi utaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya za Mwaka 2019 (Tangazo la Serikali Na. 373 la Mwaka 2019); na

(iv) Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (Kundi Mchanganyiko la Wanaume na Wanawake), Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (Kundi la Wanawake) na Wenyeviti wa Vitongoji katika Mamlaka za Miji. Kwa nafasi hizo, Uchaguzi utaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2019 (Tangazo la Serikali Na. 374 la Mwaka 2019);

**b) Upigaji wa Kura;**
Kwa mujibu wa Kanuni hizi, kura zitapigwa kwa kutumia karatasi maalum za kupigia kura ambazo zitatakiwa kutumbukizwa katika masanduku maalum ya kupigia kura; na

**c) Wagombea wa nafasi za uongozi;**
Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi watatakiwa kuwa wanachama na wadhamininiwa wa Vyama vya Siasa vyenye Usajili wa Kudumu.

**d) Tangazo la uchaguzi kwa umma;**
Kwa mujibu wa 4 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kifungu cha (1) Waziri anapaswa kutoa Tangazo la Uchaguzi kwa Umma. Kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (2) ya Kanuni hizi, Tangazo litatolewa katika magazeti ya Kiswahili na Kiingereza yanayosambazwa nchi nzima na katika vyombo mbalimbali vya habari si chini ya siku tisini kabla ya siku ya uchaguzi.

**e) Majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji;**
Kwa mujibu wa Kanuni hizi, ili kuwafahamisha wananchi majina ya maeneo na mipaka ambayo itahusika katika kujiandikisha na upigaji wa kura, msimamizi wa Uchaguzi atatangaza majina na mipaka ya Vitongoji vilivyoko katika eneo la Halmashauri husika siku sabini na mbili kabla ya siku ya uchaguzi kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji, Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Mtaa, Wajumbe wa Serikali ya Kijiji na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa.

**f) Maelekezo Kuhusu Uchaguzi;**
Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi wa Uchaguzi atatoa maelekezo ya Uchaguzi siku sitini na mbili kabla ya siku ya uchaguzi.

**g) Uteuzi wa Waandikishaji na Waandaaji wa Orodha ya Wapiga Kura;**
Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa watumishi wa umma watakaoandikisha na kuandaa Orodha ya Wapiga Kura siku hamsini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi.

**h) Uandikishaji wa Wapiga Kura;**
Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Uandikishaji na uandaaji wa Orodha ya Wapiga Kura utaanza siku ya arobaini na saba kabla ya siku ya uchaguzi na utafanyika kwa muda wa siku saba kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi katika majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma, uandikishaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na Viongozi wa Vyama vya Siasa;

i) **Vituo vya Kujiandikisha, Kupiga Kura na Kupigia Kura;**
Kwa mujibu wa Kanuni hizi, vituo vya kujiandikisha kupiga kura na kupigia kura, kwa maeneo yaliyo chini ya Halmashauri za Wilaya na Mamlaka za Miji Midogo vitakuwa katika ngazi ya Kitongoji. Kwa upande wa Mamlaka za Miji (Miji, Manispaa na Majiji), vituo vya kujiandikisha kupiga kura na kupigia kura vitakuwa katika ngazi ya Mtaa;

j) Muda wa Kuchukua na Kurudisha Fomu za Uteuzi;
Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Mtu yeyote anayekusudia kugombea nafasi za uongozi, atatakiwa kuchukua fomu ya uteuzi wa kugombea nafasi husika siku zisizopungua ishirini na sita kabla ya siku ya uchaguzi kwa kadri itakavyoelekezwa na Msimamizi wa Uchaguzi na kutakiwa kurejesha fomu husika ndani ya muda wa siku saba tangu siku ya kwanza ya uchukuaji wa fomu iliyotangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

**k) Ukomo wa Kuwa Madarakani;**
Nafasi zote zinazogombewa zilikuwa na uongozi kwa kipindi cha miaka 5. Kwa mujibu wa Kanuni hizi, viongozi hao watakoma kushika nafasi za uongozi siku saba kabla ya siku ya kuchukua fomu za kugombea uongozi chini ya Kanuni hizi.

**l) Utaratibu wa uteuzi wa Wagombea;**
Kwa kujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa wagombea wa nafasi zilizoainishwa katika Kanuni hizi, siku kumi na tisa kabla ya tarehe ya Uchaguzi kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.

**m) Kamati ya Rufani;**
Endapo wagombea hawataridhika na maamuzi ya Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi kuhusu uteuzi wa wagombea, kutakuwa na Kamati ya Rufani katika kila Wilaya ambayo itasikiliza mapingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea katika Wilaya husika. Wajumbe wa Kamati ya Rufani watateuliwa siku saba kabla ya siku ya uteuzi wa wagombea.

**n) Waangalizi wa ndani wa uchaguzi;**
Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Waangalizi wa Ndani wa Uchaguzi wataruhusiwa kuangalia uchaguzi baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Maombi ya kibali cha uangalizi wa uchaguzi yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa ndani ya muda wa siku ishirini na moja baada ya Tangazo la Uchaguzi kutolewa.

**o) Elimu ya Mpiga Kura;**
kwa mujibu wa Kanuni hizi, Taasisi yoyote inayotaka kutoa elimu ya mpiga kura katika uchaguzi, itatakiwa kuwasilisha maombi ya kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia Mwongozo wa Elimu ya Mpiga kura ulioandaliwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI.

**p) Kampeni za Uchaguzi;**
Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Kampeni za Uchaguzi zitafanyika siku saba kabla ya siku ya Uchaguzi. Aidha, Kanuni zinaelekeza, kila Chama cha Siasa kinachoshiriki Uchaguzi kitawasilisha ratiba yake ya mikutano ya kampeni ya Uchaguzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi si chini ya siku saba kabla ya kuanza kwa kampeni.

Hivyo, kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2019 ibara 4(1-3) (Matangazo ya Serikali Na. 371, 372, 373 na 374) ya mwaka 2019, Waziri mwenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anautangazia umma wa Watanzania na Vyama vyote vya Siasa vyenye Usajili wa Kudumu kuwa **tarehe 24 Novemba, 2019 itakuwa ni siku ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Tanzania Bara. Upigaji wa kura utaanza saa mbili kamili asubuhi na kumalizika saa kumi kamili jioni.**

**Ninawatakia uchaguzi mwema, amani na utulivu katika kipindi chote cha uandikishaji, uteuzi wa wagombea, kampeni na upigaji kura**

**1.0 RATIBA YA UCHAGUZI**

Ratiba ya Uchaguzi itakuwa kama ifuatavyo:

| Na. | TUKIO | TAREHE | MHUSIKA |
|---|---|---|---|
| 1. | Maombi ya Kuangalia Uchaguzi | 27 Agosti -16 Septemba, 2019 | Katibu Mkuu OR - TAMISEMI |
| 2. | Uteuzi wa Wasimamizi wa Uchaguzi | 2-9 Septemba, 2019 | Mamlaka ya Uteuzi |
| 3. | Tangazo la Majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji | 13 Septemba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 4. | Uteuzi wa Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Vituo. | 16 - 22 Septemba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 5. | Maelezo Kuhusu Uchaguzi | 23 Septemba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 6. | Uteuzi wa Waandikishaji wa Wapiga Kura | 3 Oktoba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 7. | Viapo kwa Waandikishaji wa Wapiga Kura, Wasimamizi wa Vituo na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi | 4-6 Oktoba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 8. | Elimu kwa Waandikishaji wa Wapiga Kura | 4-6 Oktoba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 9. | Zoezi la Uandikishaji wa Wapiga Kura | 8-14 Oktoba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 10. | Kubandikwa kwa Orodha ya Wapiga Kura | 15 Oktoba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 11. | Ukaguzi wa Orodha ya Wapiga Kura | 15-21 Oktoba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 12. | Pingamizi Kuhusu Uandikishaji wa Wapiga kura | 15-21 Oktoba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi Msaidizi |
| 13. | Uamuzi Kuhusu Pingamizi | 21-22 Oktoba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi Msaidizi |
| 14. | Marekebisho ya Orodha ya Wapiga Kura | 21-22 Oktoba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi Msaidizi |
| 15. | Kukata Rufaa Dhidi ya Uamuzi wa Pingamizi | 21-23 Oktoba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 16. | Uamuzi wa Rufaa | 21-26 Oktoba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 17. | Kukoma Uongozi kwa Viongozi Waliopo Madarakani | 22 Oktoba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 18. | Kuchukua Fomu za Kugombea | 29 Oktoba, 2019 | Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi |
| 19. | Kurejesha Fomu za Kugombea | 29 Oktoba-4 Novemba. 2019 | Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi |
| 20. | Uteuzi wa Kamati ya Rufani | 29 Oktoba, 2019 | Katibu Tawala wa Mkoa |
| 21. | Uteuzi wa Wagombea | 5 Novemba, 2019 | Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi |
| 22. | Uwasilishaji wa Pingamizi Kuhusu Uteuzi wa Wagombea | 5-6 Novemba, 2019 | Mwombaji/Mgombea |
| 23. | Uamuzi wa Pingamizi Kuhusu Uteuzi wa Wagombea | 5-7 Novemba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi Msaidizi |
| 24. | Kukata Rufaa Dhidi ya Uamuzi Kuhusu Pingamizi la Uteuzi | 5-8 Novemba, 2019 | Mwombaji/Mgombea/ Msimamizi wa Uchaguzi |
| 25. | Uamuzi wa Kamati ya Rufaa | 5-9 Novemba, 2019 | Kamati ya Rufani |
| 26. | Uwasilishaji wa Ratiba za Mikutano ya Kampeni kutoka katika Vyama vya Siasa | 10 Novemba, 2019 | Vyama vya Siasa/ Msimamizi wa Uchaguzi |
| 27. | Uwasilishaji wa Ratiba za Mikutano ya Kampeni kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya | 14 Novemba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 28. | Kuanza kwa Kampeni | 17-23 Novemba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 29. | Siku ya Uchaguzi | 24 Novemba, 2019 | Msimamizi wa Uchaguzi |

Kwa Tangazo hili, Wananchi wote wanaombwa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha, kupiga kura, kugombea na kushiriki katika Uchaguzi huu ili kupata viongozi bora wa Serikali za Mitaa kwa maendeleo ya nchi yetu.

**SELEMANI S. JAFO (MB.)**
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**23 Agosti, 2019**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga na Azam maombi yetu kwenu Caf

**WAWAKILISHI** wa Tanzania Bara kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba na Yanga, leo na kesho watashuka katika viwanja tofauti barani Afrika kusaka ushindi ili kuweza kuendelea kuipeperusha bendera ya nchi katika raundi ya kwanza ya kinyang'anyiro hicho cha kimataifa huku Azam FC nayo ikiwa na kibarua kigumu kwenye Kombe la Shirikisho dhidi ya Fasil Kenema ya Ethiopia.

Katika michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika, mechi zao za kwanza za raundi ya awali, Simba ambayo itashuka Uwanja wa Taifa kesho kuikaribisha UD Songo ya Msumbiji, ililazimisha sare tasa ugenini.

Hivyo, inahitaji kupata matokeo ili kuweza kutinga raundi ya awali na ya mwisho kabla ya kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, Caf.

Na endapo Simba itasonga mbele ama UD Songo, itakuna na mshindi kati ya FC Platinum ya Zimbabwe na Nyasa Bullets ya Malawi ambayo leo itakuwa ugenini ikisaka matokeo baada ya mechi ya awali kulazimishwa sare tasa nyumbani.

Kwa upande wa Yanga leo itakuwa ugenini Gaborone nchini Botswana kurudiana na mabingwa wa nchi hiyo, Township Rollers ikisaka ushindi ama sare ya kuanzia mabao mawili ili kuweza kusonga mbele baada ya mechi ya awali kulazimishwa sare ya bao 1-1 katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Inaweza kuwa mechi ngumu kwa Yanga kutokana na kuwa ugenini huku Township Rollers pia wakishuka dimbani wakiwa na rekodi ya kushinda mabao 2-1 katika michuano hiyo mwaka jana.

Hata hivyo, hiyo haiwezi kuwa sababu kubwa kwa Yanga ambayo wakati ikipoteza mchezo huo haikuwa na kocha wa sasa, Mwinyi Zahera, lakini pia kikosi hicho kwa sasa kikiundwa na nyota wengi wapya ambao hawakuwamo katika mchezo huo.

Kwa upande wa Azam itahitaji ushindi wa kuanzia mabao 2-0 ili kusonga mbele kufuatia mechi ya awali nchini Ethiopia kuchapwa bao 1-0.

Tunaamini mechi za awali zilikuwa ngumu kote kwa Simba na Yanga hata kwa Azam kutokana na ukweli kwamba ndiyo zilikuwa za kwanza za kimashindano msimu huu kwao, huku pia wachezaji wengi wakiwa wapya jambo ambalo walihitaji muda ili kuweza kupata muunganiko mzuri.

Hivyo, tayari makocha Zahera na mwenzake wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems pamoja na wa Azam FC, Etienne Ndayiragije wameona wapi ambapo wanatakiwa kufanyia marekebisho ili kupata ushindi katika mechi hizo za marudiano.

Lakini pia mechi mbili za kirafiki ambazo Yanga imecheza dhidi ya Polisi Tanzania ya Moshi na AFC Leopards ya Kenya, zitakuwa zimempa mwanga Zahera wa kujua nini ambacho anatakiwa kukifanya katika mechi hiyo ya marudiano leo.

Kwa Aussems ambaye aliiongoza Simba kutwaa Ngao ya Jamii kwa kushinda mabao 4-2 dhidi ya Azam FC Uwanja wa Taifa, ni wazi atakuwa pia ametumia mechi hiyo kurekebisha makosa yaliyojitokeza mchezo wa awali ugenini kabla ya kesho kurudiana na UD Songo, lakini pia Ndayiragije atakua amebaini wapi anapaswa kupaimarisha zaidi kabla ya kushusha majembe yake uwanjani leo.

Kwa mantiki hiyo, Nipashe tunaamini kubwa na wawakilishi hao wa Tanzania kuweza kufanya vizuri na kutinga raundi ya kwanza na kisha hatua ya makundi kabla ya robo fainali, nusu na kisha fainali kama si kutwaa ubingwa huo kabisa kwani lengo letu ni kuona timu hizo zikiandika historia mpya.

Kwa kufanya hivyo kutavutia mawakala wengi kutupia jicho soka letu, lakini pia wachezaji watajiongezea soko kubwa nje ya Tanzania jambo ambalo litawaongezea maslahi mapana kimaisha. Tunazitakia ushindi Yanga, Azam na Simba kwenye michezo yao hiyo itakayopigwa leo na kesho.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Jifanye mnyonge upate kujua

NJIA nzuri ya kujifunza jambo kutoka kwa mtu mwingine ni kujifanya mnyonge au kutoonyesha kwamba walijua. Methali hii hutumiwa kumshauri mtu mwenye nia ya kuongeza maarifa yake kwamba asione ugumu wa kujifanya mnyonge ili afaidike.

Ufafanuzi (maelezo yanayoweka wazi hali ya jambo) huu ni maalum kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF) kuruhusu klabu za Ligi Kuu kusajili wachezaji wengi kutoka nchi za nje. Kwani Tanzania haina wachezaji wenye uwezo kama au kuliko wao? Wapo wengi ila twashindwa namna ya kuwapata na kuwafunza itakiwavyo.

Twaambiwa "chako ni chako, cha mwenzio si chako." Kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa na una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine. Twafunzwa kuvitegemea vitu vyetu wala si vya watu wengine.

TFF yapaswa kuanzisha chuo maalum cha mafunzo ya kandanda kwa vijana wanaopenda mchezo huo. Chuo hicho kiwe na walimu wazawa watakaoongozwa na wataalamu wa kandanda na daktari wa viungo kutoka nje ya nchi. Kwa utaratibu huo Tanzania yaweza kupata wachezaji mahiri wa kandanda watakaoisaidia nchi na hata kutakiwa na klabu za Ulaya.

Nashindwa kuelewa ni kwa nini TFF imeruhusu klabu zinazoshiriki Ligi Kuu ya Tanzania Bara kusajili wachezaji wa kigeni kati ya saba na kumi kwa timu moja! Kwa nini isiwe wachezaji wawili au watatu ili kuwapa nafasi wachezaji wetu? Baadhi ya wachezaji wa kigeni hawana tofauti na wachezaji wetu na mara nyingine wachezaji wetu huonekana kuwa bora zaidi ya wageni.

Kupunguza wingi wa wachezaji kutoka nje utawanufaisha wachezaji wetu kwani watapata nafasi ya kucheza nje ya nchi kwa kusajiliwa na klabu kubwa za Uingereza, Ujerumani, Italia, Hispania, Ufaransa n.k. Hii itakuwa manufaa kwa pande zote mbili yaani Tanzania na wachezaji watakaosajiliwa nje ya nchi.

Tusihadaike na rangi, tamu ya chai ni sukari. Maana yake tusidanganyike kutokana na rangi ya chai kwani utamu wake hutokana na sukari. Methali hii yaweza kutumiwa kumkanya mtu kutopumbazwa au kutovutwa na sifa za nje za kitu ila akichunguze kwa ndani.

Wachezaji wageni wanaocheza kandanda nchini, hasa timu za Azam, Simba na Yanga ni wangapi huitwa makwao kuzichezea timu za mataifa yao? Labda ni wawili tu waliosajiliwa na Simba kutoka Uganda na mmoja kutoka Rwanda ndio huitwa kuzitumikia timu zao za taifa zinaposhiriki michezo ya kimataifa.

Waliobaki huja Tanzania kujitafutia maisha baada ya kushindwa kuzivutia timu za Ulaya na Afrika. Wengine, kama twakumbuka, walijileta wenyewe nchini kutafuta timu za kuwasajili. Iliposhindikana walirejea kwao kimya kimya na njaa zao!

Tanzania imegeuzwa kuwa 'jalala' la kupokea 'makapi' kutoka nje nasi kuwapapatikia kama afanyavyo kuku anayechinjwa! Kama wangekuwa wa maana wangesajiliwa na klabu kubwa za Afrika na Ulaya kama walivyo kina Mbwana Samatta na wengineo.

Msimu wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara umemalizika kwa Klabu ya Simba wanaofahamika pia kama 'Wekundu wa Msimbazi,' kutwaa ubingwa kwa mara ya pili mfululizo. Cha kushangaza ni kuwa imetwaa ubingwa huo ikiwa kwenye mji wa Singida kama ilivyokuwa msimu uliopita!

Tofauti ni jinsi ilivyokuwa msimu uliopita na huu uliomalizika majuzi. Msimu wa mwaka jana, Simba iliutwaa ubingwa wakati wachezaji wake wakiwa hotelini kutokana na Yanga kufungwa 1-0 jijini Mbeya na timu ya Magereza.

Msimu uliomalizika hivi karibuni, pia Simba ilitwaa ubingwa ikiwa Singida pia kwa kuifunga timu hiyo mabao 2-0 ingawa bao la pili lilikuwa na mushkeli (kasoro). Hata kama lisingekubaliwa, bado Simba ni bingwa kwa bao la awali lililofungwa na mshambuliaji wao hatari, Kagere mapema kipindi cha kwanza na kukosa majibu ya wenyeji, Singida United.

Toleo lililopita niliandika kuhusu maradhi yanayomsumbua Jella Mtagwa aliyekuwa mchezaji mahiri wa Yanga na Taifa Stars. Kwamba si Yanga, Shirika la Posta wala serikali inayokumbuka kumsaidia Jella kipindi hiki cha maradhi yake. Makala yangu ilikuwa chini ya kichwa: "Fadhila za punda mateke."

Mchezaji aliyecheza Simba na Cosmopolitan zamani, alinitumia ujumbe ufuatao baada ya kukerwa na hao niliowataja kutomshughulikia Jella Mtagwa: "Waandikie viongozi wa Yanga kuwauliza kama wanajua hali ya Jella Mtagwa na wachezaji wengine ambao wameifanya Yanga iwe hapo ilipo sasa." Naitwa Maige (Black Brother)/SSC & Cosmo.

"Mambo yafaayo watu ni yaingiayo chunguni." Maana yake mambo yanayofaidi watu ni yanayoingia chunguni. Hutumiwa kumtanabahisha mtu kuwa njia nzuri ya kumsaidia mtu aliye shidani ni kumkabidhi kitu sio kumpa ahadi au kumtolea maneno matupu tu.

Ile ahadi ya kumjengea nyumba aliyekuwa mchezaji mahiri wa Yanga, Sekilojo Chambua enzi zile ilitimizwa? Kadhalika, kuna wakati wachezaji wa Yanga waliahidiwa kupewa nyumba maeneo ya Kigamboni na/au Mbagala. Je, ilikuwa kuwatia hamasa wachezaji ili wacheze kwa bidii ama ilikuwa hadaa?

*marobarnabas@yahoo.com*
*0784 334 096*

# Waswekwa ndani tuhuma za ubadhirifu

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

NAIBU Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ameamuru kukamatwa kwa viongozi wanne wa mradi wa maji wa Makilenga unaotekelezwa kwa zaidi ya Sh. bilioni 3.6 katika Tarafa ya King'ori wilayani Arumeru baada ya kubainika kuwapo ubadhirifu.

Waliokamatwa na kuwekwa chini ya ulinzi ni mhasibu Waliaranga Kisetu, mwenyekiti Goodhope Nnko, meneja Onest Kyori na Ndelelo Kaaya ambaye ni fundi msaidizi.

Akitoa amri hiyo baada ya kusikiliza wananchi wa maeneo ya King'ori na Malula, Aweso aliwauliza utaratibu wa ugawaji maji katika vijiji 22 ukoje na una akiba ya kiasi gani, ndipo viongozi hao waliposhindwa kujibu.

"Nyie eneo hili mmeshindwa kusimamia mradi mna tatizo la uongozi na kuanza kutoa maji kwa upendeleo kwa baadhi ya vijiji na vingine mkiwanyima, wengine kwa vigezo vyenu, hivyo siwezi kuwavumilia," alisema.

Aidha aliahidi akifika wizarani atatuma timu ya wakaguzi ili kukagua mradi huo kubaini vizuri kiasi halisi na vifaa vya mradi vilivyoibwa.

Alisema serikali haiwezi kukubali kuona watu wanagawa maji kwa kuendekeza ukabila kwa kuwa taifa haliwezi kukubaliana nalo.

"Huu mradi serikali imegharamia na kila mwaka wanakusanya zaidi ya Sh. milioni tano lakini mpaka sasa kwa miaka mitano nawauliza akiba yao ni Sh. ngapi wanasema Sh. milioni moja. Huu ni wizi mkubwa lazima muwe chini ya ulinzi," alisema.

Pia aliagiza bodi ya mradi huo iwe na uwakilishi wa wenyeviti wa vijiji vyote ili kuweka usawa katika ugawaji wa maji.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, akizungumza kabla ya naibu waziri kuzungumza, alimwomba Aweso kufumua bodi hiyo ili vijiji vyote vinufaike na maji.

Alisema shida kubwa katika eneo hilo ni kutofautiana kati ya wenyewe na wenyewe na kuwaletea shida wananchi kwa maslahi yao.

Kwa upande wao, wananchi wa King'ori, Mwaija Omari na Mathayo Mbise, walimwomba Aweso kumaliza tatizo la maji linalowakabili kwa sababu wanabaguliwa na mradi huo kwa sababu ya ukabila.

"Sisi hapa tunabaguliwa, maji hatupati sisi wa chini huku King'ori sababu wengi tumehamia si wenyeji wa Meru mpaka wanafikia hatua kutuita Madokoo. Hii si sawa, tunaomba serikali itusaidie tunateseka sana," alisema Omari.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka (DAWASA), Jenerali mstaafu Davis Mwamunyange (katikati), akipata maelezo alipotembelea Mikoa ya kihuduma ya DAWASA ya Tegeta, Kawe, Kinondoni na Ilala, jijini Dar es Salaam jana, kujionea utendaji kazi wa mikoa hiyo pamoja na jitihada zinazofanyika katika kuboresha huduma ya maji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Atupwa jela miaka 30 kwa kubaka mtoto wa miaka 10

**Na Said Hamdani, LINDI**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi imemhukumu Issa Mpanyanje (51) kifungo cha miaka (30) jela baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka 10.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Lillian Rualabamo, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka. Kabla ya hukumu hiyo, mshitakiwa alipewa nafasi ya kujitetea na kuiomba mahakama imwonee huruma kwa madai kwamba ni kosa lake la kwanza na ana familia akiwamo mke na watoto wanaomtegemea, hivyo iwapo atapata adhabu kali watakosa huduma yake.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Rugalabamo alimwuliza Mwanasheria wa Serikali Rabia Ramadani kama anazo kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa mshitakiwa. Mwanasheria huyo alijibu kwamba hana makosa ya zamani lakini akaomba mahakama kumpatia mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya aina hiyo.

Hakimu Rugalabamo, baada ya maelezo hayo, alisema amesikia maombi ya pande zote mbili lakini kutokana na sheria kumshika mikono, anamhukumu mshtakiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani na atakapomaliza adhabu hiyo, amlipe mlalamikaji fidia ya Sh. Milioni mbili.

Awali, ilidaiwa mahakamani na mwanasheria Ramadhani kwa mshtakiwa huku akitambua anachokifanya ni kosa, Aprili, 14 mwaka huu, majira ya mchana akiwa shambani, bila huruma alimbaka mlalamikaji na kumsababishia maumivu makali sehemu zake za siri.

Mwanasheria huyo aliiambia mahakama kuwa mshitakiwa alipata mwanya huo baada ya kumshawishi mlalamikaji waende shambani akamsaidie kuvuna karanga na baada ya kufika huko alianza kumtomasatomasa kisha kumbaka, huku akimsisitiza kutomwambia mtu yeyote.

Hata hivyo, kutokana na maumivu makali aliyokuwa akiyapata mtoto huyo, waliporejea nyumbani alimweleza mama yake na hatimaye kutoa taarifa kituo cha polisi na mtuhumiwa kukamatwa kisha kufikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

# St. Anne Marie yang'ara tena Dar

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya St. Anne Marie Academy ya Mbezi, jijini Dar es Salaam, imekuwa ya kwanza kwa mara nyingine kwa Wilaya ya Ubungo katika matokeo ya mtihani wa majaribio (Mock) kwa darasa la saba.

Matokeo hayo yalitangazwa jana na Ofisa Elimu Msingi Wilaya ya Ubungo, Dar es Salaam, Chausiku Masegenya, ambaye alisema shule hiyo ni pekee iliyopata ufaulu wa zaidi ya asilimia 90, yaani 'Band One'.

Alitangaza pia majina ya wanafunzi 10 bora kwenye matokeo hayo na sita kati yao wametoka St Anne Marie na kuipongeza shule hiyo kwa kuibeba wilaya hiyo kielimu.

Ofisa Elimu huyo aliwapongeza wanafunzi wote wa shule hiyo kwa kufanya vizuri sana kwenye matokeo hayo na kuitaka shule hiyo kuendelea na jitihada zake kielimu.

Mkuu wa shule hiyo, Gladius Ndyetabura, alisema kutokana na mafanikio hayo, wilaya hiyo imeipongeza kwa kushika nafasi ya kwanza kwa mara nyingine tena.

Alisema hivi karibuni Mkoa wa Dar es Salaam uliipatia Ngao Maalum shule hiyo kama sehemu ya kutambua mchango wake katika kuinua elimu hapa nchini na kuwa miongoni mwa shule zinazofanya vizuri kitaaluma.

Ndetabura alisema shule yake ilipewa ngao inayoonyesha kuwa ni miongoni mwa shule zilizofanya vizuri zaidi kwenye matokeo ya darasa la saba nchini.

mkuu huyo alisema ingawa shule yake imeingia katika 10 bora kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka jana, hawajabweteka na badala yake wanafanya jitihada za kuwa namba moja.

"Kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka jana tumefanikiwa kuwa wa kwanza Wilaya ya Ubungo, tumekuwa wa pili Mkoa wa Dar es Salaam na tulikuwa wanane kitaifa sasa hii haitufanyi tubweteke tutapambana kupata nafasi za juu zaidi," alisema.

**"Kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka jana tumefanikiwa kuwa wa kwanza Wilaya ya Ubungo, tumekuwa wa pili Mkoa wa Dar es Salaam na tulikuwa wanane kitaifa sasa hii haitufanyi tubweteke tutapambana kupata nafasi za juu zaidi," alisema.**

HABARI KITAIFA

# Mawakili 14 serikali wamkabili Lissu

INATOKA UK 2

kana, hakuna uamuzi wowote ulioambatanishwa katika maombi ili mahakama iyapitie na kuyatolea uamuzi. Maombi yoyote ni muhimu kisheria kuambatanisha uamuzi unaomkumba," alidai Mrisha.

Akifafanua hoja za pingamizi hilo, alidai kuwa kiapo cha Alute alichoambatanisha ni nakala ya magazeti na si uamuzi, hivyo hakuna uamuzi wowote uliotolewa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, isipokuwa alitimiza matakwa ya kisheria kwa kumwandikia barua Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Taifa kwamba kuna kiti kiko wazi.

Wakili wa Serikali Mkuu, Lucas Marunde, alidai waleta maombi wanaomba mahakama imlazimishe Spika alete tamko lake la kumvua ubunge Lissu mahakamani na wadai wapewe nakala.

"Mheshimiwa Jaji, Sheria ya Uchaguzi Na. 37(3) Sura ya 343 ya mwaka 2015 inasema Mbunge anapokuwa hayupo katika kiti chake kwa mikutano mitatu mfululizo ya Bunge bila kutoa taarifa kwa Spika anamfahamisha Mwemyekiti wa Tume ya Uchaguzi kwamba kiti kiko wazi," alidai.

Alidai si Spika anayetoa tamko bali anatoa taarifa na hajishuhulishi na kitu kingine chochote na kwamba katika kesi hiyo mwombaji hakuwepo katika kiti chake cha ubunge.

Wakili Marunde alidai hakuna uamuzi wowote kutoka kwa Spika, hivyo wanaomba maombi yatupwe kwa gharama.

Hoja zingine ziliwasilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu George Mundepo, ambaye alidai kwamba mleta maombi, Alute Mughwai, hana sifa ya kufungua maombi kwa niaba ya Lissu.

Alidai sheria inaruhusu madai kufunguliwa na mhusika au anayemwakilisha mwenye mamlaka kisheria lakini shauri lililopo limewasilishwa na Tundu Lissu kupitia mwakilishi wake, Mughwai.

Kutoka na hoja hizo, aliomba mahakama iyatupe maombi kwa kuwa pamoja na mambo mengine, aliyeyawasilisha hana sifa ya kufanya hivyo.



Jaji Matupa jana alitakiwa kusikiliza maombi ya zuio la muda la kuapishwa kwa Mbunge Mteule wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, na maombi ya kupinga kuvuliwa ubunge wa Lissu lakini haikuwezekana baada ya Jamhuri kuwasilisha pingamizi la awali.

Maombi ya kupinga kuvuliwa ubunge yalifunguliwa na Lissu kupitia mawakili wake chini ya hati ya dharura, kupitia kaka yake, Wakili Mughwai, ambaye amempa mamlaka ya kisheria kufanya hivyo.

Kwa mujibu wa ombi namba 18 la mwaka 2019, Lissu anaiomba mahakama hiyo impe kibali cha kufungua kesi ili mahakama hiyo itoe amri ya kumtaka Spika Ndugai ampe (Lissu) taarifa yake ya kumvua ubunge.

Anaiomba mahakama hiyo itengue na kutupilia mbali uamuzi huo wa Spika Ndugai kumvua ubunge.

Mwombaji huyo anaomba mahakama itoe amri ya kusimamisha kuapishwa kwa Mtaturu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katika hati ya dharura, Lissu anaiomba mahakama hiyo isikilize na kutoa uamuzi wa maombi yake haraka kuwa vinginevyo Mtaturu ambaye Julai 19, mwaka huu, alitangazwa na msimamizi wa uchaguzi wa jimbo hilo, ataapishwa kushika wadhifa huo, anadai atakuwa ameathirika kwa kuwa atapoteza haki zake zote, kinga na maslahi yote yanayoambatana na wadhifa wake wa ubunge.

Uamuzi wa kumvua ubunge ulitangazwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, Juni 28, mwaka huu wakati akiahirisha mkutano wa 15 wa Bunge, huku akitaja sababu mbili.

Spika Ndugai alizitaja sababu hizo kuwa ni kushindwa kuhudhuria vikao vya bunge kwa muda mrefu bila kumjulisha kwa maandishi mahali aliko na pili ni kutokuja taarifa za mali na madeni kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Hata hivyo, Ndugai alijitetea kuwa si yeye aliyemvua ubunge bali ni Katiba ya nchi.

# Kipenga chapulizwa uchaguzi wa mitaa

INATOKA UK 2

Kuhusu ratiba ya kampeni, Jafo alisema uwasilishaji wa ratiba wa mikutano ya kampeni kutoka kwenye vyama vya siasa utapaswa kufanyika Novemba 10, uwasilishaji wa ratiba kwa Mkuu wa Polisi Wilaya Novemba 14, kuanza kwa kampeni Novemba 17-23 na uchaguzi rasmi ni Novemba 24.

Awali, Katibu Mkuu Tamisemi, Joseph Nyamhanda, alisema maandalizi yote muhimu ya uchaguzi huo yamekamilika na kwa sasa wanasubiri vifaa.

Alisema vijiji 12,319, mitaa 4,264, vitongozi 64,384 vitafanya uchaguzi huo.

CCM, CHADEMA WALONGA

Akizungumzia uchaguzi huo jana, Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Abdallah Juma Sadal, alisema taratibu zote zimewekwa sawa na wako tayari kwa uchaguzi huo ambao wanaamini utakuwa huru na utafanyika kwa amani na utulivu.

"Umefika wakati sasa wa kutengeneza demokrasia nchini kwa kuwa kanuni zipo wazi na zimetengazwa rasmi, wanaozungumza kuwa demokrasia iliyopo nchini si nzuri, jambo hili siyo la kweli maana CCM tunazidi kudumisha amani, tuna katiba inayozungumzia demokrasia, sasa hatuelewi kwanini wao wanapingana nayo," alisema.

Alisema maoni waliyotoa kama vyama vya siasa kwenye utengenezaji wa kanuni za uchaguzi yamezingatia.

Alisema kama wakuu wa mikoa wanalalamikiwa kuwapo kwenye usimamizi wa uchaguzi huo, ni vyema wakaa na upande mwingine wakubaliane ili kuwa na mawazo ya pamoja. Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Zanzibar, Salum Mwalimu, alisema kuwa kwa kauli aliyoitoa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, inaonyesha CCM imejipanga kushinda kwa nguvu za kidola na inaamini itashinda uchaguzi.

"Sisi tumejiandaa vya kutosha hatuna wasiwasi kuhusu uchaguzi huu, hivyo Watanzania wajiandae kwa kuwa wataletewa wagombea wazuri, wasitishike na CCM," alisema.

Alieleza katika uandaaji wa kanuni walipendekeza wakuu wa mikoa waondolewe kwenye usimamizi wa uchaguzi huo lakini wanashangaa wapo na wanajigamba kushinda.

"Tumejipanga tutakutana kwenye uchaguzi na kama wamejiandaa kwa uchaguzi, sawa lakini kama wamejiandaa kwa machafuko, sawa tupo tayari," alisema.

Awali, akitoa neno kwa niaba ya wakuu wa mikoa, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alisema uchaguzi huo ndiyo mhimili wa uchaguzi mkuu wa 2020 ambao kwa vyovyote vile utampatia Rais John Magufuli nafasi ya kuiongoza Tanzania kwa miaka mingine mitano.

"Sisi wakuu wa mikoa tumepokea maelekezo yote na tutazingatia kwa umakini, uadilifu, uzalendo na weledi usio na mashaka, na wananchi wote wenye sifa za kushiriki watashiriki kikamilifu ili kuchagua viongozi bora," alisema.

# Msamaha wagonjwa waitesa Muhimbili

INATOKA UK 2

Magufuli kuhusu deni hilo na walikuwa wakisubiri taratibu za kulipwa na baada ya kupokea fedha hizo, wataandika barua nyingine ya deni la Sh. 364,000 ili Rais Magufuli alimalizie.

Alisema amefurahishwa na moyo wa uzalendo ulionyeshwa na Watanzania hao walioamua kumsaidia Rais Magufuli kulipa deni hilo na kuitaka jamii kuiga mfano huo.

Wakili Msando alisema anakabidhi fedha hizo kwa niaba ya wafuasi wa ukurasa wake Instagram aliowachangisha kupitia kampeni aliyoianzisha.

Alisema aliamua kuchangisha fedha hizo baada ya kuvutiwa na nia ya Rais Magufuli ya kumsaidia mama huyo ambaye alishampoteza mama yake mzazi na hakuwa na fedha za kulipa ili akabidhiwe mwili kwa ajili ya kuuhifadhi.

"Zipo sababu tatu zilizonifanya nikaguswa na kuamua kuchangisha fedha hizi za kusaidia kulipa deni la Rais Magufuli.

"Moja ni ule moyo wake wa ubinadamu wa kutaka kumsaidia na akasema MNH wamdai yeye binafsi, wakati alikuwa na uwezo wa kuagiza hospitali ifute deni hilo au serikali ilipe gharama hizo," Wakili Msando alisema.

Wakili huyo aliongeza kuwa wametumia fursa hiyo kuhamasisha matumizi mazuri ya mitandao ya kijamii na kuhamasisha jamii kusaidia wahitaji kwa sababu hospitali hiyo ina wagonjwa wengi wasiyo na uwezo wa kupata matibabu.

# Vigogo halmashauri watimuliwa bungeni

INATOKA UK 3

kufanya maboresho ya kitengo cha kufuatilia fedha ili kuepuka ubadhirifu.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - Tamisemi, Mwita Waitara, aliahidi kuyafanyia kazi mapendekezo ya kamati hiyo na baada ya uchunguzi kukamilika, hatua kali zitachukuliwa na hakuna atakayesalimika hata kama amestaafu.

Alisema haiwezekani kufumbia macho wakati wananchi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali huku wakitegemea miradi hiyo itatue changamoto zao.

"Mradi hakuna kisa mtendaji mmoja aliyeaminiwa kushindwa kufanya kazi, viongozi wa halmashauri hii mnapaswa kutambua kuwa uamuzi huu wa kamati si mzuri kwetu,"alisema.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita, Denis Bandisa, alihakikishia kamati kuwa watayafanyia kazi kwa kuipa ushirikiano ofisi ya CAG itakapokuwa ikifanya ukaguzi huo.



# Waziri ataka maji ya mradi mpya Desemba

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ameitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA), kuhakikisha ifikapo Desemba, mwaka huu, maji safi ya visima 56 vilivyochimbwa na mradi mkubwa wa zaidi ya Sh. bilioni 520 yanawafikia wananchi ili waondokane na kero ya upungufu wa huduma hiyo.

Aweso alitoa agizo hilo jana jijini hapa wakati wa ziara yake ya kukagua miundombinu ya mradi huo.

Alisema katika mradi huo, mbali na visima hivyo, kumejengwa matangi 10 ya kuhifadhiwa maji ambayo kwa siku kupitia visima hivyo, yatazalisha zaidi ya lita milioni 200 kwa saa, huku mahitaji yakiwa lita milioni 90 kwa muda huo.

"Hii ina maana maji yatakuwa mengi zaidi ya matumizi na hii itaondoa kabisa tatizo la maji na kuwa historia. Ninachoomba wananchi wavumilie miezi michache hii wakati miundombinu inaendelea kukamilishwa ili waanze kuunganishiwa majisafi," alisema.

Alisema ni vyema ujenzi wa tangi la kuhifadhi maji la lita milioni 10 linalojengwa eneo la Ngaramtoni likamilike mapema ili maji hayo yaanze kupambana kwa wananchi.

Naibu Waziri alisema kisima kilichoko eneo la Majimoto wilayani Hai, kitatoa lita 200,000 hadi 500,000 kwa saa, jambo litakalowezesha hata wananchi wa pembezoni mwa mabomba hayo yatakapopita kupata huduma hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa AUWSA, Mhandisi Ruth Koya, alisema tatizo la maji litakwisha baada ya serikali kutoa zaidi ya Sh. bilioni 520.

"Hali ya upatikanaji maji itakuwa nzuri ifikapo Desemba, mwaka huu. Naomba tu wananchi tuvumilie miezi hii michache tunapokamilisha ujenzi wa miundombinu," alisema

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Auwsa, Dk. Richard Masika, alisema kukamilika kwa mradi huo kutawezesha Arusha kupata maji lita milioni 200 kwa siku, ambayo ni zaidi ya mahitaji halisi.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, alisema kukamilika kwa mradi huo kutawezesha Arusha kuondokana na upungufu wa maji uliopo kutoka asilimia 44 hadi asilimia 100 ifikapo mwakani.

# Wanasayansi wabobezi wa mazingira kukutana

**Novatus Makunga,** ARUSHA

ZAIDI ya wanasayansi wabobezi wa mazingira 200 wa ndani na nje, watakutana Jumatano ijayo jijini hapa kutathimini na kuweka mikakati ya kuyahifadhi maeneo tengefu nchini.

Wataalamu hao wanakutana katika Kongamano la Kisayansi la Maeneo Tengefu lililoandaliwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc), ambalo litafunguliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene.

Meneja wa Nemc Kanda ya Kaskazini, Lewis Mtemi, aliwaaambia waandishi wa habari mjini hapa jana kwamba kongamano hilo limelenga kupitia matokeo mbalimbali ya utafiti na kubadilishana uzoefu wa hatima ya maeneo tengefu nchini.

Aliyataja baadhi ya maeneo hayo ambayo mengi yamekumbwa na athari za kimazingira kuwa ni pamoja na Hifadhi ya Ziwa Manyara, Hifadhi ya Taifa ya Ghuba ya Jozan Chwaka, Bonde la Ngorongoro, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Mnazi Bay na kisiwa cha Mafia.

**Lengo ni kujengana kisayansi na kupata maazimio ambayo yatatoa picha halisi na hatimaye kuwasilishwa kwa watunga sera kwa ajili ya utekelezaji kwa manufaa ya taifa.**

Mtemi alisema katika maeneo hayo kuna tishio kubwa la kutoweka kwa aina ya viumbe ambao ni adimu katika uso wa dunia.

Alitoa mfano wa kupungua kwa theluji katika Mlima Kilimanjaro, kupungua kwa kina kwa Ziwa Manyara na kumezwa kwa baadhi ya visiwa katika Bahari ya Hindi.

Meneja huyo alisema hatua ya kuingizwa katika maeneo tengefu inatambuliwa na kusimamiwa kwa karibu sana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco) kutokana na umuhimu wake na kwamba nao watashiriki katika kongamano hilo.

"Lengo ni kujengana kisayansi na kupata maazimio ambayo yatatoa picha halisi na hatimaye kuwasilishwa kwa watunga sera kwa ajili ya utekelezaji kwa manufaa ya taifa," alisema.

Aidha, Mtemi alisema wanasayansi hao pia wataangalia suala zima la mabadiliko ya tabianchi na kuibuka kwa viumbe vamizi katika maeneo tengefu na kuathiri bioanuwai.

Mbali na athari za kimazingira, Mtemi alisema watajadili na kuweka mikakati ya kutumiwa kwa fursa zinazopatikana katika maeneo hayo kwa ajili ya faida za kiuchumi.

Wanasayansi hao wanatoka katika vyuo vya elimu ya juu, taasisi za utafiti na za usimamizi wa uhifadhi, utalii na mazingira zikiwemo Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tawa).



Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, Jumaa Aweso, akiangalia maji katika eneo la maji moto, kwenye moja ya visima vya mradi wa zaidi ya Sh.bilioni 520, unaotekelezwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (AUSWA), jijini Arusha juzi. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# CCM yashinda makamu m/kiti Arusha

**Na Allan Isack,** ARUSHA

DIWANI wa Kata ya Olturoto kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Baraka Simon, amechaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru.


Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Wilson Mahera, alisema kuwa kura zilizopigwa ni 33 na hakuna kura iliyoharibika na Abert Oltulele wa Chadema kutoka kata ya Oloirien, alipata kura 13 huku Simon akipata kura 20.

"Kwa mamlaka niliyopewa ninamtangaza Baraka Simon kuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha kwa kipindi cha mwaka mmoja," alisema Mahera.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa, Simon aliwashukuru wajumbe hao kwa kumchagua na kuahidi kufanya kazi kwa ushirikiano na wajumbe wote ili kuwatumikia wananchi wa halmashauri hiyo.

Pia aliwasihi madiwani wote kushirikiana bila kujali tofauti zao za vyama na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 hadi 2020.

Uchaguzi huo umefanyika kwa mujibu wa kanuni, sheria na taratibu za kuongoza Baraza la Madiwani kwamba kila baada ya mwaka mmoja kumchagua Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri.



# Mawenzi yalia upungufu wa watumishi hospitalini

Na Paul William, MOSHI

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro, Mawenzi, inakabiliwa na upungufu wa wataalam wa kada mbalimbali wakiwamo madaktari bingwa wa afya, watoto, mionzi, dawa za usingizi , pua na masikio pamoja na mafundi sanifu wa vifaa tiba.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Josephine Rogath, alisema jana wakati wa zaira ya Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania Thuwaybah Kissasi, alipotembelea wodi ya wajawazito na waliojifungua ikiwa ni kuelekea kongamano la kumpongeza Rais John Magufuli litakalofanyika leo.

Dk. Rogath alisema hospitali hiyo kongwe ambayo ilianza kujengwa kama zahanati ya kutibu askari wa Kijerumani mwaka 1920, kwa sasa ina watumishi 449 wa kada mbalimbali na ina upungufu wa watumishi 232 wa kada mbalimbali sawa na asilimia 34.

**Dhamira ya serikali ni kuwatumikia wananchi bila kujali itikadi za kisiasa wala dini na kuwataka kila mmoja kuhakikisha anatimiza majukumu yake.**

Alisema upungufu huo ni kwa kada ya madaktari bingwa 14, maofisa wauguzi wasaidizi 33 na wauguzi 95.

Pia alisema hospitali haina kabisa madaktari bingwa wa dawa za usingizi, ofisa utumishi na wataalam wa kada za wahudumu wa afya katika chumba cha kuhifadhia maiti.

Alitaja changamoto nyingine wanayokabiliana nayo ni ukosefu wa uzio kuzunguka hospitali hali inayosababisha kukosekana kwa usalama wa wagonjwa, watumishi na mali za hospitali.

"Uchakavu wa miundombinu ya hospitali zikiwamo wodi na majengo mbalimbali ni changamoto nyingine inayotukabili pamoja na ukosefu wa vifaa tiba kama vifaa vya mionzi (ultra sound), CT Scan, ECG na vifaa kwa ajili ya chumba cha wagonjwa mahututi (ICU)," alisema.

Kissasi aliyeongozana na Katibu Mkuu wa UWT, Mwalimu Queen Mlozi, aliwatia moyo watumishi wa hospitali hiyo kuendelea kufanya kazi kwa bidii japo kuna changamoto hizo na kuahidi kwamba serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, itaendelea kuzitatua hatua kwa hatua.

Alisema dhamira ya serikali ni kuwatumikia wananchi bila kujali itikadi za kisiasa wala dini na kuwataka kila mmoja kuhakikisha anatimiza majukumu yake.

Pia alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi kuendelea kumuunga mkono Rais Magufuli kwa kutekeleza Ilani kwa vitendo na kuwataka kuzidi kumwombea na kuwafichua wale wote wanaokwamisha utekelezaji wa Ilani.



Makamu Mwenyekiti mstaafu wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Albert Msole akielezea maendeleo waliyofanya kwa kipindi cha miaka minne, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Tume yaonya migogoro ya wakulima

Na Mary Mosha, HAI

TUME ya Taifa ya Umwagiliaji imewataka wakulima wa mpunga na mboga katika skimu ya Mtambo kujiepusha na migogoro isiyo ya lazima na badala yake kuwekeza nguvu ya pamoja katika kuinyanyua na kuleta mabadiliko ya kiuchumi.

Mhandisi wa Uwagiliaji Kanda ya Kilimanjaro, Saidi Ramadhani, alisema jana alipotembelea katika skimu hiyo iliyoko kata ya Masama Rundugai wilayani ya Hai huku akiwataka wakulima kushikamana katika kutatua changamoto za skimu hiyo yenye uwezo wa kulisha wananchi wa wilaya takribani tatu.

Alisema kwa sasa ni muhimu kutazama mambo yenye kuleta tija kwa wakulima ikiwamo ukarabati wa miundombinu, kupitisha katiba na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria ili kuzalisha kwa manufaa.

"Leo tumefika hapa katika skimu hii tukiwa na timu ya wataalamu wa udongo, lengo likiwa kupokea changamoto mbalimbali zinazoikabili skimu pamoja na wakulima wake, kutafuta njia ya kuzitatua kwa haraka ili kuzalisha kwa wingi zaidi kwani skimu hii imekuwa ikawahudumia wakulima ya vijiji vya Chekimaji, Mkalama na Kawaya," alisema.

"Tumeamua kukutana na viongozi wa matawi, watendaji wa vitongoji na vijiji katika kata hii, ili kujadili kwa pamoja changamoto zinazowakabili katika kuboresha skimu hii," aliongeza.

Omary Juma, kiongozi wa kijiji katika kijiji cha Chekimaji, alisema ili kuhakikisha wakulima wanapata faida na skimu hiyo, ni lazima serikali iangalie namna ya kuboresha miundombinu ikiwa ni pamoja na kusimamia sheria ndogo ndogo za kudhibiti vyanzo vya maji na wanaolima ndani ya mita 60.

Alisema kwa kufanya hivyo kutasaidia skimu hiyo kusonga mbele na kusaidia katika kuleta tija kwa wakulima.

Mwenyekiti wa Skimu hiyo, Sabiti Moshi, alisema skimu hiyo ina zaidi ya wakulima 2,100 na ina zaidi ya hekta 2,100 itasaidia wakulima kujikwamua kiuchumi na kuleta mabadiliko chanya.

"Licha ya kuwa na matawi mbalimbali yanayohusika na skimu hii, tumekuwa tukijikusanyia mapato kutokana na wakulima kila msimu ili kufanya marekebisho ya miundombinu hasa mifereji. Lakini ikiwa tutapata msaada kutoka serikalini katika kuimarisha miundombinu, maji yatawafikia wakulima wengi zaidi."alisema

Naye Ofisa Kilimo Umwagiliaji wa Wilaya ya Hai, John Chuwa, alisema kwa sasa serikali imewekeza nguvu katika kuimarisha skimu hiyo, ikiwa ni pamoja na kumalizia upitishaji wa katibu na usajili ili ijiendeshe kwa mujibu wa sheria na kanuni.

# Kilimanjaro kinara uchangiaji wa damu

Na Paul William, MOSHI

UMOJA wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Kilimanjaro, umeongoza katika kampeni maalum ya kuchangia damu kitaifa iliyoandaliwa na jumuiya hiyo baada ya kuchangia chupa 345.

Hayo yalibainishwa jana na Katibu wa UVCCM Mkoa wa Kilimanjaro, Asia Halamga, alipozungumza na gazeti hili kuwa vijana na wananchi katika mkoa walijitokeza katika maeneo mbalimbali kuchangia damu.


Alisema uchangiaji huo uliofanyika Agosti 17, mwaka huu, katika wilaya zote za mkoa wa Kilimanjaro, vijana 789 walionyesha nia ya kujitolea kuchangia damu kwa hiari lakini baadhi yao walikutwa kuwa na damu ndogo na wengine kuwa na damu inayowatosheleza wenyewe.

Alisema chupa za damu 345 zilikusanywa na kuufanya mkoa wa Kilimanjaro kuongoza katika kampeni hiyo maalum ya kuchangia damu huku Wilaya ya Rombo ikiongoza kwa kuwa na chupa 86. Same ilikusanya damu na Mwanga 75.

Wilaya zingine na idadi ya chupa kwenye mabano ni Moshi Mjini (49), Moshi Vijijini (32) na Hai (26). Hata hivyo, alisema changamoto kubwa waliyokumbana nayo ni kwa baadhi ya vijana na wananchi kuogopa kupima afya zao.

Katibu huyo alisema kuwa, hili lilijionyesha baada ya idadi kubwa ya waliojitokeza kuchangia damu kukutwa kuwa na damu ndogo huku wengine wakiwa na damu inayowatosha wenyewe na kuwataka wananchi kujijengea dhamira ya kupima afya zao mara kwa mara.

Halamga alitumia pia nafasi hiyo kuwapongeza wote waliojitokeza kwa hiari kuchangia damu na kuwataka wananchi kuendelea na moyo huo kwa kuwa mahitaji ya damu katika hospitali nchini bado ni makubwa huku akiwataka pia kuachana na dhana ya kudai kuwa damu inauzwa wakati inatolewa bure.



# Taasisi yaomba kurudishiwa mali

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

JUMUIYA ya Wakulima Tanzania (Taso) imeomba kurejeshewa mali zake na Wizara ya Kilimo baada ya kupata usajili ili kutekeleza majukumu yake.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti wa Taso, Shaaban Muyombo, alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha Kamati ya Utendaji ya Jumuiya hiyo kilichofanyika jana jijini hapa.

Alisema kamati hiyo inamwomba Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, kurejeshewa mali zao ili kuendelea kutekeleza majukumu yao.

Muyombo alisema awali mali za jumuiya hiyo zilikabidhiwa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa husika kila kanda kutokana na kusitishiwa usajili na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa sababu ya mkanganyiko wa katiba yao lakini wamerekebisha.

Mwenyekiti huyo alisema baada ya marekebisho hayo, walipewa barua ya kurudishiwa usajili wao Julai 3, mwaka huu, na wameshaanza majukumu yao ya rasmi tangu wakati huo.

"Tunashindwa kutekeleza baadhi ya majukumu kutokana na mali za jumuiya kuendelea kushikiliwa na makatibu tawala wa mikoa," alisema.

Alizitaja baadhi ya mali hizo kuwa ni akaunti zote za benki za kanda na taifa, hati za viwanja vya maonyesho ya Nanenane na ofisi.

Muyombo alibainisha kuwa kwa sasa jumuiya hiyo inafanya kazi katika mazingira magumu kwa kutumia fedha za viongozi kutokana na kutokuwa na fedha.

Alisema wanategemea kufanya uchaguzi wa viongozi wa wa jumuiya kuanzia ngazi ya kanda lakini wamekwama kutokana na kukosa fedha za uendeshaji .

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Taifa wa Baraza la Taso, Jaji Mstaafu Edward Mwesiumo alisema jumuiya hiyo inafanya kazi kwa kushirikiana na serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Wizara Mifugo na Uvuvi.

Jaji Mwesiumo alisema Taso inafanya kazi katika kanda tano ambazo ni Kanda ya Kati yenye mikoa ya Dodoma na Singida, Kaskazini (Arusha, Kilimanjaro na Manyara) na Mashariki (Morogoro, Dar es Salaam, Tanga na Pwani).

Alizitaja kanda zingine kuwa ni Nyanda za Juu Kusini yenye mikoa ya Katavi, Mbeya, Songwe, Rukwa, Iringa, Njombe na Ruvuma, na Kusini yanye mikoa ya Lindi na Mtwara.

Katika kikao hicho, wajumbe wote wa kanda hizo walihudhuria kwa kujitegemea kutokana na changamoto ya kushikiliwa kwa akaunti za jumuiya hiyo.

# Sido, viwanda vyapania kuongeza ngozi thamani

**Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) imeweka mikakati ya kuongeza thamani ya bidhaa za ngozi kuanzia inapochunwa hadi utengenezaji wa bidhaa yenyewe.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Stella Manyanya, alisema hayo juzi wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa shirika hilo jijini hapa.

Alisema hatua hiyo ni makubaliano ya pamoja ya viongozi wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) katika mkutano wa 39 uliomalizika hivi karibuni jijini Dar es Salaam.

Manyanya alisema ili nchi hizo zijikwamue kutoka kwenye umaskini ni lazima kuweka msisitizo katika maendeleo ya sekta ya viwanda.

**Katika mazao ya mashambani msisitizo umewekwa kwenye zao la alizeti kwa ajili ya kuzalisha kwa wingi mafuta ya kupikia.**

Alisema moja ya makubaliano katika mkutano huo ni kuboresha thamani ya bidhaa za ngozi ili kuleta ushindani katika soko la kimataifa.

"Hivyo sisi wizara husika tumeweka mikakati ya kushirikiana na Sido kuhakikisha viwanda vingi vinazalishwa chini ya usimamizi wa taasisi hii na tumeamua kuitumia Sido katika hili kwa sababu ndilo shirika lililopo muda mrefu kwa ajili ya kuhudumia viwanda vidogo," alisema.

Naibu Waziri alisema ngozi ina uhitaji mkubwa na uzalishaji wa nchini ni mdogo kulinganisha na idadi ya mifugo iliyopo.

Alisema lengo ni kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa katika viwanda zinaleta ushindani katika soko la kimataifa, jambo ambalo litaleta manufaa kwa taifa.

Manyanya alisema katika mazao ya mashambani, msisitizo umewekwa kwenye zao la alizeti kwa ajili ya kuzalisha kwa wingi mafuta ya kupikia.

Alisema tayari wameanza uboreshaji wa viwanda na wameanza Mtwara katika kiwanda cha kubangulia korosho jambo ambalo limesaidia vijana wengi kupata ajira.

"Tunaendelea kutekeleza azma yetu ya uboreshaji viwanda. Tumefanya hivyo pia Bukoba, Manyara, Katavi, Simiyu na Dodoma kufuatilia utendaji kazi wa Sido lengo likiwa ni kuona viwanda hivyo vinaleta manufaa," alisema.

Aliipongeza Sido mkoa wa Dodoma kutokana na hatua kubwa ya uboreshaji wa maeneo ya shirika hilo jambo ambalo linaonyesha inazingatia malengo yaliyowekwa na serikali katika sekta ya viwanda.



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, akifafanua jambo kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, jijini Dodoma juzi, kuhusu maamuzi ya serikali katika kushughulikia madeni yanayodaiwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), kwa wadaiwa sugu. **PICHA/ WUUM**

# Maofisa elimu maalum wapewa somo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAOFISA elimu maalum na watu wazima wametakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuendana na dira ya nchi inayotaka kuandaa jamii ya watu walioelimika wenye maarifa na ujuzi.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anayeshughulikia Elimu, Tixon Nzunda, alisema hayo juzi wakati akifunga kikao kazi cha maofisa elimu wa mkoa, maafisa elimu maalum na maafisa elimu ya watu wazima, jijini hapa.

Nzunda alisema kuwa nchi yenye uchumi wa viwanda inatakiwa kuwa na watu wanaoweza kushindana, hivyo ni vigumu kufikia malengo bila kuwa na watu wenye maarifa sahihi, ujuzi kamili, kujiamini, wazalendo na wanaoipenda nchi yao kwa ajili ya kuleta mabadiliko ya kweli na maendeleo katika mapinduzi ya viwanda.

Alisema sekta ya elimu ni kubwa hivyo amewaomba kujenga mshikamano, kufanya kazi kama timu na kusaidiana kwa hali na mali ili kuleta mabadiliko katika sekta hiyo kwa kuisaidia jamii kuona umuhimu wa elimu nchini.

"Acheni majungu, mafanikio ya idara yawe ya kila mmoja. Msitengeneze makundi ndani ya idara na ndani ya sekta kwa kuwa sekta ya elimu ni mafanikio ya taifa, watu walioelimika, wanaojiamini, wenye maarifa, ujuzi na wanaoweza kujiamini," alisisitiza Nzunda.

Alisema katika kuleta maendeleo ya elimu nchini, ni lazima kufanya kazi kwa umoja na upendo kwa kuwa bila hivyo hakutakuwa na mabadiliko na kutarudisha nyuma juhudi za serikali.

Aliwataka maofisa elimu nchini kuhakikisha wanasimamia taaluma kuanzia ngazi ya awali, msingi, sekondari na watu wenye mahitaji maalum kwa kusimamia mitaala ya elimu na kuhakikisha maofisa elimu kata wanatimiza majukumu yao kikamilifu ili kuimarisha elimu kuanzia ngazi ya awali.





# Shein apigia debe matumizi Kiswahili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Muhamed Shein, amevitaka vyombo vya habari nchini kutumia vyema lugha ya Kiswahili katika utangazaji na uandishi wa habari.

Akipokea taarifa ya utekelezaji wa Mpango Kazi kwa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Juni, mwaka huu jana, Dk. Shein aliitaka wizara kukutana na wahariri wa vyombo vya habari kuipatia ufumbuzi changamoto hiyo.

Dk. Shein alisema Zanzibar ndiyo kitovu cha lugha fasaha ya Kiswahili, hivyo ni vyema kuitumia kwa ufasaha.

Aliitaka idara ya Habari (Maelezo) Zanzibar kuweka utaratibu mzuri wa kutoa vibali vya kupiga picha na kuhakikisha sheria za nchi zinafuatwa hasa kwa wageni wanaofika Zanzibar kufanya shughuli hizo.

Pia alisisitiza haja ya kuendelea kuzitunza na kuzihifadhi vyema nyaraka za serikali.

**Katika kipindi hicho, wizara ilishughulikia mradi wa kuimarisha maeneo ya kihistoria ya Fukuchani na Makamandume, mradi uliogharimu Sh. milioni 850.**

Kuhusu uendeshaji wa shughuli za makumbusho, Dk. Shein aliitaka idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, kuendelea kuhamasisha jamii ya Wazanzibari, wakiwamo wanafunzi, kutembelea maeneo hayo ili kufahamu historia ya asili ya Zanzibar.

Aidha, alisema iko haja ya kuendeleza uhusiano na ushirikiano mwema uliopo katika sekta ya utalii, kati ya Zanzibar na Indonesia kwa kushirikiana na Chuo cha Utalii cha Bali cha nchini humo.

Dk. Shein aliupongeza uongozi wa wizara kwa kutekeleza vyema majukumu ya kazi zake sambamba na kuandaa kwa umakini mkubwa taarifa za utekelezaji wa mpango kazi.

Naye Waziri wa Wizara hiyo, Mahamoud Thabit Kombo, alisema katika kipindi cha Julai, mwaka jana hadi Juni, mwaka huu, wizara imetekeleza miradi mikuu mitatu, ukiwemo ujenzi wa studio na ofisi za ZBC Pemba kupitia Kampuni ya ujenzi ya Chuo cha Mafunzo Zanzibar. Alisema awamu ya kwanza ya kazi hiyo inayohusisha ghorofa ya chini imekamilika.

Alisema katika awamu ya pili ya ujenzi huo, mkandarasi ataendelea na ujenzi wa ghorofa ya pili, uezekaji, upigaji wa plasta na kupaka rangi.

Pia alisema katika kipindi hicho, wizara ilishughulikia mradi wa kuimarisha maeneo ya kihistoria ya Fukuchani na Makamandume, mradi uliogharimu Sh. milioni 850.

Alisema Wizara imelifanyia matengenezo makubwa eneo la kihistoria la Fukuchani, ili kurudisha sura na haiba yake ya awali pamoja na matengenezo eneo la kihistoria la Mkamandume yanaendeleo.

Waziri alisema matengenezo hayo yanaenga kuziimarisha kuta za asili katika pande tatu za jengo hilo na kuvirudisha baadhi ya vivutio vya asili vilivyomo ndani ya eneo hilo.

Vilevile alisema katika kipindi hicho wizara ilishughulikia mradi wa kuimarisha utalii kwa wote, ukihusisha ujenzi wa kituo cha utalii katika eneo la Kwa Bihole Bungi, mradi utakaotumia Sh. Bilioni 1.3 hadi kukamilika kwake.



Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru 2019, Mzee Mkongea Alli kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar, akigawa chandarua Mwajuma Hassan wa Manispaa ya Singida juzi, baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa jengo la X-ray litakalogharimu zaidi ya Sh. Milioni 21.1. **PICHA: ELISANTE JOHN**

# Watakiwa kujihadhari tishio la mamba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, imewataka wananchi wa Shehia za Mchikichini na Hawaii kuchukua tahadhari maalumu kufanya shughuli za kijamii katika Mto Barafu.

Tahadhari hiyo imetolewa baada ya kubainika kuwapo kwa mamba huku serikali ikichukua hatua za haraka kuondosha kadhia hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema hayo jana baada ya kufanya ziara maalum katika maeneo hayo kwa kukamatwa kwa mamba katika mto hua ambao wameanza kuzua taharuki kwa wananchi wa shehia hizo.

Akizungumza na wananchi, viongozi wa wilaya ya Magharibi A, Ayoub alisema kwa sasa serikali ya wilaya, shehia na wataalamu wa idara ya misitu watafanya kazi kwa pamoja kuondoa tatizo hilo mara moja na kuwawezesha wananchi kufanya shughuli zao kwa usalama.

Mamba hao waliobainika katika Mto Barafu, inasemekana wanatoka katika kituo cha Zanzibar Park baada ya uongozi wa kituo hicho kukiri kuharibika kwa miondombinu wanamofugiwa wanyama hao na pengine baadhi ya mayai kusambazwa na maji yanayopita katika eneo la hifadhi hiyo na kuelekea maeneo ya Mchikichini ambako inakisiwa ni kilomita tatu kutoka katika hifadhi hiyo.

Naye Ali Mwinyi, mtaalam kutoka idara ya Misitu, amekiri kupokea na kuhifadhi baadhi ya mamba waliokamatwa katika eneo hilo na kuwatoa hofu wananchi kuwa bado ni wadogo na hawawezi kuwa na madhara kwa binadamu.

Imebainika kuwa mamba wanne wamepatikana katika eneo la Mto Barafu na kikundi cha vijana 12 ambao wanawakamata mamba hao huku serikali za wilaya na mkoa zikiahidi kuanza kusafisha eneo lote la mto kuanzia kesho kwa kushirikiana na uongozi wa Zanzibar Park, wananchi na wataalamu wa idara ya misitu.

# Tadea yaviponda vyama vya upinzani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Ada Tadea kimetoa tathmini ya hali ya kisiasa nchini na kusema vyama vya upinzani vitapata wakati mgumu kushinda katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ujao.

Kimesema hali hiyo inatokana na kasi ya CCM ya utekelezaji wa Ilani ambao umelenga kuleta maendeleo na ustawi wa jamii.

Hayo yalisemwa juzi na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Juma Ali Khatib, alipozungumza na waandishi wa habari akielezea tathmini ya hali ya kisiasa kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa.

Khatib alisema vyama vya upinzani vimepoteza dira na mwelekeo wa kisiasa na badala ya kujikita katika utekelezaji wa ilani za vyama vyao, vimekumbwa na migogoro ya kisiasa.

Alisema wananchi wengi kura zao zitaelekezwa CCM kutokana na kasi ya maendeleo inayotokana na usimamizi wa miradi ya maendeleo na huduma za jamii.

"Viongozi wa vyama vya upinzani tumepoteza dira na mwelekeo wa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi na sasa tumejikita katika migogoro ya kisiasa," alisema.

Khatib aliongeza kuwa ni vigumu kuiondoa madarakani CCM ambayo viongozi wake wameonyesha uwezo na ubora katika kutekeleza na kusimamia masuala ya maendeleo.

Alitoa mfano wa Rais John Magufuli ambaye alisema ameonyesha uwezo mkubwa katika kipindi cha miaka minne kwa kutekeleza miradi mikubwa ya miundombinu na nishati ya umeme.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Tanzania itakuwa na uwezo mkubwa wa uzalishaji wa umeme, hivyo kutekeleza dhana ya maendeleo ya viwanda.

"Rais John Magufuli ameonyesha uwezo mkubwa wa uongozi katika kutekeleza Ilani ya CCM katika maeneo ya miundombinu na nishati ya umeme," alisema.


Kwa upande wa Zanzibar, alisema CCM itashinda katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kutokana na upinzani kutawaliwa na ubinafsi na uchu wa madaraka.



Soma UK. 14
**DARASA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI AGOSTI 24, 2019



# MCHEZO WA SIRI! INAWEZEKANA HARMONIZE KUIACHA WCB?

UK.16

## BASI SAWA



## Tulivundwe aachia 'Teketea' dawa za kulevya

MWANAMUZIKI anayechipukia wa nyimbo za asili Mariam Mwawalo 'Tulivundwe', amesema kuwa ameshaachia ngoma yake ya 'Teketea' ambayo inapiga vita dawa za kulevya.

Akizungumza na gazeti hili kuhusu wimbo huo, Tulivundwe alisema Teketea umeachiwa katika njia za audio na video kwa lengo kuwafikia watu kwa urahisi.

"Wengi wameanza kuupokea wimbo wangu na kila mmoja amekuwa na maoni yake, lengo langu kubwa ni kuhakikisha kila kijana anakuwa salama dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya," amesema Tulivundwe.



## Saida ampa tano Tibaijuka

MKONGWE wa ngoma za asili, Saida Kalori, amesema katika maisha yake amelelewa vizuri na mbunge Anna Tibaijuka, ambaye anamfananisha kama mama yake mzazi.

Amesema akiwa na umri wa usichana alikuwa akilelewa na mama yake Tibaijuka na kwamba kutokana na malezi yake mazuri bado anapambana kupigania maisha yake ya muziki.

"Namshukuru mama Anna Tibaijuka kwa malezi yake, hajawahi kunichoka ni mwanamke mpambanaji na mimi nafuata njia yake kwa kuendelea kufanya kazi katika muziki kwa muda mrefu licha ya kukabiliana na changamoto nyingi," amesema Saida.



# DARASSA

## AWANANGA WABAYA WAKE

RAPA mkali, Darassa, ambaye ametoa singo yake mpya 'Shika' hivi karibuni, elezwa ndani ya wimbo huo amewasema watu waliokuwa wakimtabiria mabaya.

|Wimbo huo ambao amemshirikisha Maua Sama, kuna maneno ambayo yanaonekana kuwasema watu ambao inadaiwa wanamchukia pale anaposema 'Masharti ya mganga wameyakosea, wamekuja kuzima kumbe wamechochea'.


Vijembe hivyo vinatokana na msanii huyo kudaiwa kuwa kimya kwa muda mrefu kutokana na matumizi ya dawa ya kulevya. Lakini aliporudi kwa kasi ameachia ngoma tatu mfululizo na kuonesha ukali wake katika muziki huo.

## INSTA-TWITTER





**Hii** wiki siichekei, itanikoma. Naitaarifu tu ijue mapema isiseme niliishtukiza- **Idriss Sultan.**



**Kwenye** mahusiano sijawahi kutendwa, nimeoa ila bado sijabahatika mtoto. Mara nyingi tukiwa kambini huwa nakuwa mwenyewe, mke huwa namuacha nyumbani na kambini tunaweza kukaa hata mwezi au hata wiki mbili-**Aishi Manula.**



## Johari: Wakware wapo kila kona

MWIGIZAJI mkongwe wa Bongo Muvi, Blandina Chagula, maarufu kama Johari, ametetea kashfa ya ngono katika tasnia hiyo na kueleza suala hilo lipo katika sanaa tofauti nchini.
Akihojiwa na EATV amesema hakuna vitendo vya uharibifu wa kingono kwa waume na wake za watu, badala yake tuhuma hizo hazina ukweli za kitafiti.
"Hapana mimi sidhani kama tatizo hilo lipo Bongo Muvi peke yake, nahisi hawajafanya tafiti vizuri, wakifanye vizuri zaidi utagundua sehemu zozote hata watu wanaokaa ofisini hivi vitu vipo, " amesema Johari.




**@burudanitele**

**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

## UNASEMAAA...



# RAYVANNY unachosema kinatoka moyoni?

MWANAMUZIKI Rayvanny amesema haumii kuona wimbo wake 'Tetema' haujaingia katika tuzo za Afrima.
Akizungumza hivi karibuni msanii huyo amesema wimbo huo utabaki kuwa mkubwa kutokana na chati za muziki katika mbalimbali duniani unatamba katika nafasi za juu.
"Kuna nyimbo nyingi zimetoka hapa katikati nadhani ndiyo sababu ya kutochaguliwa, nashukuru Tetema inazidi kupaa katika nchi mbalimbali hilo linanipa moyo," amesema Rayvann.

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Punguza** kuvisifia na kuvikweza vitu ambayo huna au uwezo wako wa kua navyo bado haujafikia. Sababu utaishia kuona maisha yako si lolote si chochote na furaha moyoni mwako itaota mabawa, ilihali hakuna kitu kikubwa zaidi ya uhai ulio nao. Usifie huo na shukuru sana kwa hilo-**Nikki wa Pilli.**



**Sura** za mke na mume wa Kitanzania. Wanawake wenzangu tupunguze kuongea sana jamani. Hata mtu akiwa pembeni bado unaongea na mikono kama unaongoza kwaya!!-**Faraja Kota Nyalandu.**



**Kwenye** ile ajali ya moto hapa kwetu moro mimi binafsi nilipoteza wana wa karibu kabisa zaidi ya wanane akiwemo fundi wangu mkubwa wa gari.
Kifupi huku kwetu kila siku tunazika majeruhi, tukizidi kujifunza kumbe maisha ya duniani ni mafupi na ni ubatili mtupu, ndio maana mimi nazidi kusistiza kuwa NIKIFA NICHOMWE MOTO kama hawa wanangu wa Msamvu na watu wa Moro wasipofanya hivyo wakiwemo familia yangu basi laana itawashukia wote-**Afande Sele.**

# Kuumbe!

# MCHEZO WA SIRI! INAWEZEKANA

## HARMONIZE KUIACHA WCB?



HATIMAYE imejulikana kuwa mwanamuzi nyota kutoka WCB, Harmonize, ameomba kujiondoa rasmi katika kundi hilo.

Ukweli wa kujiondoa kwa harmonize umekuja baada ya miezi kadhaa ya uvumi katika mitandao ya kijamii kwamba hali si shwari ndani ya lebo hiyo na msanii huyo yupo mbioni kutimka.

Harmonize anakuwa msanii wa pili kujiengua WCB, mwaka jana Rich Mavoko, alivunja mkataba wake kwa madai ya kudhulumiwa baadhi ya haki zake.

Mmoja wa Wakurugenzi wa kundi hilo, Salam Sharif amethibitisha kwamba Harmonize anabaki katika lebo hiyo kimkataba pekee lakini moyo wake haupo.

Salam wakati akihojiwa na Wasafi radio, amesema harmonize ameandika barua ya kuomba kujiondoa rasmi katika kundi hilo na wakati wowote uongozi utakaa kuangalia namna bora ya kuvunja mkataba.

“Kwa sasa harmonize moyo wake haupo ndani ya WCB ameandika barua ya kuomba kuvunja mkataba wake, sisi kama viongozi tutakutana kujadili suala hilo kwa kufuata kanuni na masharti ya mkataba ili kila upande usiwe na malalamiko,” amesema Salam.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo ni kuwa hawezi kumlazimisha kuendelea na lebo hiyo wakati mwenyewe mtu amesimama kuamini anaweza kuwa peke yake.

“Unapoondoka katika mazingira mazuri ule uhusiano mzuri utabaki, ameshaandika maombi kilichobaki uongozi kujadili na kilichobaki ni kuangalia kuvunja mkataba,” ameeleza.

**KWELI KAJIONDOA?**

Baada ya tangazo hilo kutoka uongozi wa WCB, watu mbalimbali wamejitokeza kutoa maoni yao na baadhi wamekwenda mbali na kuona kama mchezo unafanyika katika kuliteka soko la muziki nchini.

Watu hao wanadai kwamba kuondoka Harmonize ndani ya kundi hilo kirahisi ni jambo gumu na kwamba kile kinachoendelea kama kuna mkakati wa kupanua soko kimkakati.

Harmonize ambaye yupo juu kimuziki anadaiwa kutaka kutengenezwa kuwa adui wa nje wa Diamond, lakini kiundani umoja wao unaimarika huku wakizoa pesa kutoka kwa kila msanii.

Moja ya dhana hiyo inakaziwa na jambo lililokuwa likiendelea katika mitandao ya kijamii ambalo wasanii hao walikuwa wakishindanishwa huku Diamond akielezwa kutakiwa kupinduliwa na msanii huyo.

Jambo la pili ambalo wachambuzi hao wanasema ni mkakati wa WCB kutaka kumuondoa Ali Kiba kuwa mshindani wa Diamond kwa sababu upinzani wao hauleti tija kwenye kundi hilo.

Licha ya dhana hiyo kupingwa na mashabiki wengi wanaomkubali Diamond, lakini wanaokubali dhana hiyo wanadai kimsingi Harmonize hawezi kuachana na Diamond kwa sababu yeye ndiye aliyemuibua mwaka 2015 na baadhi ya biashara wanashirikiana.

Wanaeleza kwa kumtengeneza Harmonize kuwa mpinzani wa Diamond, itawafanya WCB kupata pesa nyingi kwa mchezo wa siri.

Mmoja wa wasanii maarufu wanaokubaliana na dhana hii ni Mkude Simba, ambaye mara baada ya taarifa hiyo aliandika katika ukurasa wake wa Instagram kwamba jambo hilo haliwezekani na kwamba kinachofanyika ni sawa na kukusanya pesa mkono wa kulia na kushoto.

Hata hivyo, viongozi wa WCB wanapingana na dhana hiyo na kueleza ni upuuzi mtupu.



# NGOMA ZA MWANA FA ZILIZOZAA MISEMO USWAZI

**Na Adam Fungamwango**

KAMA kuna wasanii wa kizazi kipya ambao wanapaswa waheshimiwe sana nchini Tanzania, si kwa kuleta mageuzi tu ya muziki huo kukubalika, lakini pia kukuza lugha ya kiswahli ni Hamisi Mwinjuma ambaye maarufu kama Mwana FA.

Hakuitwa Mwanafalsafa kwa bahati mbaya, ukizisikiliza ngoma zake nyingi zina baadhi ya maneno ambayo mtu anapoyasikia inabidi akae na kutafakari.

Ni maneno yanayofikirisha na inamfanya mtu ayachukue kama funzo kwenye maisha yake.

Msanii huyo amekuwa na ushawishi mkubwa katika jamii kutokana na ngoma zake nyingi kupendwa na mashabiki na kuibua misemo au msamiati ya lugha hapa Bongo.

Hii ni kutokana na jinsi alivyokuwa na uwezo wa kutunga nyimbo zinazogusa jamii, akichagua pia maneno yenye uwezo wa kuiteka hadhira.

Zipo nyingi, lakini hizi ni ngoma zake tano tu ambazo majina ya nyimbo hizo yaligeuka kuwa misamiati ya misemo ya mambo mbalimbali kwenye jamii.

**Ingekuwa Vipi**

Ngoma hii ilitoka mwanzoni mwa miaka ya 2000. Iliteka mashabiki wengi kutokana na maudhui ya ngoma yenyewe. Katika ngoma hii, Mwana FA alijaribu kueleza kuwa mara nyingi vitu vinakuwepo duniani kwa kutegemeana na ndiyo maana hiki kipo na hiki kipo. ‘Ingeimba nini Sister P kama asingekuwa Zay B, ingekuwa vipi miti, ingekuwa vipi Bongo mitumba isingehalalishwa, ingekuwa vipi ingekuwa ulipe buku tu kwa kila pumzi...?” ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye ngoma hiyo.

Jina la ngoma hiyo likageuka msemo hapa Bongo, kwani yoyote akitaka kuelezea jambo linalotegemeana na lingine basi atasema ‘Ingekuwa Vipi.’

**Habari Ndiyo Hiyo**

Katika ngoma hii aliyomshirikisha AY, Mwana FA anaelezea vitu mbalimbali yanayotokea ndani ya jamii, kuna vinavyowezekana na visivyowezekana na vya lazima na visivyo vya lazima. Anasema ‘ndiyo maana kwenye kaburi hawaweki AC’. Ngoma hii iliyotoka 2007 ilitamba kinoma na kutengeneza pia msemo kwa Wabongo. Akikutana na mtu yoyote na kumweleza jambo ambalo anayeelezwa atashangaa, au ni jipya kwake, atamwambia ‘habari ndiyo hiyo.’

Hata wale wenye tabia ya kusutana na kuzodoana, atakwenda kwa mgomvi wake na kumpasha, akishamaliza atakwambia tu ‘habari ndiyo hiyo.’

**Unanitega?**

Hapa Mwana FA alikuwa akiwalenga akinadada wenye tabia ya kuvaa nguo zisizokuwa na staha, zile ambazo zinaonyesha asilimia kubwa ya maungo yao.

Baadhi wanavaa kwa sababu ya mazoea na malezi, wengine ni sababu ya kuwavutia wanaume.

‘Mbona miguu iko wazi unanitega? Mbona kifua kiko wazi unanipenda?’ Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye ngoma hiyo.

Hii ilitoka mwaka 2009 ilitokea kupendwa mno na mashabiki wa bongo fleva.

Mitaani sasa ikawa shida. Ngoma ikaza msemo kwa akinakaka. Akipita demu tu akiwa na kanguo kafupi utasikia ‘unanitega?’

**Bado Nipo Nipo**

Jamaa alitoa ngoma mwaka 2008 ambayo maudhui yake yaliacha wengi hoi na baadhi midomo wazi. Akasema kuwa yeye kuoa bado sana kwa sababu kila anapoona madhila wanayoyapata watu waliooa, kama vile kusalitiwa na vituko vingine vya ndani ya ndoa, hashawishiki kufanya hivyo.

Akasema anasubiri kwanza azeeke na siyo sasa, kwani bado yupo yupo tu.

Pamoja kwa kwamba ilikuwa ngoma yenye utatautata hivi, lakini ilitokea kupendwa mno na kuzaa msemo.

Yoyote ambaye bado hajaoa, atasema ‘mimi bado nipo nipo’ na wale ambao hawataki kuoa kwa wakati huo kila mmoja atakwambia ‘bado nipo nipo kwanza’.

**Asanteni Kwa kuja**

Licha ya maudhui murua yaliyomo kwenye ngoma hiyo, lakini kikubwa ni jina la ngoma hiyo iliyotoka mwaka 2016 pia likawa msemo sehemu mbalimbali Bongo.

Kwenye sherehe mbalimbali inapomalizika, washereheshaji watawashukuru wahudhuriaji kwa kuwaaambia kuwa ‘asanteni kwa kuja’, viwanjani na kwenye sehemu zote zenye mikusanyiko hali inakuwa hivyo hivyo.

Wakati mwingine msemo huo unakuwa kama wa mzaha, mtu anapokwenda sehemu na kukosa kitu alichofuata ataambiwa tu kitu hicho hakuna, lakini ‘asante kwa kuja’.



# Vijimambo

1. Hii ndio inaitwa 'nikinywa maji, nakuona kwenye glasi' - Agatha Mbale, Moro Town.
2. Ai weeewe, naoomba - Ebby Mbwambo, Tanga.
3. Hahahaaa, endelea kuomba tu mzee baba, atakupa tu - Maunda Alawi,
4. Duuh, kweli utoto kazi! Kidume kinategemea kabisa kimegewe mkate! - Beneali Moussa, Zenji.
5. Naomba, ukinipa na mie nikinunuliwa soda nakupa - Mauwa Minde, Kibada Kigamboni DSM.
6. Lazima huyo dogo atakua wa Bush Stars, anaiomba picha mkate! - Sultani Ubwa, Kibada DSM.
7. Endelea tu kuomba, huyo siyo mchoyo atakumegea tu - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
8. Kama ulikuwa hujui tafsiri halisi ya neno 'zwazwa', basi ndio hiyo - Beneali Moussa, Migombani Zenji.
9. Naenda kukusemea kwa mama yako umeomba mkate kwa watu ->Julius Anthony, Usagara Tanga.
10. Acha uchoyo wewe, mwenzio anakuomba ndio unaingiza wote mdomo! - Mama Nah, Manzese DSM.
11. Mwache na uchoyo wake, na wewe ukinunua vitu vyako usimpe - Rehema Bwahoja, Buguruni DSM.
12. Dogo utachubuka 'makongoro' kwa kupiga magoti, hiyo picha tuu - Subira Bwahoja, DSM.
13. Jamani, si mngemuambia kama hiyo ni picha tu sio mtu kweli. Ona sasa anavyotia huruma - Dule DSM.
14. Yes, hiyo ndio dawa ya ombaomba. Kesho leteni roli lenye picha ya hela - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
15. Daaah, mjukuu wa 'Matonya' anadhalilika hivi hivi kwa picha tu - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
16. Huyo naye kubwa zima hajajua tu picha na mtu wa ukweli? Muacha achune magoti - Kole, Msata Pwani.
17. Hapo atalifuata gari mpaka wapi kwa kupiga magoti hivyo Magdalena Kachenja, Mabwepande DSM.
18. Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba - Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.
19. Kweli walimu wanakazi. Huyo mpaka aje kujua hiyo ni picha tu si atakua Chuo Kikuu! - Pili Mpanjira DSM.
20. Mmmh, mie mgeni hapa, acha nipite tu! - Abass Ngulunga, Msasani Macho, DSM.
21. We mtoto utagongwa na magari buree. Huyo sio mtu kweli ni picha tu - Bernad Isuja, Makore Dodoma.

**SMS Bomba ya Leo:**

**Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba -Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.**

## PICHA MPYA




**TUMA MESEJI - 0773 477311**




## Kama ipo, hakuna atakayezuia

**Na Adam Fungamwango**

WATU wanaweza kuleta fitina, kuchochea kitu ili mwezake asipate. Mara nyingine huomba yamkute mabaya, lakini kama Mwenyezi Mungu amemsimamia yote hayatamfika kamwe.

Mara nyingi wanachoweza binadamu hawa wabaya ni kuchelewesha tu, lakini kilichopangwa na Mungu kipo pale pale.

Msemo huu unadhihirika kwenye filamu ya 'Kishkwambi'. Imechezwa na baadhi ya wasanii mastaa kama Salim Ahmed maarufu kama Gabo, Sabrina Ally, Mohamed Fungafunga 'Mzee Jengua', Omari Clinton, Kasuku, bi Staa na mwimbaji wa muziki wa taarabu, Hadija Kopa.

Filamu inaanza kwa kuonyesha kuwa kuna maandalizi kabambe ya harusi kati ya Gabo aliyecheza kama Achebe kwenye picha hiyo na mchumba Aminata.

Hata hivyo, harusi hiyo inakuwa na mambo mengi ya kuikwamisha.

Kuna vizabizabina, wanaopita kwa bwana na bi harusi watarajiwa kupandikiza maneno ili kufanya ndoa isifanyike.

Baadhi yao ni Bi Staa, huku mkuu ya fitina zote ni Hadija Kopa, aliyecheza kama shangazi wa bwana harusi Gabo.

Shangazi anapandikiza watu wake waopita huku na huko kueneza propaganda.

Kwanza kabisa Gabo anaambiwa mchumba wake ana jini mahaba, hivyo akimuona linaweza kumdhuru yeye bwana harusi. Pia anaambiwa mchumba wake huyo si mwaminifu. Kwa upande wa pili, Aminata naye anafuatwa na kuwambiwa anayetaka kumuoa ana mwanamke mwingine anayempenda sana, hivyo anatangaza kwa watu kuwa hawezi kumuoa yeye.

Hali hiyo inawafanya wakikutaka kwa ajili ya maandalizi ya harusi yao kusiwe na maelewano, kila mmoja akimlaumu mwenzake. Sababu ya msingi hakuna.

Gabo anakataa mpango wa shangazi yake wa kusitisha kumuoa Aminata.

Lakini alikubali ushauri wa kutokwenda mwenyewe kumuoa, badala yake amtumie mdogo wake, Clinton. Ushauri huo ulitolewa na mganga alikopelekwa Gabo kwa usimamizi wa shangazi yake, Hadija Kopa. Clinton naye ana mambo mengi. Yeye ni mchezaji wa kutegemewa wa timu ya soka mtaani kwao.

Siku ya harusi inaangukia siku ya mechi na wapinzani wao. Gabo na wenzake hawamuoni nyumbani kwa ajili ya maandalizi, inabidi wamfuate uwanjani na gari pamoja na nguo za harusi ili aende akamuwakilishe kaka yake. Aoe kwa niaba yake, kisha ampelekee nyumbani kwa ajili ya kukwepa uchawi wa bi harusi anayesemekana ana jini mahaba.

Clinton anakutwa akiwa katikati ya mechi, hivyo hivyo na jasho anavishwa nguo rasmi za bwana harusi, na sehemu za usoni alizokuwa na majeraha ya soka kwa kuchezewa rafu, anabandikwa plasta.

Kwa bi harusi nako balaa. Bi harusi na dada zake wamekodisha matarumbeta na kigodoro. Lakini kundi hilo likiwa na akinadada wengine waalikwa, lilipokanyaga tu hapo, lilitimuliwa na baba wa bi harusi Mzee Jengua kwa madai ya hawezi kuruhusu ngoma haramu nyumbani kwake. 'Bwana harusi' wa kukodi anafika nyumbani kwa bi harusi na wapambe wake na kabla ya tukio la kufungishwa ndoa anataarifiwa kuwa tayari timu yake imeshafungwa bao moja, kitu ambacho kinafanya aanze kulia. Hata hivyo wapambe wanamwambia mechi bado inaendelea na hapo anaponyamaza.

Ndoa inafungwa, bi harusi anapelekwa kwa mwenyewe bwana harusi halisi. Bi harusi anamuuliza mwenzake kwa nini hakufika, anaongopewa anaridhika.

Mambo yanaanza. Pete aliyovaa Gabo haivuki. Kwa sonara, hospitali kote wakashindwa. Hadija anamwambia Gabo yote hayo ni uchawi wa mkewe.

Ndoa ikaanza kuwa chungu bado mapema. Mke akaona huenda kuna mkono wa mtu. Akamchukua mumewe na kumpeleka 'akasomewe' kwa ustaadhi.

Kisomo kinafanikisha pete kuvuka. Gabo na mdogo wake Clinton wakashtuka na kuona yote yanayotokea ni tabia ya kumuendekeza shangazi yao kwa kufuata kila anachokisema. Na huenda yote yake ni yeye ndiye mhusika mkuu.

Kikao cha wanandugu kikaitishwa. Ndugu wanambana shangazi Hadija na hatimaye anakiri kuwa ni kweli anahusika na matatizo yote na tangu mwanzo amekuwa akiiwekea vipingamizi ndoa ya mtoto wa kaka yake. Alipoulizwa sababu alidai kuwa alichokuwa anataka ni kwamba, Gabo amuoe binamu yake, Mwasiti.

Mwasiti ni binti yake Hadija. Alichokuwa anataka shangazi ni kwamba Gabo asimuoe Aminata, mwanamke kutoka ukoo mwingine, badala yake amchukue binamu yake, Mwasiti.

Ndugu wote wanashtuka na kushangaa kwa wakati mmoja, kwani wanafahamu kuwa Mwasiti asingeweza kuwa mke bora, kwa sababu hana tabia nzuri, pia hajui kupika. Mwisho wa yote Kopa anaomba radhi. Gabo na mkewe wakaanza kuishi kwa amani.




# KAVUKA MPAKA

## SNOOP DOGG AMFANANISHA NIPSEY NA YESU

KATIKA hali isiyo ya kawaida, rapa mkongwe duniani Snoop Dogg, amewashangaza watu baada ya kutoa kauli yenye utata kwa kumfananisha msanii mwenzake sawa na Yesu Kristo.

Snoop eti amemfananisha marehemu Nipsey Huslle kama Yesu kutokana na matendo yake aliyoyafanya hapa duniani kipindi cha uhai wake.

Rapa huyo akekaririwa akisema baadhi ya matendo yake yanakaribiana na yale aliyofanya Yesu miaka 2000 iliyopita.

Snoop amesema alama ambayo ameiacha Nippsey ni kubwa ikiwamo kuisadia jamii yake pamoja na mambo mengine mengi.

Kauli hiyo ambayo kwa sasa imeubua mijala mikali kwenye mitandao ya kijamii ameitamka alipokuwa akifanyiwa mahojiano kwenye kipindi cha The Breakfast Club.

"Angalia athari aliyokuwa nayo, athari ile ile Yesu alikuwa nayo," alisema.

"Watu wengi hawakumjua, lakini hakika walitaka kujua juu yake mara tu atakapofariki. Halafu mara walipogundua juu yake, walielewa ni nini urithi wake. Sasa, urithi wake unaishi zaidi na yeye kutokuwa hapa. Ndio maana nasema, 'Sijawahi kumuona Yesu, lakini nimekuwa nikisikia juu yake;"ameongeza kusema.

Snoop alizidi kutoa kile anachokiamini juu ya jinsi Nipsey karibu anavyoonekana kama Yesu.

"Tuna imani zaidi kwake na tunajua ikiwa unaamini kwake, hii itafanyika kwasababu babu zako na bibilia imekuwa ikikupa habari hii yote," akaongeza "Ni kama, ndivyo alivyo. Tulipoenda, ndivyo atakavyokuwa kwa sababu huwezi kumgusa, huwezi kumuona, una picha zake tu na sura yake inaonekana kama Yesu. Umbo la mfupa, macho…"

Hata hivyo kumekuwepo na mgawanyiko wa maoni kati ya wafuasi wake ambao wapo wanaopinga dhana hiyo na wapo wanaomuunga mkono wakisema msanii huyo amefananisha kwa matendo wala si nafasi na hadhi aliyokuwa nayo Yesu.

# Larry King, Shawn watalakiana tena



UNAWEZA kusema mwaka 2019 ni mbaya kwa ndoa za mastaa kuvunjika, sasa ni zamu ya mtangazaji maarufu Larry King ambaye ametalakiana na mkewe Shawn King.

Ripoti za uhakika zinasema tayari wanandoa hao wamefungua maombi ya kupeana talaka na sababu kubwa ya kuachana ni kuwa na mambo tofauti yasiyoweza suluhishwa.

Hii ni mara ya pili kwa Larry King na Shawn King kuachana tangu mwaka 2010 walivyofanya hivyo na kurudiana. Shawn anakuwa mwanamke wa saba kutalakiana na staa huyo.



## Jamani Katie hukuweza kupatana na Foxx?

MASTAA wengine ambao hawakuachwa na dudu baya wa mwaka 2019 ni mwigizaji wa Hollywood Katie Holmes ambaye ameachana na mpenzi wake Jamie Foxx baada ya kuwa katika uhusiano zaidi ya miaka sita.

Kulingana na taarifa za uhakika zinasema mshindi huyo wa tunzo za the Oscar alionekana jijini Los Angeles usiku wa Ijumaa iliyopita Sela Vave.

Sababu kubwa ya mapenzi yao kuyeyuka inatokana na tuhuma za Foxx kumsaliti Katies kuwa na wanawake wengine.

## Wizkid unajua kuwarusha watu roho

WIKI hii mashabiki wa mwanamuziki Wizkid, walipatwa na mshangao baada ya kukuta ukurasa wa Instagram wa msanii huyo kuwa mtupu.

Wizkid ambaye ana jumla ya wafuasi milioni 8.2 wanaomfuatilia kila siku, alifuta picha zote katika ukurasa wake na kuibua mjadala mzito mitandaoni.

Tukio hilo limewafanya mashabiki wake kua na maswali mengi kuhusu msanii huyo, lakini hakuna taarifa yoyote kutoka kwa Wizkid inayofafanua jambo hilo.





## Burna Boy wape wafurahie

MKALI wa muziki kutokea Nigeria, Burna Boy, amezidi kuwapagawisha mashabiki baada ya wiki hii kuachia ngoma yake mpya 'Pull Up' ambayo ipo ndani ya albam yake.

Albam yake hiyo ya nane 'African Giant' aliyoiachia rasmi July 26,2019, imekuwa na ngoma nyingi kali lakini baadhi yake hakuzitambulisha.

Mwimbaji huyo ambaye amekuwa miongoni mwa wanamuziki wa Afrika Walioshirikishwa katika albamu ya Beyonce inaitwa The Lione King, amekuwa akifanya vizuri katika muziki Afrika.

## Drake aiba midundo 'In My Feelings'

SHUTUMA za kuiba nyimbo zimezidi kuwaandama wanamuziki nyota wa Marekani, safari hii rapa Drake amefunguliwa shtaka la kuiba mdundo wa ngoma ya 'In My Feelings'.

Anayelalamika ni Samuel Nicholas III ambaye anadai Drake alichukua midundo hiyo kwenye ngoma yake halali ya 'Roll Call' na kudai kuwa hakulipwa chochote na mwanamuziki huyo.

Wimbo wa 'In My Feelings' iliachiwa rasmi Agosti 3, mwaka jana katika mtandao wa You Tube ambapo mpaka sasa imetazamwa na jumla ya watu Mil.200.





## MIONZI YA SHERIA

# Jinsi ya kulinda mirathi ya mwenye ulemavu kiakili

**Na John Juma**
**0716217615**

MIRATHI ya mtoto mdogo na yule asiyekuwa na akili timamu hushikiliwa au kusimamiwa na nani kwa niaba yake? Hilo ni swali ambalo pengine wenye kuishi na wahitaji hao wanajiuliza.

Kwa kawaida mtu anapofariki huacha warithi wa namna mbalimbali yumkini katika wahusika anaweza kuwamo mtoto au watoto wadogo wenye umri kuanzia miaka ziro mpaka 18 au hata wasio na akili timamu wakati mwingine.

Tafasiri zaidi juu ya wahusika hao inaweza pia kupatikana kwenye vifungu vya 3 na 4(1) vyote vya Sheria ya Mtoto Tanzania ya mwaka 2009.

Tunapoangalia suala hili mwongozo wa sheria hiyo elekezi, unasemaje kwa mtoto mdogo? Kifungu cha 23 cha Sheria ya Mirathi Tanzania kwenye sura ya 352 kina sema kuwa urithi au hati ya kusimamia mirathi haiwezi kutolewa kwa mtoto mdogo.

Tukiachana nahilotujue kuwa ikiwa mtoto mdogo siyo mrithi pekee isipokuwa wapo ndugu zake wengine ambao ni warithi. Kwa hiyo basi mmoja wao muadilifu anayeaminiwa atateuliwa kusimamia mirathi yote ikiwemo ya mtoto mdogo. Msimamizi huyo atakuwa na wajibu wa kuhakikisha anatunza mali ya mtoto au watoto hao hadi wanapokuwa na kufikia uwezo wa kutunza mali zao binafsi.

Pili pale ambapo mtoto au watoto wadogo ndiyo warithi pekee wa mali, yaani hakuna mkubwa kati yao.

Ikiwa hilo litatokea basi mlezi wa mtoto au watoto hao anaweza kuiomba mahakama kusimamia mirathi hadi watakapokua wamefikia umri wa miaka 18.

Taasisi ya udhamini (trust cooperation), pia inaweza kuomba au kukabidhiwa bila kuomba jukumu la kusimamia mali za watoto hadi watakapokuwa wameshatimiza umri wa miaka kumi na nane .

Kifungu cha 22 cha Sheria ya Mirathi ,sura 352 kinahusika na kuelekeza utekelezaji wa jukumu hilo.

Hivyo basi, yeyote atakayeteuliwa kati yao atakuwa na wajibu mkubwa wa kuhakikisha anatunza mali za mtoto au watoto hao kwa kadri mahakama itakavyoelekeza.

Isitoshe, wakati mwingine wanaweza kujitokeza walezi wengi kila mmoja pengine akitaka kusimamia mali za watoto husika.

Ikiwa hivyo , suala zima litapelekwa mahakamani ili iamue nani hasa kisheria anafaa kusimamia mali hizo kwa kuzingatia zaidi mustakabali wa baadaye wa mtoto au watoto hao. Kwa mtoto mdogo asiye na akili timamu, kifungu cha 23 cha Sheria ya Mirathi ya sura ya 352, kinakataza kabisa mtu asiye na akili timamu kusimamia mali au kupewa hati ya kusimamia mirathi. Hii haijalishi hata kama ni katika mazingira, ambayo mtajwa ndiyo mrithi pekee ni lazima apate msaada.


Tena, kifungu cha 37 cha sheria hiyo hiyo kinasema, ikiwa mtu anayestahili kurithi au kusimamia mirathi hana akili timamu, basi mali zake zitatunzwa na mtu, ambaye anamtunza mhusika huyo.

Yaani, atasimamia mali hizo kwa maslahi ya mlengwa. Lakini, kama (endapo) kutakuwa na pingamizi lolote litakaloibuka kuhusu mhusika kusimamia

za asiye na akili timamu. Maombi yatatakiwa kupelekwa mahakamani sambamba na sababu za mlengwa kudhani mhusika hafai kabisa kutekeleza majukumu hayo.

Ni muhimu sana. Mlengwa,msimamizi huyo wa mali za mirathi kwa niaba ataruhusiwa kutumia fedha inayotokana na sehemu au mali husika kwa matumizi ya mtoto au watoto hao; ikiwa tu ni aina ya mali zinazoweza kuzalisha kipato cha ziada. Mfano nyumba na magari, mashamba.

Kwa matumizi (muhimu) kama vile mahitaji ya chakula, mavazi, malazi, matibabu, elimu kwa ustawi chanya wa mhusika au ni mtoto au watoto hao.



## KALAMU YA MWALIMU

# Fursa lukuki za Kiswahili, tunajipangaje Watanzania?

**Na Reubeni Lumbagala**

WAHENGA walisema nyota njema huonekana asubuhi. Na hili limedhihirika pasi na shaka; nyota ya lugha ya Kiswahili kung'aa mapema. Hii ni kutokana na serikali kuweka mkazo wa matumizi yake katika shughuli mbalimbali za kitaifa na kimataifa.

Mkazo huu umesaidia kurudisha hadhi ya lugha ya Kiswahili iliyoanza kupotea miaka ya nyuma na kwa sasa heshima ya Kiswahili imerejea kwa kishindo kikubwa kwa kuvuka mipaka ya Tanzania.

Siku chache zilizopita, Mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), ulimalizika ambapo Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mkutano huu wa kihistoria wa maendeleo ya nchi zilizo kwenye ukanda wa kusini mwa Afrika na tena Kiswahili kikatumiwa.

Katika mkutano huo, Rais John Magufuli alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa SADC kwa kipindi cha mwaka mmoja akipokea kijiti hicho cha uongozi kutoka kwa Rais wa Namibia Hage Geingob.

Kabla ya Mkutano huu, lugha rasmi ambazo zimekuwa zikitumiwa na nchi wanachama wa SADC katika shughuli na mikutano yao ni lugha ya mkoloni ya Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Lakini historia mpya imeandikwa katika mkutano ulioisha siku chache jijini Dar es Salaam ambapo lugha ya Kiswahili imepitishwa kuwa lugha rasmi ya kutumika katika shughuli za SADC na kufanya lugha rasmi ziongezeke kutoka lugha tatu na kuwa lugha nne.

Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, alikuwa na ndoto za kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya Afrika. Alipigania sana lugha hiyo iwe lugha rasmi lakini ni jambo la faraja kuona kuwa hata kama Baba wa Taifa hayupo hai leo lakini ndoto yake hiyo imetimia kwani sasa Kiswahili lugha adhimu inatumika katika Jumuiya nyingi za Afrika kama Umoja wa Afrika (AU), Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na sasa SADC. Pia, lugha hii inatumika na kufundishia vyuo vikuu mbalimbali vya bara la Afrika na mabara mengine kama Asia, Amerika na Ulaya, hali iliyochangia ongezeko kubwa la watumiaji wa Kiswahili.

Kutokana na Rais Magufuli ambaye ni Mwenyekiti kupia chapuo na kuifanya lugha ya Kiswahili kutumika katika shughuli za SADC, nchi 15 za Jumuiya ya SADC, ukiachilia Tanzania ya 16, watahitaji walimu wa Kiswahili.

Hili ni soko kubwa ambalo linaweza kuwasaidia vijana wa Kitanzania kupata ajira za kufundisha Kiswahili.

Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa, amekuwa mdau mkubwa wa lugha hiyo kwa kuanza kujifunza lugha ya Kiswahili kwa juhudi kubwa. Rais Magufuli alipohudhuria sherehe za kuapishwa kwa Rais Ramaphosa, alimpelekea zawadi ya vitabu mbalimbali vya Kiswahili ili aweze kuvitumia na kujifunza.

Ni jambo la kufurahisha kuona miezi michache tu imepita, Rais Ramaphosa ameanza kuzungumza na kuandika Kiswahili fasaha.

Vilevile, serikali inayoongozwa na Rais Ramaphosa imepitisha lugha ya Kiswahili kuanza kutumika kufundishia katika shule za Afrika Kusini mapema mwakani.

Azma hii inatoa fursa za ajira kwa walimu wa Kiswahili kwenda kufundisha katika shule na vyuo vya Afrika Kusini. Lakini mara zote, fursa hazisubiriwi zimfuate mtu bali fursa hufuatwa na kuchangamkiwa.

Kama Watanzania tutabaki nyuma katika kuchangamkia soko la kufundisha Kiswahili, wenzetu wa nchi jirani kama Kenya, Uganda na Rwanda watachukua nafasi hizo na sisi kubaki kuwa watazamaji na walalamikaji.

Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) limefanya kazi nzuri ya kuandaa kanzidata (database) ya wataalam wa lugha wa Kiswahili wanaohitimu katika vyuo mbalimbali hapa nchini kwa kukusanya taarifa zao na vyeti vyao vya kitaaluma.

Kanzidata hiyo ni maalum kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa walimu hao wa Kiswahili pindi fursa za kufundisha Kiswahili zinapojitokeza hasa nje ya nchi.

Nitoe wito kwa mabalozi wetu wanaowakilisha nchi yetu katika nchi mbalimbali ulimwenguni kuwa vinara wa kutafuta fursa kwa ajili ya watanzania kwenda kufundisha lugha ya Kiswahili katika nchi wanazofanya kazi zao. Ni wakati wa kutumia diplomasia ya lugha katika kukitangaza Kiswahili kwani wapo walaji wengi wa bidhaa hii adhimu ya lugha ya Kiswahili.

Pia pongezi ni kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Paul Makonda,mara baada ya kumalizika kwa mkutano wa SADC ameanza jitihada za kuwasaidia walimu wa mkoani humo kupata fursa za kufundisha Kiswahili nje ya nchi.

Makonda alisema "Tutachangamkia hii fursa ya kuhakikisha walimu waliopo kwenye mkoa huu ambao hawajapata kazi, kwa kuwasiliana na Wizara ya Mambo ya Nje ili wakafundishe lakini pia walimu ambao watataka kuanzia mkoani, wanaweza kuanzia kwa Ofisa Elimu Mkoa ili kuchangamkia fursa hii muhimu".

Pamoja na hilo upo umuhimu wa kujifunza lugha nyingine za kimataifa kama Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kireno na Kichina ili kuweza kuwa walimu wazuri kwa nchi zinazotumia lugha hizo katika kuwafundisha Kiswahili. Tafakari

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

***Maoni: 764 666349.***

# Kampeni dhidi ya udhalilishaji yaanza kuzaa matunda Pemba



Nyumba ya familia wanayoishi wasichana ambao walitelekezwa eneo la Selemu, Sheria ya Selemu Wilaya ya Wete kisiwani Pemba, baada ya kufanyiwa ukarabati na msamaria mwema. **NA MPIGAPICHA WETU**

**Na Theodatus Muchunguzi**

KAMPENI ya pamoja ya wadau mbalimbali dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia imeanza kutoa mafanikio katika baadhi ya maeneo hususan Wilaya ya Wete, kisiwani Pemba, kutokana na matukio mengi kuanza kuripotiwa katika mamlaka husika na wahusika kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Taarifa hizo za kutia moyo kutokana na kushamiri kwa vitendo vya udhalilishaji kisiwani Pemba zimebainishwa na Ofisa wa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Wete, Haroub Suleman Hemed, akisema kwamba:

"Haikuwa kazi rahisi kufikia hapa tulipo. Imetuchukua miaka kadhaa kuhamasisha watu kuhusu masuala yanayohusiana na udhalilishaji wa kijinsia, ambao kwa kiasi kikubwa unawaathiri wanawake na watoto."

"Angalau sasa watu wanapata uelewa kuhusuana na masuala ya udhalilishaji na sasa wanaripoti matukio hayo katika mamlaka husika," ofisa huyo aliwaeleza waandishi wa habari kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa-Zanzibar).

Kwa mujibu wa Hemed, kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, hali ya udhalilishaji wa kijinsia ilikuwa mbaya katika wilaya hiyo, ambayo ina jumla ya shehia 36, lakini sasa mambo yanaboreka ambapo matukio mengi yanaripotiwa, huku wahusika wakifikishwa mahakamani na kuhukumiwa.

Hemed anatoa mfano kwa kubainisha kuwa kati ya Januari na Juni, 2018, jumla ya matukio 73 yaliripotiwa katika mamlaka husika na kwa kipindi hicho kwa 2019, yameripotiwa 47, huku naadhi ya wahusika wakihukumiwa.

Hemed anaonekana kuridhishwa na hatua zinazochukuliwa na kusababisha kupungua kwa idadi ya matukio na kueleza zaidi kwamba:

"Hii isingewezekana bila ushiriki wa dhati wa viongozi kuanzia ngazi za chini hadi ngazi ya wilaya pamoja na ngazi ya taifa. Katika ngazi ya chini tunafanyakazi na waratibu wa masuala ya udhalilishaji was kijinsia ambao wapo kila shehia, ambao wanaripoti ofisini kwetu.

"Pia wanaripoti matukio hayo Polisi na kituo cha one-stop center ambacho kilianzishwa katika wilaya hiyo kwa ajili ya kushughulikia matukio ya udhalilishaji wa kijinsia," anasema Hemed na na kuongeza kuwa mamlaka za wilaya ziliuda kamati maalum ya kumlinda mtoto, ambayo inajumuisha wataalamu 12.

Zaidi anaeleza: " Jitihada hizi zote zinaendana na Mpango wa Taifa wa Zanzibar wa kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA-VAWC), 2017-2022, ambao unaeleza azma ya serikali kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na watoto."

"Jitihada hizi zimesaidia katika kuboresha kampeni dhidi ya udhalilishaji katika wilaya hii, ambayo ina wakazi zaidi ya 300,000," anasema Hemed, anapozungumzia mchango wa vyombo vya habari nchini kupitia Tamwa Zanzibar katika vita dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia.

Mratibu wa Tamwa- Zanzibar kisiwani Pemba, Fathiya Mussa, anataja utekelezaji, utoroshaji, vipigo na ubakaji kuwa ni matukio yanayoongoza kwa udhalilishaji katika kisiwa hicho.

Anasema kwamba kuna matukio kadhaa ya familia na wanawake ambao wametelekezwa na waume zao, hali ambayo imechochea udhalilishaji wa kijinsia.

Hata hivyo, uibuaji wa matukio ya udhalilishaji kijinsia umeanza kuzaa matunda kutokana na waathirika kupata misaada. Kwa mfano, baba aliyetekeleza mke na watoto wakiwamo wa kike wawili, kisha mama yao kuolewa mahali pengine, watoto hao wameanza kupewa msaada na wasamaria wema.

Tamwa Zanzibar ndiyo iliyowezesha misaada hiyo baada ya mmoja wa mwanahabari inaoshirikiana nao (young fellow) kuibua matukio ya udhalilishaji kijinsia kuibua tukio hilo na kuriripoti kwenye vyombo vya habari.

Kuibuliwa kwa tukio hilo kuliwaibua wasamaria wema na kuwapa misaada kadhaa ikiwamo kuwapati vyakula sabuni, fedha taslimu, kuwakarabatia nyumba yao kwa kuiezeka kwa bati, kuipaka rangi, kuweka dari na sakafu katika eneo la Selemu, Sheria ya Selemu Wilaya ya Wete.

Mmoja wa mabinti hao, Shahida Abdallah (22), anasema ameshajifunza shughuli za kupiga picha za video, hivyo anaamini kuwa akipata msaada wa kamera anaamini kuwa itamsaidia kujiingizia kipato cha uhakika cha kuendesha maisha yake.

Mdogo wake, Mariam Mbarouk Salum (18), anaeleza kuwa shughuli anayotaka kuifanya ni ya ushonaji ikiwa atapata mafunzo na msaada wa cherehani.

Mabinti hao wanaoishi pamoja katika nyumba hiyo, wanawashukuru wadau wa kupambana na udhalilishaji hususan Tamwa kwa kuibua tukio hilo ambalo limewafanya waishi bila msaada kwa kipindi kirefu baada ya kukumbwa na mkasa wa kutelekezwa na kubaki bila msaada.

Uibuaji wa matukio ya udhalilishaji pia umemsaidia mama mmoja, Fatma Issa (26), mkazi wa Shehia ya Ole Mjini Wilaya ya Chacke Chake, ambaye anasema kuwa alitelekezwa na mumewe na kuondoka nyumbani hapo zaidi ya takribani miaka mitatu na kumuacha na watoto wadogo wawili wa kiume kabla ya kuolewa na mwanauke mwingine.

Kuibuliwa kwa tukio hilo kumemwezesha mtoto wake mkubwa kuandikishwa na kuanza masomo ya darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Ole mwishoni mwa Julai 390, mwaka huu, baada ya kuwezeshwa na Tamwa Zanzibar kwa kumpatia mahitaji mbalimbali muhimu ya ya shule.

Februari mwaka huu, Mfuko wa Idadi ya Watu wa Umoja wa Mataifa (UNFPA), uliisaidia Serikali ya Zanzibar kutekeleza NPA-VAWC, ambao unajumuisha kuwajengea uwezo polisi, ambao wapo mstari wa mbele katika kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

UNFPA iliahidi kuendelea kusaidia ukarabati wa jengo la Dawati la Jinsia la Polisi, ambalo kinatoa mchango muhimu kwa kujenga uaminifu kati ya polisi, wanawake na watoto, na kupalilia njia ya kupatikana kwa haki, kitu ambacho hakikuwapo kabla.

Mfuko huo pia umeahidi kuongezea polisi rasilimali kwa ajili ya kuchunguza kesi zinazohusiana na matukio ya udhalilishaji na kuwafikisha wahusika katika mkono wa sheria.

Jitihada hizo pia zinaonekana kuanza kuzaa matunda katika Wilaya ya Chake, ambapo jumla ya kesi 45 za udhalilishaji wa wanawake na watoto zimeripotiwa katika Ofisi ya Wilaya hiyo Mkoa wa Kusini Pemba kuanzia Januari hadi Julai mwaka huu.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Rashid Hadid Rashid, anasema hali ya matukio ya udhalilishaji mwaka huu yameongezeka kwa kesi 15 ukilinganisha na mwaka jana.

Alisema kuanzia Julai hadi Disemba mwaka jana Ofisi hiyo ilipokea kesi 30 za udhalilishaji wa wanawake na watoto, ambapo mwaka huu wamepokea jumla ya kesi 45.

Anataja sababu ya kuongezeka kwa kesi hizo ni kutokana na wananchi kupata mwamko wa kuyaripoti matukio hayo kwenye vyombo vya sheria.

"Zamani wananchi hawakuwa na utamaduni wa kuripoti matukio haya ya udhalilishaji kwa kuona aibu, na ndio maana yalionekana kuwa kidogo, lakini kutokana na mwamko wanaoupata sasa wanayaripoti kila siku bila ya woga," anaeleza Mkuu huyo wa wilaya.

Alieleza kati ya kesi hizo zilizoripotiwa, ubakaji ni kesi 30, ambapo mwaka jana ziliripotiwa tisa na mwaka huu zimeripotiwa 21.

"Pia kuna kesi za utelekezwaji wa watoto, ambazo kinababa hutelekeza familia zao ama kwa kwenda dago au kuwapa talaka wake zao, jambo ambalo linasababisha kuongezeka udhalilishaji," anabainisha Rashid.

Anawataka wanaume kuacha tabia ya kutoa talaka kiholela, ili kupunguza vitendo vya udhalilishaji na ukatili kwa wanawake na watoto.

Aidha anawaomba wazazi na walezi kushirikiana katika kurejesha malezi ya zamani ya kuwalea watoto kwa pamoja, jambo ambalo litasaidia sana kupunguza udhalilishaji ndani ya jamii.

"Pia muhali (aibu) ni tatizo kubwa linaloikumba jamii yetu ambayo husababisha kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji siku hadi siku, hivyo wananchi waache rushwa muhali na watoe ushahidi mahakamani," anasema.

**MAKALA**

# Tatu: Obama, uhamasishaji vimenitoa kiuchumi

**Na Gaudensia Mngumi**

LINAPOTAJWA jina Barack Obama wapo wanaokumbuka jambo moja pekee nalo ni, Rais wa zamani wa Marekani. Lakini kwa Tatu Abdallah Mahupa (Tama), sivyo.

Mwanamama huyu anachokiwaza pale Obama, anapotajwa ni mpenyo mkubwa (mafanikio) alioupata kwenye biashara wakati rais wa zamani wa Marekani alipoapishwa.

Tatu mfanyabiashara anayeishi Tandahimba mjini mkoani Mtwara hivi karibuni alizungumza na Nipashe iliyokuwa wilayani humo na kueleza kuwa ujio wa Obama madarakani ulikuwa siku kubwa.

"Nilikuwa mwanamke na mfanyabiashara wa kwanza Tandahimba kununua runinga, kuiweka uwanjani na kuonyesha watu usiku kucha tukio la kuapishwa Obama huko Washington."

"Siwezi kuisahau Januari 2009. Ndiyo siku niliyouza bidhaa kuliko siku zote (hakutaja kiasi) niliuza watu walijaa kwenye uwanja wa duka langu kuangalia TV kuanzia asubuhi saa 4 hadi saa 7 usiku kushuhudia mbashara kiapo cha Obama.Kila kilichorushwa kuhusu Obama nilikitangaza. Hakika niliuza na kupata mafanikio makubwa. "anasema Tatu.



Sofia Mnalombe akizungumza kwenye mkutano na wadau wa haki za mabinti na kinamama (hawapo pichani) **PICHA ZOTE: GAUDENSIA MNGUMI**



Tatu au Mama Tama, akihudumia mteja dukani kwake Tandahimba .

Anasema aliuza soda, vitafunwa, sigara, pipi, chakula na kwa ujumla siku hiyo ilimpandisha chati na kuandika historia katika maendeleo ya wanawake wajasiriamali.

Mfanyabiashara huyu ni maarufu kama Tama, kifupisho cha majina Tatu Abdallah Mahupa, na anachojivunia pamoja na kuwa mfanyabiashara wa kwanza kumiliki na kuonyesha runinga uwanjani huko Tandahamimba, ni kuwa wa kwanza kukodisha viti na maturubai mjini Tandahimba.

Anakiri kuwa ni tofauti na wanawake wengi katika maeneo ya Mtwara na Lindi ambako kuna mfumo dume unaowalazimisha wanawake kutegemea mume kwa asilimia 100, lakini pia ni sehemu talaka holela zilipokubuhu.

Licha ya eneo hilo kuwa maarufu kwa kilimo cha korosho, muhogo na ufuta, kinamama wengi hawana mashamba wala kauli juu ya mazao wanayoshiriki kuyazalisha.

### CHIMBUKO MAFANIKIO

Tama anaiambia Nipashe kuwa amehamasika kufanya biashara na kumiliki mali hasa ardhi na ni miongoni mwa wakulima wakubwa waliouza korosho mwaka huu kutokana na mabadiliko na hamasa za kutaka wanawake wagutuke.

'Nimeuza kilo 4500 za korosho katika chama cha msingi cha AMCOS Mchichira Leka Tulage." Anasema Tama na kwamba anamiliki shamba na viwanja pamoja na makazi aliyoyajenga kwa juhudi binafsi.

Anaeleza kuwa alikuwa mjasiriamali tangu akiwa Mbagala jijini Dar es Salaam, huko alikuwa akiuza chapati na kupeleka vitambaa vya nguo za kike nyumbani kwao Tandahimba kuuzia wateja mbalimbali mjini na nje ya mji.

### HAMASA KWA WANAWAKE

Tama mwenye miaka 40 anakiri kuwa kampeni zilizofanywa na mashirika mbalimbali ya kijamii kuhamasisha wanawake kuamka kuwekeza ili kubadili maisha yao Tandahimba na maeneo mengine mkoani Mtwara, yanaamsha ari mpya.

Anasema wengi wanamiliki ardhi kutokana na juhudi binafsi na wanajua kusimamia haki zao hasa wale wanaonyanyaswa kiuchumi.

Maelezo yake yanathibitishwa na baadhi ya wanawake wengi wanaosema mkoani Mtwara kuna mwamko wa kujitambua kutokana na mafunzo mbalimbali ya kuwahamasisha kinamama kudai haki zao na kujikita kwenye kwenye ujasiriamali.

Mathalani, hamasa imekuja kutokana na kampeni mbalimbali zilizofanywa na wadau wakiwamo shirika la kimataifa la Action Aid, Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa) ambao wamekemea ukatili na kuhamasisha mabadiliko na hasa kupinga talaka holela na kutelekeza wanawake na watoto.

Akizungumzia uhamasishaji katika ziara ya hivi karibuni iliyofanywa na wanahabari na maofisa wa Action Aid, kuangalia mafanikio baada ya kampeni za uwezeshaji kinamama, Mratibu wa shirika hilo Tandahimba na Newala, Dinno Celestine, anasema:

"Mafunzo yametolewa kukabiliana na unyanyasaji na kudai haki za kinamama, tumewafunza masuala ya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia GBV, pia ukatili dhidi ya wanawake (VAW) na ukatili dhidi ya watoto- VAC na kuwapa mikakati ya kudai na kulinda haki zao na zile za kushirikishwa kwenye uongozi."

Wanawake pamoja na kupewa mafunzo ya ujasiriamali na kuanzisha vikundi vya uzalishaji pia wanajizatiti kumiliki ardhi, mazao kama korosho na kufanyabiashara, anaongeza.

Mathalani ziara hiyo ilifika katika kijiji cha Pachoto kilichoko wilayani Newala na kukuta wanawake waliohamasika wakieleza kuwa baada ya mafunzo ya Action Aid, wamewekeza kwenye miradi ya kutengeneza batiki, kulima uyoga, kubangua na kuuza korosho.

Mwaka 2006, shirika hilo la kimataifa katika kupambana na umaskini liliwasaidia wanawake wengi kuhamasika na kuanzisha asasi ya kutetea haki zao ya Newora_(Newala Women Rights Association), anasema Mratibu Celestine.

Mwenyekiti wa Newora Wilaya, Sophia Mnalombe, akielezea zaidi anasema asasi hiyo ina wanachama takribani 8,000 na kwamba kazi za asasi hiyo zimesambaa katika kata 18 kati ya 24 za wilaya hiyo.

Mnalombe anasema baada ya mafunzo wanajisimamia na kujitetea mathalani wakipewa talaka kiholela wanahoji sababu.

"Zamani wanawake wakitalikiwa walikuwa kimya na waoga hawaulizi sababu za kuachwa kiholela. Siku hizi zama zimebadilika."

### KUTUMIA SHERIA

Aidha, Mnalombe anaeleza kuwa zama hizi wanasimamia na kuhoji mgawo wa mali za familia kwa misingi ya sharia, mambo waliyojifunza kwenye uwezeshaji na kutumia mgao wanaopata kuanzisha biashara zao.

"Zamani wanawake walipoachwa wakirudi kwa wazazi wao waliambiwa tumwachie Mungu lakini sasa sivyo. Mwanaume anapotoa talaka mwanamke anataka mgawo wa mali ufanyike kwa maandishi na kuwe na mashahidi," anasema Mnalombe.

"Tunapotetea haki tunawahamasisha viongozi wa vijiji kushiriki kwenye mazungumzo mathalani watendaji wa vijijji na vitongoji. Wawepo kwenye mashauri mbalimbali iwe unyanyasaji, talaka na kutelekeza familia.Hii imezuia talaka kumwagwa ovyo."

### KAMATI ZA HAKI

Katika kuwawezesha wanawake kudai haki zao Mratibu wa Action Aid, Celestine, anaeleza kuwa kwa kushirikiana na jamii hizo waliunda kamati za vijiji za kutetea haki za wanawake na watoto(VWRC).

Swahiba Gatamo ni mjumbe wa kamati ya Kijiji cha Amani wilayani Newala ya kutetea haki za wanawake na watoto.

Anasema : "Tunaposikia kuna malalamiko tunayafuatilia na kuyafikisha kwa viongozi wa kijiji. Tunachukua maamuzi yao hadi kwenye ofisi ya mtendaji wa kata. Tunafuatilia kila jambo hatua kwa hatua na kupata ufumbuzi."

Gatamo anaeleza kuwa wanafuatilia masuala kama kutelekeza watoto, haki za wajane, wanapodhulumiwa na kuwatetea kupitia Newora na serikali za vijiji.

Akizungumzia faida za kuhamasika na kudai haki za kiuchumi na za kibinadamu Fatuma Kassim, ambaye ni mjumbe wa kamati ya haki za wanawake kijijini Pachoto, anasema jukumu mojawapo analofanya ni kusaka taarifa za unyanyasaji kijijini hapo.

"Tukizipata tutandika barua kupeleka taarifa kwa mtendaji wa kijiji, kata , mahakamani na kwenye ngazi za dini-Bakwata," anaongeza Gatamo.

Anasema wanafuatilia na kutafuta wanawake wanapotelekezwa, kupewa talaka holela, wazazi kukataa kusomesha watoto, ndoa za utotoni na kufuatilia haki za kielimu kwa wasichana na wanawake kudhulumiwa kwenye familia na ndani ya ndoa

### MAFANIKIO KIUCHUMI

Wanawake hawa wanasema kufahamu haki zao kumeleta mwamko wa kumiliki mali na kufanyabiashara.

"Licha ya kuwa na changamoto kama kunyooshewa vidole kuwa wanawake hawa wanaingilia masuala ya watu, kutishiwa amani na kukosa ushirikiano hasa kutoka kwa wanaofanya unyanyasaji, kwa ujumla kujua haki zetu kumetuwezesha kutoka ndani na kuanza kufanyakazi zinazobadilisha maisha yetu" anasema Gatamo.

# EDITHA & NASRA

## Wanasayansi wagunduzi mmea tiba na kichocheo nyuki kuongeza asali



Washindi wa jumla, Nasra Mpochi na Editha Philipo walioshika ngao wakiwa wanakabidhiwa tunzo na Waziri wa Elimu, Profesa Joyce Ndalichako, wanaoshangilia ni wanafunzi wenzao na wafanyakazi wa YST. **PICHA: ELIZABETH ZAYA.**

**Na Elizabeth Zaya**

MAONYESHO ya wanasayansi chipukizi mwaka huu, yamewaibua wasichana na kuthibitisha kuwa mabinti wanaweza. Ni baada ya kazi zao kuibuka kidedea na kuwashawishi majaji kuwa walichofanya kinaweza kubadili maisha ya Mtanzania, kiuchumi, kiafya na kijamii.

Yakiandaliwa na taasisi ya Young Scientists Tanzania(YST) kuanzia Julai 31 hadi Agosti mosi mwaka huu, jijini Dar es Salaam, maonyesho hayo yanashirikisha wanafunzi 190 wa shule za sekondari na kazi za kibunifu 95.

Kazi za Shule ya Sekondari ya Chief Dodo ndizo zilithibitisha ubora wa wanafunzi wa kike walioibuka washindi na kuibua mawazo mapya ya kimaendeleo yaliyogusa sekta muhimu za afya na uchumi.

### MABINTI WALIONG'ARA

Washindi katika maonyesho hayo walipatikana baada ya kazi zao kuchujwa na majaji lakini pia kushuhudiwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, aliyekuwa mgeni rasmi.

Akiwahamasisha wanasayansi hao anasema, serikali itaendelea kushirikiana na YST kuendeleza vipaji vya wanasayansi hao chipukizi na kuwatafutia fursa katika Jumuia ya Maendeleo, Kusini mwa Afrika(SADC).

Washindi wa jumla ni kutoka Sekondari ya Chief Dodo iliyoko Manyara, ambao pamoja na mambo mengine walimfurahisha Profesa Ndalichako kuona mwamko walionao wasichana hao kupambana na wenzao wa kiume katika masomo ya sayansi.

Vinara hao ni Editha Philipo wa kidato cha tatu na Nasra Mpochi wa kidato cha nne,waliokabidhiwa kitita cha Shilingi milioni 1.3 (wote wagawane), ufadhili wa masomo ya chuo kikuu, medali pamoja na safari ya kwenda kuiwakilisha Tanzania katika maonyesho ya wanasayansi chipukizi Afrika Kusini mwaka huu.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, Nasra Mpochi anasema wazo lililowapa ushindi lilihusu namna mti wa kivumbasi ulivyo suluhisho kwa wafugaji wa asali.

Anaeleza kuwa walilipata wazo kwenye bustani ya shule yenye mti huo ambako mara kwa mara walijaa nyuki waliogeuka kuwa kero shuleni.

"Nyuki walikuwa wanatusumbua sana, walikuwa wanazunguka mmea huo na kutuletea usumbufu hata kushindwa kusoma vizuri kwa kuogopa kung`atwa, ikabidi tufanye uchunguzi kufahamu kitu kilichopo katika mti huo wa kivumbasi ambacho kinawavutia nyuki,"anasema Nasra.

"Ilibidi pia twende kwa wafugaji wa nyuki walio katika sehemu tofauti na tulichukua mti wa kivumbasi na kuupaka katika sehemu za juu za mizinga ya nyuki, halafu tukakaa mbali kidogo kuangalia, tukaona nyuki wanajaa katika sehemu ya mzinga tulilopaka mti huo," anasema Nasra.

Anaongeza kuwa na katika mizinga yote waliyoweka huo mti wa kivumbasi ndani ya mwezi mmoja walivuna asali nyingi tofauti na ilivyokuwa imezoeleka walifikia asilimia 50 na mizinga midogo ilipatikana asali yenye kilo sita.

Anasema pia walibaini kwamba unasaidia kutibu, ni dawa ya tumbo linalojaa gesi na inapochomwa hufukuza wadudu hatarishi kama mbu.

### MUDA WA UTAFITI

Mwanafunzi huyu anasema walitumia miezi minne kufanya utafiti na kugundua kuwa pia unatumika kuoshea vya kuhifadhi maziwa na pia ni kiungo cha chai kinachoipa harufu nzuri.

Anasema wamepanda mti huo na sasa wanauza dawa na kiungo cha chai :" tunafunga majani matano kila fungu na tunauza kwa Sh.100, pia shule imetuwezesha kwenda kutembelea vijiji vingine kuwafundisha kupanda na kutumia dawa hii", anasema Nasra.

"Tunawashukuru sana YST kwa kututambulisha kitaifa na kimataifa, tunaamini kwamba kazi yetu hii itafika mbali, sisi tuliweza kuwafikia wananchi katika eneo dogo, lakini kwa sasa tutafikia idadi kubwa zaidi,"anaongeza Nasra.

Mshindi mwenza Editha ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha nne anasema kushinda kwao katika tuzo hizo kumewaongezea nguvu ya kujipanga kufanya vizuri zaidi masomo ya sayansi.

"Tunawaasa na wasichana wengine wasikate tamaa, wapende masomo ya sayansi kwa sababu wakidhamiria wanaweza kufanya vizuri zaidi,"anasema Editha.

Anaongeza : "Tunashukuru kazi yetu imewasaidia watu kwa namna mbalimbali. Ukichukua mbegu za kivumbasi, ukaanzisha bustani unaweza kuweka mizinga na kupata asali, hivyo tunaona kwamba pia ni fursa nzuri ambayo inaweza kuwapatia pia vijana ajira ya kujiajiri wenyewe."

### MAONI YA MWALIMU

Mwalimu wa wanafunzi hao Jackson Warae, anasema baada ya kufanya utafiti wa mti kivumbasi walizungumza na wafugaji wa nyuki kuhusu changamoto ya uvunaji wa nyuki.

"Tulifanya utafiti na kuwahoji wafugaji wa nyuki ambao walisema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni nyuki kushindwa kuingia kwenye mizinga, mpaka wasubiri msimu wa maua, kwa hiyo nikakaa na wanafunzi, tukafanya utafiti na tukatumia mti wa kivumbasi, kupaka kwenye mizinga na tukatengeneza juisi ya maua ya mti huo".

Anasema waliiweka kwenye mizinga na ikawavutia nyuki waliokuwa wanaingia kwa wingi na asali ilipatikana nyingi zaidi, anasema Warae.

Anasema kupitia kazi hiyo waliyobuni, imeanza kusaidia jamii inayoizunguka shule hiyo na maeneo ya karibu na kuiomba serikali kuwatunza vijana hao wanaojifunza ubunifu na utafiti katika umri mdogo.

### MASHINDANO

Ni mara ya tisa YST kuandaa maonyesho hayo na yamekuwa yakifanyika kila mwaka na kushirikisha shule za sekondari kuonyesha kazi za kisayansi na teknolojia za kibunifu zilizotafitiwa na wanafunzi wa shule hizo chini ya usimamizi wa walimu.

Katika maonyesho hayo kwa miaka tisa mfululizo, wanafunzi ambao wamekuwa wakishiriki wamekuwa wakipata fursa ya kuboresha ujuzi wa kisayansi kupitia mpango wa uwezeshaji unaoendeshwa na YST na kuratibiwa na waratibu wa mikoa mbalimbali wa taasisi hiyo.

Wadau waanzilishi wa YST Dk.Gozbert Kamugisha, ambaye anaungwa mkono na Karimjee Jivanjee Foundation , Shell Exploration na Uingereza kutoa ufadhili, anasema walichukua hatua hiyo baada ya kuona tija ya maonyesho hayo kwa nchi, hususani katika kutengeneza wabunifu na wanasayansi wengi na kuwahamasisha wanafunzi kupendelea masomo hayo.

### KAZI ZILIZOONEKANA

Maonyesho ya mwaka huu wanafunzi walionyesha kazi za kibunifu katika Nyanja za kemia, fizikia na hisabati , biolojia na mazingira, sayansi ya jamii na teknolojia, anasema.

Zote zilijikita katika kutafuta utatuzi wa matatizo katika afya, kilimo na usalama wa chakula, mawasiliano na usafirishaji, nishati na mazingira, elimu, mahusiano ya kijamii na matatizo ya kijamii.

Dokta Kamugisha anasema kuna haja ya kufanya mabadiliko ya masomo ya sayansi yawe ya vitendo ili miradi inayobuniwa iwe na faida kwa jamii na isaidie kuamsha ari ya wanafunzi kusoma masomo hayo zaidi.

HABARI KIMATAIFA

# Wasiojulikana wamteka mkosoaji

**HARARE,** Zimbabwe

**EU iliondoa sehemu kubwa ya vikwazo vya kiuchumi kwa nchi ya Zimbabwe mwaka 2014.**

MKOSOAJI wa Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa (pichani), ametekwa nyara na watu wasiojulikana ambao baadaye walimwachilia baada ya kumtesa.

Mateka huyo ni mchekeshaji wa mitandaoni nchini Zimbabwe, Samantha Kureya, maarufu kwa jina la 'Gonyeti' alitekwa na watu wasiojuliakana akiwa nyumbani kwake jijini Harare.

Ripoti zilisema kuwa baada ya kutekwa alipigwa na kujeruhiwa vibaya. Kureya ambaye pia ni mwanahabari alielezea namna wanaume watatu waliokuwa wamefunika nyuso zao walivyoyamia nyumba yake na kumchukua kwenda kumtesa.

Mwanahabari huyo amekuwa mkosoaji wa serikali ya Emmerson Mnangwanga na jeshi la polisi kupitia vichekesho vyake..

Tukio hilo linatokea miezi miwili baada ya Zimbabwe na Umoja wa Ulaya (EU) kufanya mazungumzo rasmi ya kisiasa baada ya miaka takribani 17 ya sintofahamu iliyozuka wakati wa uongozi wa rais wa zamani Robert Mugabe.

Mabalozi kutoka nchi za Umoja wa Ulaya walioko Zimbabwe walikutana na wawakilishi wa serikali katika awamu ya kwanza ya mfululizo wa mazungumzo yaliyopangwa kufanyika baina ya pande hizo mbili kujaribu kumaliza miongo kadhaa ya vikwazo vya kiuchumi kwa Zimbabwe.

EU iliondoa sehemu kubwa ya vikwazo vya kiuchumi kwa nchi ya Zimbabwe mwaka 2014 lakini imekuwa haitoi msaada wa kifedha kwa serikali hiyo. **RFI**



Moto ukiteketeza Amazon wiki hii: **PICHA MTANDAO.**

## Yataka mazungumzo Kiir, Machar

**JUBA,** Sudan Kusini

JUMUIYA ya Maendeleo ya Nchi za Afrika Mashirika (IGAD), imetaka kufanyika kwa mazungumzo ya ana kwa ana baina ya Salva Kiir na Riek Machar.

Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Afrika Mashariki (IGAD), imemuomba Rais wa Sudan Kusini, Salva Kiir kuanza kugawa kiasi cha dola za Marekani milioni 100 kilichoahidiwa kama sehemu ya kuratibu utekelezwaji wa mkataba wa amani.

Jumuiya ya IGAD ambayo ilifanikisha kupatikana kwa makubaliano ya amani, imeuomba utawala wa Juba kuwa wazi na kuweka mchakato maalumu wa uwajibikaji katika matumizi ya fedha za kuratibu utekelezwaji wa mkataba wa amani.

IGAD pia iliwataka Rais Salva Kiir na hasimu wake Dk Riek Machar, kupanga kuwa na mazungumzo ya ana kwa ana ili kupata suluhu ya masuala tata yaliyosalia ili kuanza utekelezaji wa mkataba wenyewe.

Awali serikali ilikuwa imeahidi kuanza kutoa fedha inayohitajika kutekeleza mkataba huo, lakini mpaka sasa haijafanya hivyo.

Tume maalumu inayosimamia utekelezwaji wa mkataba wa amani nchini Sudan Kusini imeripoti kuwa kati ya mwezi April na Julai ni dola za Marekani milioni 6.5 pekee ndizo zilitolewa kwa ajili ya usalama.

Julai mwaka huu, viongozi kutoka Sudan Kusini na Uganda walifanya mkutano wa pamoja kwenye mji wa Magwi ulioko Sudan Kusini, uliolenga kujadili vitisho vya kiusalama na changamoto baina ya nchi hizo mbili. **BBC**

## Rais akataa ushauri wa nje

**BRASILIA,** Brazil

MSITU wa Amazon huko Brazil ulio na umuhimu mkubwa na ukielezewa kuwa ni 'mapafu ya dunia' umeungua takribani mara 73,000 tangu Januari hadi Agosti mwaka huu

Hata hivyo, Rais wa Brazil Jair Bolsonaro amepingana na ushauri unaotolewa na mataifa mbalimbali kufuatia hofu ya msururu wa matukio ya moto Amazon.

Kitisho hicho kinatokana na msitu huo unaotajwa kama "mapafu ya dunia", kuharibiwa na mfululizo wa matukio ya yanayoibua mjadala wa nani wa kulaumiwa.

Rais Jair Bolsonaro ameandika kwenye ukurasa wa twitter kwamba serikali yake imefungua milango ya majadiliano, lakini kwa kuzingatia data halisi na pande zote kuheshimiana.

Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron aliuita moto huo "janga la kimataifa", huku akitoa mwito kwa wakuu wa mataifa yaliyoinukia kiviwanda duniani, G-7 kufanya kikao cha dharura kujadili janga hilo katika mkutano wao wa kilele unaofanyika Ufaransa.

Aliandika, "nyumba yetu inaungua. Kwa kweli, msitu wa Amazon, mapafu yanayozalisha asilimia 20 ya hewa ya Oksijen duniani unateketea."

Bolsonaro alijibu kwa kuandika "Ninajuta kwamba Macron anataka kujiimarisha kisiasa kwa kutumia suala hili la Brazil na mataifa mengine ya Amazonia. Mawazo yake ni ya kikoloni kwa kuyataka mataifa ya G-7 kujadili suala hilo bila ya kushirikisha nchi nyingine za ukanda huo".

Bolsonaro anatoa matamshi hayo wakati Brazil ikiwa mwenyeji wa mkutano wa kikanda wa Umoja wa Mataifa kuhusu mazingira utakaofanyika mjini Salvador, kuelekea mkutano wa kilele nchini Chile, mwezi Desemba.

Jamii ya watu wanaoishi kwenye msitu huo wameeleza kusikitishwa kwao na namna msitu huo unavyoteketezwa.

Handech Wakana Mura ni kiongozi wa jamii hiyo, "Tunasikitika kwa sababu msitu huu unateketea kila wakati, tunahisi hali ya hewa inabadilika na dunia inauhitaji huu msitu. Watoto wetu na sisi tunauhitaji pia."

Wataalamu wa mazingira wanasema uharibifu kwenye msitu huo uliongezeka kwa mara tatu ilipofika mwezi Julai taasisi ya kitaifa ya utafiti wa masuala ya angani, INPE ilisema.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres ameeleza wasiwasi wake mkubwa kutokana na moto kwenye msitu huo. Aliandika kwenye twitter, "katika wakati ambapo kuna mzozo mkubwa wa hali ya hewa, hatuwezi kubeba mzigo mwingine wa uharibifu wa chanzo kikuu cha oksijeni na bayoanuwai. Ni lazima Amazon ilindwe".

Mapema, mkuu wa utumishi wa rais Bolsonaro, Onyx Lorenzoni, aliyatuhumu mataifa ya Ulaya kwa kuongezea chumvi changamoto za kimazingira nchini Brazil ili kuvuruga maslahi yake ya kibiashara. **DW**

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# JUMBA JEKUNDU- 15

Mtunzi anapatikana (0716 350534)

**Na Adam Fungamwango**




"Haya ni makaburi." Alinyamaza kwanza na kuangalia Kadili kana kwamba alitaka kuyasoma mawazo yake, mara baada ya kupokea taarifa hiyo.

Miguu ilianza kumtetemeka.

"Sasa mimi hapa nataka unijibu maswali yangu machache tu nitakayokuuliza. Ukinijibu kiufasaha na ukweli, nitakuachia na hapa utaondoka kwenda kuungana na familia yako. Lakini kama ukinijibu utumbo, utapata mkong'oto ambao hujawahi kuushuhudia maishani mwako. Pia humu hutoondoka. Utauawa na kuzikwa humu humu ndani."

Akayakumbuka maongezi hayo aliyoyafanya masaa kadhaa yaliyopita na yule jamaa baunsa. Ndipo alipojua kuwa akifanya masihara huenda akauawa na kuzikwa ndani ya jumba hilo jekundu.

Sasa alitambua kuwa lengo la kuletwa pale ni kuonyeshwa makaburi ya watu wengine waliowahi kuingizwa kwenye jumba hilo.

"Makaburi haya wamezikwa watu ambao jeuri. Waliokuwa wanajifanya wajanja na hawataki kujibu ukweli maswali waliyoulizwa.

Sasa na wewe kama unataka uzikwe humu, jifanye mjanja. Inabidi ujibu maswali yote kwa ufasaha na ukweli." Alisema huku mkono ukimshika tena Kadili baada ya kuachia kwa sekunde kadhaa.

"Tena hawa wote wanazikwa wakiwa hai. Wanafia humo humo kaburini. Mimi nilitaka kukuonyesha tu, kwa hiyo yule jamaa akija tena kukuuliza maswali yake, usimdanganye, mjibu sahihi, umesikia?"

Kadili hakujibu kitu. Hakujua sasa ni jibu gani ambalo walitaka kutoka kwake. Ana uhakika kuwa alijibu maswali yote kwa ufasaha, na hakuongopa hata chembe.

Aseme ni kweli ana mahusiano na Edina wakati si kweli? Na kama akijibu hivyo ndiyo itakuwa salama yake kutoka ndani ya jumba jekundu akiwa hai? Aliwaza.

Akaona kuwa hata akisema ni kweli ana uhusiano na Edina ndiyo atakuwa amejichongea kabisa, hivyo akaona heri nusu shari kuliko shari kamili.

"Kama wamedhamiria kuniua, nikisema kweli au si kweli wataniua tu. Ni bora nisimame kwenye msimamo wangu kwa sababu chochote kile nitakachokisema hakitoaminika." Aliwaza.

Wakati huo mkono wa jamaa yule ulikuwa kwenye mkono wa Kadili. Alimvuta na kumrejesha kwenye selo yake. Akakaa chini kusubiri hatma yake.Ghafla aliingia yule baunsa wa mwanzo. Kama kawaida mkononi alikuwa ameshikilia mkanda wa suruali ambao tayari ulikuwa umeshamuonja Kadili hapo mwanzo.

**Tena hawa wote wanazikwa wakiwa hai. Wanafia humo humo kaburini. Mimi nilitaka kukuonyesha tu, kwa hiyo yule jamaa akija tena kukuuliza maswali yake, usimdanganye, mjibu sahihi, umesikia?**

"Nadhani umeona ulichoenda kuonyeshwa." Alivunja ukimya. Kadili hakujibu chochote, bali alimuangalia kihuruma huku akiwa amejikunja.

"Nakuuliza kwa mara nyingine, Edina una uhusiano naye gani?" Alihoji kwa msisitizo na sauti ya kutisha.

"Bwana mkubwa, mimi nilishaeleza tangu awali, mimi ninatoka kwenye familia masikini sana, siwezi kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Edina. Alikuwa patna wangu wakati wa kucheza muziki tu..." Kabla hajamalizia, alistukia amepigwa na kitu mabegani. Maumivu makali kana kwamba anaunguzwa na moto yalimpata. Alilia kwa uchungu mkubwa. Aligaragara kwa maumivu licha ya kwamba chini ya sakafu kulikuwa na maji. Ndipo alipogundua kuwa alikuwa amepigwa na mkanda wa suruali.

Alikuwa ni kama ameshachoka na mateso. Alidhohofu pia kwa njaa, kwani tangu afike hapo, si tu kwamba alikuwa hajala chakula, bali hata maji hakuwahi kutia hata tone kinywani.

"Hutaki kujibu swali langu siyo? Unanidanganya ee."

Kadili alimuangalia baunsa yule kwa jicho la huruma na kukata tamaa, Akajikuta akitamka.

"Mimi nilichoongea ni kweli na kama hautaki au haukikubali hicho, basi niue tu, mimi niko radhi. Bora kufa kuliko kuteseka hapa na mateso haya, baridi pamoja na njaa kwa kitu ambacho sijafanya."

Maneno yale alionekana kumuingia vilivyo baunsa. Pamoja na ukatili wake, alimuangalia Kadili kwa jicho kali, lakini kwa mbali likichanganyika na la huruma.

Alisogea nyuma hatua mbili, akageuka na kuufuata mlango. Aliufungua akatoka na kuufunga kwa nguvu.

Alijua sasa amekwisha. Kama akirudi kwa mara ya tatu kinachofuata ni kuuawa kama si kwenda kuzikwa hai kwenye makaburi yaliyo katikati ya bustani ya jumba lile jekundu.

Alimuwaza mama yake yuko katika hali gani saa hizi. Alimkumbuka rafiki yake Meze na dada zake. Aona kabisa kuwa atauawa bila maiti yake kupatikana. Kama ingekuwa uwezo wake angewaomba watesi wake wakimuua, basi wafanye uungwana maiti wakaitupe karibu na nyumbani kwao usiku wa manane ili uzikwe na familia yake.

*****************************************

"Unajua wewe mbishi sana." Ilikuwa ni kauli ya kwanza aliyoisikia kwa mtu mwingine aliyeingia kwenye selo hiyo kwa ajili ya kumtoa ndani, lakini haijulikani anapopelekwa.

Hakuwa yule baunsa aliyekuwa akimuuliza maswali na kupiga kwa mkanda wa suruali. Na wala si yule jamaa kibonge aliyemtembeza kwenye bustani na makaburi ndani ya jumba lile.

Kwanza huyu alikuwa kijana zaidi kuliko wenzake. Lakini hakuwa na mwili mkubwa. Kadili alifuatana na kijana yule mpaka kwenye chumba kimoja ambacho ni kama stoo vile. Hata hivyo kulikuwa na viti viwili vya chuma.

"Kaa hapa, nakuja." Ilikuwa ni kauli ya kijana yule aliyeonekana pia ni mpole na hakumchukulia Kadili kama mhalifu.

Dakika tano zilipita, aliingia msichana mmoja mwembamba mrefu aliyebeba sinia lililokuwa na chakula. Hakikuwa kingi sana, lakini kilinukia kiasi cha kumfanya mate kumvuja Kadili, ukichukulia kuwa alikuwa na njaa kwa muda mrefu.

Chakula kiliwekwa kwenye kiti kingine. Hakuongea kitu chochote zaidi ya macho yake kumtazama sana Kadili na yalikuwa yakiongea kuwa 'hiki ni chakula chako'. Ulikuwa ni wali na nyama iliyopikwa vizuri. Pembeni kulikuwa na mboga za majani, matunda, maziwa na maji ya kunywa.

Kadili alianza kula kwa pupa kutokana na njaa aliyokuwa nayo bila hata kumuangalia msichana yule aliyekuwa akiondoka huku akimtazama Kadili kwa makini na mshangao.

Ndipo alipogundua kuwa hakuwa amekula tangu jana yake mchana. Muda huo ilikuwa ni jioni majira ya saa 10 hivi kwa jinsi alivyoliona jua alipotolewa selo na kijana yule.

Kitu pekee alichokumbuka ni kwamba wakati anachukuliwa nyumbani alikuwa anakula ugali na hata hivyo aliondoka akiwa bado hajamaliza.

**Itaendelelea Jumamosi**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**

Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA Tutumie

E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL FOR ARUSHA**
**AT ...........................ARUSHA**
**APPEAL/APPLICATION NO 357 OF 2019**
**(FROM ORIGINAL APPLICATION NO... .......WARD TRIBUNAL ).**

**MBOYO LOULU ............APPLICANT/APPELLANT**
**VERSUS**
**PROSPER LEIYA.......... ............RESPONDENT**

**SUMMONS/NOTICE**

TO: PROSPER LEIYA
WHERE EVER YOU ARE.

Take notice that the above matter is coming for mention/hearing on 17 day of Sept 2019 before the Hon.F.MDACHI Chairman of the tribunal.

You are hereby commanded to appear at 11. When the case will be mentioned/heard.

GIVEN under my hand and the Seal of this Tribunal this 21 day of August 2019

215386902

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 67 OF 2019
In the matter of the Estate of the late ESTER MILANG'TONE MPANDAH
AND
In the matter of the application for letters of Administration by ABIGAILI G. MWENDA

**GENERAL CITATION**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the 5th Day of September, 2019.

The will of the said deceased is deposited and open for inspection of the court.
Date 22nd day of August 2019

215386802

## KUPOTEA KWA CHETI




**Zulfa Ramadhani Omary** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1181/0067** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Senge.

**Yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: SIN/SIN/RB/218509/2019**

115386302

## KUPOTEA KWA CHETI



**Fortunatus Killian Haule** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1880-0187** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika Shule ya Sekondari Mbezi Inn.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kitu chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: DAR/GOG/RB/221663/2019**

115386902

## KUPOTEA KWA CHETI



**Vumilia R. William** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index **namba S0585/013** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka1993 katika Shule ya Sekondari Munanila.

**Yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: NZ/RB/4406/2019**

115386002

## KUPOTEA KWA KADI

**Aaron Loth Makulu**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T925 AHJ aina ya NISSAN HARDBORD P/K, yenye chasis namba B041912.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa;
**DAR/KIJ/RB/237080/2019**

115387002

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**THOMPSON P MBOYA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya RANGE ROVER T 907 AWG yenye Chassis namba SALLPAMM3TA333942 na Injini namba, 42D 42D10567A

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Polisi Taafifa :
**MS/TR//RB/1500/2019**

## TAARIFA KWA UMMA



**Uongozi wa Chuo cha Kilimanjaro Institute of Technology and Management (KITM)** unapenda kuufahamisha umma kwamba mwenye picha hapo juu **Robert Msele ambaye** alikuwa ameajiriwa katika idara ya masoko siyo mfanyakazi wa chuo hiki tena kuanzia 17 Agosti 2019.

Umma unatahadharishwa kutoshirikiana naye katika jambo lolote linalohusiana na Chuo cha (KITM) kwani hakitawajibika na shughuli yoyote itakayomuhusisha mtajwa hapo juu.

**Regency Park Hotel,**
**Dar es Salaam Tanzania.**

## TANGAZO LA ZABUNI

Tunahitaji mzabuni wa kuleta vitu vifuatavyo kwa mkataba, 2019/20.

1. Kuku
2. Samaki
3. Nyama
4. Vitu vya madukani/dry goods
5. Mbogamboga na matunda.

**Tuma maombi yako yakiambatanishwa na bei kwa bidhaa husika**
**gm@regencyparkhotel.co.tz**
**Simu: +255 715 534821**


CLASSFIED ADVERTISEMENT

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la
Nipashe kila siku

NJOO UTAN-GAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# MARTIAL AFURAHIA UPATINA NA RASHFORD

**MANCHESTER,** England

BAADA ya kuanza vizuri pamoja msimu huu, Anthony Martial ameiambia Sky Sports namna uhusiano wake na Marcus Rashford unavyowasukuma washambuliaji hao kuendelea kuimarisha viwango vyao.

Wachezaji wote wameingia msimu huu wa 2019/20 wakiwa na pointi ya kujiimarisha na wamepewa nafasi ya kufanya hivyo, huku Romelu Lukaku akiwa amewaachia nafasi baada ya kuondoka.

Wachezaji hao wawili kwa pamoja wamefunga mabao manne kwenye mwanzo wa Ligi Kuu ya England msimu huu.

"Kwenye mazoezi, tuna mashindano kati yetu ya kufunga mabao," alisema Martial akiiambia Sky Sports.

"Tunapimana nani anaweza kumaliza kuwa mfungaji bora. "Nani anashinda? Ndio, hilo linategemea... muda wingine ni yeye, muda mwingine mimi. Kwenye mechi, Marcus anapenda kucheza katikati, kama mimi. Wote tunakuwa na jukumu moja uwanjani.

"Hii ni nafasi yetu kuonyesha ubora wetu katika klabu hii kubwa kabisa duniani, na naamini kwamba ushirikiano wetu uwanjani utakuwa msaada mkubwa zaidi kwa timu msimu huu."

# *Mustafi, Elneny mkiondoka itapendeza sana - Arsenal*

**LONDON,** England

UNAI Emery amesema kwamba ni bora Shkodran Mustafi na Mohamed Elneny wakaondoka Arsenal kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili, kwa ajili ya kuimarisha vipaji vyao.

Kati yao hakuna aliyekuwa sehemu ya kikosi hicho msimu huu na sasa kocha wa Arsenal, Emery amedokeza kwamba, tayari amewaambia wawili hao ni kama hitaji la ziada kikosini hapo.

"Tuna wachezaji aina kama yao na wao wanajua hali halisi. Kwa mfano, Elneny na Mustafi, wanajua hali yao kwenye kikosi," alisema Emery kuelekea kwenye mchezo wao dhidi ya Liverpool leo Jumamosi, wakati akizungumza na Sky Sports.

"Nataka wachezaji wawe na furaha hapa, nataka wachezaji wawe mashujaa hapa, na mwaka jana kwa mfano Mustafi na Mo, walipokuwa hawachezeshwi hawakuwa na furaha.

"Nimezungumza nao mara kadhaa mwaka jana kuhusu hali hii na nafikiri walichukua mazungumzo yangu kuwa chanya na nawashauri waondoke, waweza kupata furaha sehemu nyingine.

"Ni wachezaji wakubwa, lakini hapa nafasi yao kutokana na hali halisi ni ndogo, hawataweza kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara.

"Nimezungumza nao na kuwaambia hali ilivyo na wenyewe wanajua, wanatakiwa kwenda kucheza katika timu nyingine ili kuthibitisha ubora wa vipaji vyao, kwani nafasi yao hapa ni ndogo."







## Oxlade-Chamberlain asaini mkataba mpya Liverpool

**LIVERPOOL,** England

ALEX Oxlade-Chamberlain amesaini mkataba mpya wa kuendelea kucheza hapo Liverpool utakao muweka hadi mwaka 2023.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye alijiunga na Klabu hiyo kwa pauni milioni 35 kutoka Arsenal Agosti 2017, alisaini mkataba huo hapo Melwood Alhamisi. Kiungo huyo miezi yake 24 aliyokaa hapo Anfield imekuwa haina mafanikio kwa kiasi fulani.

Alikuwa nguzo muhimu mwanzoni mwa msimu, hasa katika mechi za Ligi na ushindi wa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City kabla ya kuumia mguu dhidi ya Roma Aprili 2018.

Oxlade-Chamberlain alihusika katika mechi nne tu katika kikosi hicho msimu wa mwaka 2018-19 baada ya kupona.

Na ameanza katika mechi mbili za Ligi Kuu msimu huu na kuonekana kama mmoja wa wachezaji muhimu kwa kocha, Jurgen Klopp.

"Ni kitu ninachokiona kama nafasi nzuri kwangu, natumaini nitakuwa na kiwango bora zaidi hapa," alisema Oxlade-Chamberlain akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

## HABARI MICHEZO

# Aubameyang: Fowadi Arsenal sawa na Liver

**LONDON,** England

PIERRE-Emerick Aubameyang anaamini Arsenal wana zana za kuweza kulingana na washambuliaji watatu ambao waliiwezesha Liverpool kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Timu pekee zilizoshinda mechi zake zote mbili za mwanzo za Ligi Kuu ya England msimu huu, Liverpool na Arsenal zinakutana leo Jumamosi kwenye mchezo utakaopigwa pale kwenye dimba la Anfield.

Arsenal walichapwa mabao 5-1 katika mchezo wao wa mwisho nyumbani kwa Liverpool, lakini wameanza msimu huu vizuri na wanaweza kucheza kwa pamoja, Aubameyang, Alexandre Lacazette na Nicolas Pepe kwenye safu yao ya ushambuliaji.

Inaweza kutengeneza safu hatari zaidi ya ushambuliaji dhidi ya ile ya Liverpool inayoongozwa na Mohamed Salah, Sadio Mane na Roberto Firmino.

"Kama tulivyoona msimu uliopita, Liverpool inacheza na washambuliaji watatu mbele na wanacheza vizuri mno," amesema Aubameyang akiiambia Sky Sports.

"Kwa nini sio sisi? Nafikiri tunaweza kufanya hivyo.

"Utakuwa mchezo mgumu dhidi ya Salah, Mane na Firmino.

"Ni wachezaji wakubwa. Mara zote wanajaribu kwenda mbele na kujaribu kufunga mabao na kusaidia. Ni moja kati washambuliaji bora duniani."

Aliongeza: "Naona mfano. Pepe na mimi, ni wachezaji wenye kasi kama ilivyo kwa Mane na Salah, huku Laca ni mchezaji anayeweza kukaa na mpira na kwa uhakika ni mzuri kama Firmino.

"Hivyo, tunaweza kusema, tunakaribia kuwa imara zaidi."





# PSG BADO YAIKAZIA BARCA KWA NEYMAR

**PARIS,** Ufaransa

BAADA ya Klabu ya Barcelona kukataliwa kwa ofa ya kumrudisha kwa mkopo, Neymar kutoka PSG, wakaamua kutoa ofa ya pauni milioni 137, lakini nazo zimekataliwa.

Mabingwa hao wa Ufaransa wanataka kulipwa pauni milioni 229 kwa ajili ya kumuachia mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil ili aweze kurudi Hispania.

Wakati Barcelona ikienda chini ya dau la pauni milioni 198 ililomuuza Neymar kwenda PSG mwaka 2017, PSG inataka kumuuza nyota huyo kwa faida zaidi na inatazamiwa Barcelona itarudi tena siku chache zijazo.

Neymar alishatibuana na uongozi wa PSG na kufikia kuomba kuondoka kwenye klabu hiyo. Huku Rais wa PSG akisema wamechoshwa na vituko vya staa huyo.

Barcelona ina nafasi ya wiki chache hadi kufikia Septemba 2, mwaka huu kuweza kumrudisha Neymar kwenye kikosi chake na inaaminika itarudi na dau jingine.

# Ribery kucheza hadi miaka 40

**ROME,** Italia

FRANCK Ribery ana matumaini ya kucheza hadi zaidi ya umri wa miaka 40 baada ya kujiunga na Fiorentina, lakini akasema hana nia ya kuwa mpizani wa Cristiano Ronaldo.

Miaka 12 ya Ribery kukaa pale Bayern Munich ilimalizika wakati mkataba wake ulipomalizika mwishoni mwa msimu wa 2018-19, ambapo alishinda taji la tisa la Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Winga huyo wa zamani wa Ufaransa, amesaini mkataba wa miaka miwili kucheza pale La Viola.

Na Ribery, ambaye anapanga kufuata nyayo za mkongwe wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Francesco Totti, anatarajia kuiongoza Fiorentina kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Tumekuwa na makubaliano ya muda mrefu, lakini nina furaha kubwa kuwa hapa Florence," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36.

"Nimeona hamasa kubwa na kujiamini, ndio maana nimeamua kuwa hapa. Kiuhalisia mke wangu amenisaidia kufanya chaguo hili, kwa sababu familia yangu ni muhimu mno.

"Nina ari kubwa, mara zote nataka kucheza. Nina mkataba wa miaka miwili na nataka kuwasaidia wachezaji vijana. Nataka kutoa kitu fulani kwa klabu, nataka kuwarudisha Fiorentina kwenye tatu bora katika msimamo.

"Nimekuja hapa kuisaidia timu, ambayo ni Fiorentina. Siko hapa kushindana na Ronaldo. Serie A ni mashindano makubwa na kuna wachezaji wengi wazuri."



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# PEP ATAANZA DHIDI YA LIVERPOOL- EMERY

Kiwango chake binafsi kimeendelea vizuri, leo anaweza kupata dakika nyingi zaidi, kitu muhimu...

**LONDON,** England

KOCHA Unai Emery ameweka wazi kuwa leo yupo tayari kumwanzisha mchezaji wake aliyesajiliwa kwa rekodi ya dau kubwa klabuni hapo, Nicolas Pepe wakati Arsenal itakapoivaa Liverpool kwenye mechi ya Ligi Kuu England.

**Mshambuliaji huyo wa Ivory Coast alitua Arsenal kwa dau la euro milioni 72 akitokea Lille siku za mwisho kabla ya dirisha la usajili kufungwa na alicheza wakati wakishinda dhidi ya Newcastle United na Burnley.**

Kocha wa Gunners, Emery amekuwa akikataa kumwanzisha winga huyo mwenye umri wa miaka 24, kutokana na kukosa mechi nyingi za maandalizi ya msimu mpya hapo Arsenal.

Lakini Emery amefunguka kushawishika na kuona anastahili kumpa majukumu Pepe dhidi ya Liverpool wakati huu timu hizo mbili pekee zenye rekodi ya asilimia 100 ya kushinda mechi zote za Ligi Kuu msimu huu, zikikutana kesho katika Uwanja wa Anfield.

"Kitu muhimu ni kama binadamu, ni kumsaidia yeye na familia yake kujisikia furaha hapa. Kwa sasa ana wiki tatu za kufanya kazi hapa na sisi," Emery alimzungumzia Pepe.

"Hajajiandaa kwa msimu mpya hapa, lakini maendeleo yake yanaonekana kuwa mazuri. Kwa mfano, katika mechi ya kwanza, alicheza dakika 15 pale Newcastle, kisha akacheza dakika 45 dhidi ya Burnley.

"Nadhani kiwango chake binafsi kimeendelea vizuri. Kwa Jumamosi (leo), labda anaweza kupata dakika nyingi zaidi.

"Nitakwenda kuamua kesho (leo), lakini kweli maendeleo yake yamekuwa mazuri na amekuwa mzuri kwa timu na kwake.

"Kitu muhimu zaidi ni kuzoea na kumsaidia ajisikie rahisi na furaha kuwa na sisi."

Emery, ambaye pia jana alitarajiwa kufanya maamuzi kuhusu kuwapo kwa Mesut Ozil (aliyekuwa mgonjwa) na Granit Xhaka (majeraha ya mguu), ameiongoza Arsenal kushinda mechi mbili za ufunguzi za ligi kwa mara ya kwanza katika kipindi cha muongo mmoja.

Lakini katika mechi ya mwisho Arsenal kwenda Anfield walichapwa mabao 5-1 na kikosi hicho cha Jurgen Klopp, na Emery amesema jaribio dhidi ya Wekundu hao ni fursa kwa kikosi chake kuonyesha ubora.

"Kila mechi ni changamoto kubwa na kila mechi ni kwa ajili yetu kujiandaa vizuri iwezekanavyo. Wazo ni kuendelea kutengeneza kwa namna yetu na staili," aliongeza.

## ZISIKUPITE

### SANCHEZ KUIGHARIMU UNITED

MANCHESTER United inakabiliwa na gharama ya pauni milioni 12 za kumlipa mshahara Alexis Sanchez, 30, msimu huu, hata kama nyota huyo wa kimataifa wa Chile atajiunga na Inter Milan kwa mkopo kabla ya dirisha la usajili Ulaya kufungwa. ***(ESPN)***

### INTER YAKWAMA KWA VIDAL

BARCELONA imekataa ofa kutoka Inter Milan ya kuipata saini ya kiungo wa kimataifa wa Chile, Arturo Vidal, 32, kwa mkopo. ***(Mundo Deportivo)***

### BAYERN KUMPIGA BEI BOATENG

BAYERN Munich imefungua milango ya kumuuza beki Jerome Boateng, kwa pauni milioni 22. ***(Mail via Marca)***

### LLORENTE AKARIBIA UNITED

MANCHESTER United inakaribia kukubali dili la kuinasa saini ya mshambuliaji wa zamani wa Tottenham na Hispania, Fernando Llorente, 34. ***(Gazzetta dello Sport - via Star)***

### CABALLERO ATAKIWA MADRID

KIPA wa Chelsea, Muargentina Willy Caballero, 37, anatakiwa na Real Madrid. ***(Marca - in Spanish)***

### SILVA APIMWA AFYA MONACO

KIUNGO wa Leicester City, Adrien Silva, jana alikwea pipa kuelekea Monaco kufanyiwa vipimo vya afya. Silva, atasajiliwa kwa mkopo msimu huu. ***(Daily Telegraph)***

### MADRID WAMFUATA NEYMAR

UJUMBE kutoka Real Madrid upo Ufaransa kufanya mazungumzo na Paris St-Germain kuhusu uwezekano wa kuinasa saini ya Neymar, 27. ***(Marca - in Spanish)***

### LANZINI ANOGEWA WEST HAM

MSHAMBULIAJI wa West Ham, Muagentina Manuel Lanzini, amesema anataka kuongeza mkataba wake wa kuendelea kubaki na 'Hammers' hao na kwa sasa wapo kwenye mazungumzo. Lanzini, 26, mkataba wake wa sasa unamalizika majira ya joto yajayo. ***(Sky Sports)***

### APEWA DAU LA LUKAKU

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, atakuwa tayari kutumia pauni milioni 75 katika dirisha la usajili Januari, ambazo zimepatikana kwa kumuuza mshambuliaji Mbelgiji Romelu Lukaku, 26, aliyejiunga na Inter Milan mapema mwezi huu. ***(Talksport)***

### BENTEKE, PALACE WATETA

MSHAMBULIAJI Mbelgiji Christian Benteke, 28, na kiungo Muingereza James Tomkins, 30, wapo katika mazungumzo ya kuongeza mkataba na Crystal Palace. ***(Guardian)***

### LILLE YAJIAMINI KWA SANCHES

LILLE inaamini itainasa saini ya kiungo Mreno Renato Sanches, 22, kutoka Bayern Munich. ***(L'Equipe)***

### CITY YAMKOMALIA ALMADA

MANCHESTER City inamfuatilia kwa karibu kiungo wa Velez Sarsfield, Muargentina Thiago Almada, 18, ambaye bado hajaongeza mkataba na klabu hiyo. ***(A Bola, via Manchester Evening News)***

HABARI MICHEZO

## Marefa Ligi Z'bar waanzia darasani

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

Zaidi ya waamuzi 65 wa wilaya saba za Unguja wanatarajia kushiriki mtihani wa utimamu wa mwili na masomo darasani na watakaofaulu ndio watakaochezesha mechi za Ligi Kuu visiwani Zanzibar, imeelezwa.

Mtihani huo ambao unatarajiwa kufanyika katika Uwanja wa Amaan visiwani hapa, utatanguliwa na upimaji wa afya zoezi ambalo litafanywa na daktari kutoka Jeshi la Kujenga Uchumi, JKU.

Katibu wa Kamati ya Waamuzi wa Soka Zanzibar (ZAFRA), Muhsini Ali Kamara, alisema mtihani huo utawashirikisha waamuzi wa Unguja pekee kwa kuwa kwa upande wa Pemba wao tayari wameshafanyiwa.

Alisema maandalizi kwa ajili ya mtihani huo yapo vizuri na waamuzi hao baada ya kumaliza mtihani huo wa utimamu wa mwili watashiriki mafunzo ya darasani yatakayofanyika kwa muda wa siku tatu.

Aidha, alisema mtihani wa utimamu wa mwili utaanza saa 1:00 asubuhi na waamuzi watakaofaulu ndio watakaochezesha Ligi Kuu Zanzibar na si vinginevyo.

Alisema ili mwamuzi aweze kufaulu na kuchezesha ligi, lazima awe amefikia viwango viwili ikiwamo kupasi mtihani wa utimamu wa mwili na masomo ya darasani.

## Tanzania U-15 yatolewa Cecafa

**Na Somoe Ng'itu,** ASMARA

TIMU ya Soka ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 15 (U-15), imeyaaga mashindano ya Afrika Mashariki na Kati baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa wenzao wa Rwanda katika mchezo wa Kundi B uliochezwa jana mchana kwenye Uwanja wa Asmara nchini Eritrea.

Kutokana na matokeo hayo, Rwanda imefikisha pointi tisa na ina mechi moja mkononi dhidi ya Uganda wakati Tanzania yenye pointi tatu itakamilisha mechi zake za hatua ya makundi kwa kuikabili Ethiopia hapo kesho.

Rwanda imeungana na Kenya na Burundi kutoka Kundi A kutinga hatua hiyo ya nusu fainali ambayo itaanza kuchezwa Jumatano mjini hapa huku timu sita, wakiwamo wenyeji wakirejea nyumbani.

Mabao ya Rwanda katika mchezo huo wa jana uliochezeshwa na refa, Lemma Niguissie kutoka Ethiopia yalifungwa na Kennedy Hoziyana dakika ya tano na la ushindi liliwekwa kimiani na Eric Iramiye dakika ya 33.

Rabin Sanga aliifungia Tanzania bao pekee katika mechi hiyo katika dakika ya nane kwa njia ya penalti baada ya Joseph Fundusho kufanyiwa faulo katika eneo la 18 na beki wa Rwanda.

Kocha wa Tanzania U-15, Maalim Saleh, alisema baada ya mchezo huo kuwa kikosi chake hakikuwa na bahati katika mechi hiyo kwa sababu walitengeneza nafasi nyingi, lakini walishindwa kuzitumia vema.

# NADO AREJEA, CHILUNDA AWAPANIA WAHABESHI

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Azam FC ikizidi kuimarika kuelekea mechi yao ya leo ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Fasil Kenema, kufuatia kurejea kwa mshambuliaji wao, Iddi Suleiman 'Nado', straika anayekuja juu kwa sasa wa timu hiyo, Shaaban Chilunda, amesema anachokitaka leo ni matokeo chanya tu na si vinginevyo.

Nado aliikosa mechi ya Ngao ya Jamii waliyokubali kulala kwa mabao 4-2 dhidi ya Simba Jumamosi iliyopita, lakini juzi Nipashe lilimshuhudia akiwa mazoezini na wenzake akijifua tayari kwa mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Chamazi leo saa 10:00 alasiri.

Kurejea kwa Nado kunaongeza matumaini kwa Azam FC kuweza kupata matokeo katika mechi hiyo ambayo wanatakiwa kushinda zaidi ya mabao 2-0 ili kuweza kusonga mbele kufuatia mechi iliyopita kukubali kipigo cha bao 1-0 ugenini, Ethiopia.

**Katika hatua nyingine, Chilunda amesema kazi yake kubwa leo yeye na wachezaji wenzake ni kushirikiana na kuhakikisha wanashinda.**

"Tunahitaji mashabiki kutuunga mkono, waje uwanjani kwa wingi kwani tuna kazi kubwa ya kufanya kuweza kupata matokeo," alisema straika huyo aliyefunga bao la kwanza wakati wakilala 4-2 dhidi ya Simba.

Tayari Azam imetangaza viingilio vya mechi hiyo kuwa vitakuwa Sh. 3,000 kwa majukwaa ya mzunguko wakati VIP A na B ni Sh. 10,000 na Sh. 5,000 tu.

Kwa kila atakayeingia uwanjani leo atakutana Ice Cream ya Ukwaju mlangoni na tiketi za mchezo huo zinapatikana kwenye vituo vya Magomeni Ice Cream Center, Azam Shop Kariakoo, Mbagala Rangi Tatu na kama zikibaki zitauzwa uwanjani leo.



Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Simai Mohammed Said, akiwasalimia wachezaji wa Yanga alipowatembelea mazoezini mjini Gaborone, Botswana juzi. Simai ambaye pia ni Mwakilishi wa jimbo la Tunguu, Zanzibar yupo Botswana kwa ziara ya kikazi wakati Yanga leo itamenyana na wenyeji, Township Rollers katika mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: MTANDAO**

## *TPBL yaanika mabadiliko Ligi Kuu*

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Ligi Kuu ikianza leo, Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPBL) imetangaza kubadili baadhi ya mfumo wa uendeshaji ambapo suala la wachezaji wa kigeni na mavazi ya makocha yameguswa.

Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Boniface Wambura akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam, alisema mabadiliko hayo yanaendana na mpango wa kuboresha ligi hiyo. Wambura alisema, kwa upande wa wachezaji wa kigeni hawatapewa leseni za kucheza mpaka pale watakapopatiwa vibali vya makazi na kazi, pia wachezaji wote wa kigeni watakaosajiliwa msimu ujao lazima wawe wanacheza timu za taifa au Ligi Kuu nchini mwao.

"Klabu zote za Ligi Kuu zinatakiwa zisajili wachezaji watatu wa kutoka U-20 na wapatiwe nafasi ya kucheza, aidha timu za Ligi Kuu zitapungua kutoka 20 za sasa hadi 16 katika misimu miwili ijayo, tunaanza kupunguza timu mbili msimu ujao kisha mbili nyingine katika msimu unayofuata, lakini michezo ya mchujo ('Play Off') itakuwapo kama kawaida, pia tunahitaji Ligi Daraja la Kwanza na la pili ichezwe kwa ligi moja na si ya makundi kama ilivyo sasa," Wambura alisema.


Alisema katika mabadiliko hayo, timu mwenyeji ndiyo itakayotakiwa kuandaa gari la wagonjwa katika mchezo husika pamoja na waokota mipira na iwapo timu mwenyeji haitafanya hivyo itapokonywa pointi na makatibu wake kupewa adhabu.

"Tumefanya hivi kwa kuwa timu mwenyeji huchukua asilimia 60 ya mapato, vilevile kamishna wa mechi anatakiwa ajue mapema vazi la benchi la ufundi katika mkutano kabla ya mechi (pre-match meeting)na kama kocha atavaa tofauti ijulikane mapema na avae vizuri na akivaa tofauti kamishna ataruhusiwa kumuondoa.

# Michezo

Jumamosi Agosti 24, 2019

Nipashe

PSG bado yaikazia Barca kwa Neymar UKURASA 29



Kikosi cha Yanga. **PICHA: MAKTABA**

## Sababu KMC FC kutupwa nje Caf

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya KMC inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni, imesukumizwa nje ya michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika kwa kuchapwa mabao 2-1 na AS Kigali ya Rwanda, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana.

KMC, ambayo kwenye mechi ya kwanza iliyochezwa Kigali nchini Rwanda, ililazimisha sare ya bila kufungana, lakini ikashindwa kufanya hivyo nyumbani mbele ya mashabiki wake.

Inaonekana wazi KMC iliathiriwa zaidi na muda wa kuanza mechi kwani ilichezwa saa tisa mchana na kusababisha wachezaji wake kuchoka mapema kwa kuishiwa pumzi.

Kama vile haitoshi, timu hiyo ilionekana haina wachezaji wenye viwango vikubwa, hasa wa kigeni ambao mara nyingi huonekana kuzibeba sana timu za Tanzania kwenye michuano ya kimataifa ya klabu.

Mchezaji aliyeonekana kuwa na kiwango kikubwa kuliko wenzake alikuwa ni Mrundi Yusuph Ndikumana, huku wengine wakiwa hawana jipya la kuisaidia timu.

AS Kigali walianza kulitia msukosuko lango la KMC dakika ya 18 wakati Ndikumana alipookoa kwa kisigino mpira uliokuwa tayari umeshamchanganya kipa Juma Kaseja ukielekea wavuni.

# Yanga yaachiwa mji, Simba waitana Taifa

## ●●● Township Rollers yaikimbia, morali wazidi kupanda, huko Msimbazi wataka uwanja utapike...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Yanga ikitarajia kushuka dimbani Botswana leo kwenye mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wemeendelea kuufurahia mji wa Gaborone baada ya wenyeji wao kuukimbia kwa muda, huku watani zao, Simba wenyewe wakiita mashabiki kuutapisha Uwanja wa Taifa uzi mwekundu kesho.

**Township Rollers mapema wiki hii ilituma maombi Shirikisho la Soka Afrika (Caf) ikiomba mechi hiyo isichezwe Uwanja wa Taifa, Gaborone na badala yake ikachezwe Uwanja wa University of Botswana (UB), ambao unachukua tariban watazamaji 10,000, lakini ilikataliwa kutokana na kuchelewa kutuma ombi hilo.**

Hata hivyo, baada ya kukataliwa ombi hilo huku tayari ikiwa imeutoa ule wa Uwanja wa Taifa, Gaborone kwa Yanga kujifua, ambao mechi itachezwa leo, waliamua kuukimbia mji na kutoa nafasi kwa Yanga kujivinjari bila presha.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, akizungumza jana kuelekea mchezo huo wa leo, alisema wamefurahi kuachiwa mji na kwamba hawana presha ya figisufigisu kutoka kwa wenyeji wao.

"Tunafurahi kwani sasa tunatawala mji kama wenyeji, ingawa hiyo haiwezi kuwa sababu ya kusema tunaweza kushinda, ila hakuna fitina yoyote na leo (juzi) tumewaruhusu wachezaji wetu kwenda kutembea kusoma mazingira ya mji.

"Kocha, Zahera amependekeza hivyo baada ya programu yake ya mazoezi," alisema.

Alisema wachezaji wana ari ya ushindi na juzi walitembelewa na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Simai Mohammed Said, na kuwapa hamasa ya kufanya vizuri kuelekea mchezo wa leo.

Kwingineko kwa upande wa Simba imeendelea kujifua kuelekea mechi yao dhidi ya UD Songo itakayopigwa Uwanja wa Taifa kesho ikiwa ni baada ya ile ya awali ugenini nchini Msumbiji kumalizika kwa sare tasa.

Simba imewaita mashabiki wake kujitokeza kwa wingi uwanjani na kuujaza Uwanja wa Taifa ili kuwapa presha wapinzani wao UD Songo.

Afisa Habari wa Simba, Haji Manyara, kupitia mtandao wake wa Instagram, jana alitoa wito kwa mashabiki wa klabu hiyo si tu kujitokeza uwanjani, bali pia wahakikishe uwanja mzima unatapika jezi nyekundu.

"Jumapili hii (kesho), vaa Kisimba huku mbele tumewava kampuni inayotudhamini!! Unakujaje uwanjani huku hujavaa jezi yako?" Alihoji Manara akiwataka mashabiki wa timu hiyo kuvaa jezi mpya za msimu huu.

Simba inahitaji ushindi wowote ili kusonga mbele katika michuano hiyo na kama ikisonga mbele itakutana na mshindi kati ya FC Platinum ya Zimbabwe na Nyasa Bullets ya Malawi ambayo leo itakuwa ugenini ikisaka matokeo baada ya mechi ya awali kulazimishwa sare tasa nyumbani.

Kwa upande wa Yanga, ikifanikiwa kusonga mbele itakutana na mshindi wa mechi kati ya Green Mamba ya Eswatini na Zesco ya Zambia ambayo leo inahitaji tu kulinda ushindi wake wa mabao 2-0 iloupata katika mechi ya kwanza ugenini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002